SUPA JACKPOT
TZS. 1,056,554,107
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 3

**MWALIMU** jela miaka 20 kwa ukatili dhidi ya wanafunzi wake




UKURASA 13

Nipashe
Jumamosi Desemba 10, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581155
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

## RIPOTI MAALUM

# Familia zinavyogeuza watoto kitegauchumi kupitia ukahaba

UKURASA 4



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akisalimiana na Rais wa Zimbabwe, Emmerson Mnangagwa, walipokutana katika Mkutano wa 10 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Nchi za Afrika, Caribbean na Pacific (OACPS), jijini Luanda, Angola, jana. Majaliwa anamwakilisha Rais Dk. Samia Suluhu Hassan. **PICHA: OWM**

UKURASA WA 7

### SHEHENA YA MAFUTA KUPIKIA YANASWA NJIANI YAKIPELEKWA BANDARI BUBU

JESHI la Polisi Kikosi cha Wanamaji limekamata majahazi matano yakiwa yamebeba shehena ya mafuta ya kupikia yakiwa kwenye madumu 2,352 yenye...

UKURASA WA 9

### DIWANI AWA MBOGO WAJAWAZITO KUTOZWA FEDHA

DIWANI wa Orbomba, Longido mkoani Arusha, Ndiono Laizer, ameishutumu idara ya afya ya halmashauri hiyo, kufumbia macho malalamiko kuhusu...

UKURASA WA 10

### NHC YATANGAZIA KIAMA WADAIWA SUGU

SHIRIKA la Nyumba la Taifa (NHC), limetangaza kiama kwa wapangaji wenye madeni 'sugu' kujiandaa kisaikolojia kuondoka kwa nguvu katika nyumba...

# Nauli treni SGR zapendekezwa

UKURASA 2



Masanja Kadogosa

# Utafiti wataja taasisi 5 zenye shida kimaadili

UKURASA 2

**MICHEZO** SIMBA YAKAMILISHA HESABU KWA EAGLE UK. 32

**KATUNI** UK. 6

# Nauli treni SGR zapendekezwa

**Na Romana Mallya**

SHIRIKA la Reli Tanzania (TRC) limetangaza nauli pendekezwa kwa reli ya kisasa (SGR) kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma, zikianzia Sh. 59,494 kwa daraja la kawaida hadi Sh. 71,392 kwa daraja la kati.

Nauli kwa mtoto wa miaka minne hadi 12 kwa daraja la kawaida kwa ruti hiyo ni Sh. 29,747 na daraja la kati ni Sh. 35,696.

Taarifa iliyotolewa jana na Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano cha Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA), ilibainisha kuwa hayo ni maombi waliyopokea kutoka TRC kuhusu nauli ya treni ya SGR.

Ilibainisha kuwa kutokana na mapendekezo hayo, Desemba 19 mwaka huu, LATRA itaitisha mkutano wa kukusanya maoni ya wadau wa Mkoa wa Dar es Salaam na baadaye watafanya kwa Morogoro na kumaliza na Dodoma.

Mapendekezo mengine yaliyotolewa na TRC kwa safari ya Dar es Salaam-Bahi kwa daraja la kawaida kwa mkubwa ni Sh. 65,894 na mtoto Sh. 32,947 na daraja la kati mkubwa ni Sh. 79,072 na mtoto Sh. 39,536.

Nauli ya Dar es Salaam-Soga kwa daraja la kawaida kwa mkubwa ni Sh. 9,494 na mtoto 4,747 na kwa daraja la kati mkubwa ni Sh. 11,392 na mtoto Sh. 5,696.

"Nauli ya Dar-Ruvu kwa mkubwa kwa daraja la kawaida ni Sh. 14,394 na mtoto 7,197, daraja la kati ni Sh. 17,272 na mtoto Sh. 8,636. Dar-Ngerengere daraja la kawaida kwa mkubwa ni Sh. 19,494 na mtoto Sh. 9,747 na daraja la kati ni Sh. 23,392 na mtoto Sh. 11,696," ilibainisha taarifa hiyo.

Mapendekezo mengine ni Dar-Morogoro kwa daraja la kawaida nauli kwa mkubwa Sh. 24,794 na mtoto Sh. 12,397 na kwa daraja la kati kutoka Dar-Morogoro nauli kwa mkubwa ni Sh. 29,752 na mtoto Sh. 14,876.

Mapendekezo mengine ni Dar-Mkata kwa daraja la kawaida kwa mkubwa Sh. 30,194 na mtoto Sh. 15,097 na daraja la kati ni Sh. 36,232 na mtoto Sh. 18,116.

"Nauli ya Dar-Kilosa kwa daraja la kawaida kwa mkubwa Sh. 35,694 na mtoto Sh. 17,847 na kwa daraja la kati kwa mkubwa ni Sh. 42,832 na mtoto Sh. 21,416.

"Daraja la kati kwa safari ya Dar-Kidete kwa mkubwa wamependekeza iwe Sh. 49,672 na mtoto Sh. 24,836 na daraja la kawaida kwa mkubwa 41,394 na mtoto Sh. 20,697.

"Daraja la kawaida Dar-Gulwe kwa mkubwa Sh. 47,294 na mtoto Sh. 23,647 na kwa daraja la kati nauli inayopendekezwa kwa mkubwa ni Sh. 56,752 na mtoto Sh. 28,376.

"Dar-Igandu kwa daraja la kawaida nauli iliyopendekezwa kwa mkubwa ni Sh. 53,294 na mtoto Sh. 26,647 na kwa daraja la kati kwa mkubwa ni Sh. 63,952 na mtoto Sh. 31,976," ilibainisha taarifa hiyo.

Kwa upande wa nauli za awali za kuanzia kutoa huduma kituo kwa kituo zilizopendekezwa na TRC kwa Dar-Pugu kwa daraja la kawaida kwa mkubwa Sh. 4,694 na mtoto Sh. 2,347 na daraja la kati kwa mkubwa ni Sh. 5,632 na mtoto 2,816.

Akizugumza na Nipashe jana kuhusu nauli hizo, Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Habibu Suluo alisema uchukuaji wa maoni kwa wananchi watautekeleza ndani ya siku 90 (miezi mitatu).

"Tuna wataalamu wa uchumi wa kuangalia hizi gharama za uendeshaji, na tunajua SGR inajengwa kwa kodi za Watanzania, tunajua namna ya kuliendesha.

"Lakini, lazima tuwaambie wananchi TRC wanataka kufanya nini, sisi ni marefa tunakuwa katikati, tunasikiliza na kufanya uchambuzi na kupeleka ngazi za serikali," alisema.

**WADAU WAFUNGUKA**

Aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Francis Nanai alisema bei zote zinazotangazwa zinapaswa kuakisi maisha halisi ya watu na si vinginevyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga alisema nauli zinapaswa kuwa nafuu ili kuwawezesha wasafiri kutumia usafiri huo waliokuwa wakiusubiri kwa muda mrefu.

Mfanyabiashara na Mkazi wa Dodoma, Judith Petro alisema mradi wa SGR umetekelezwa kwa fedha za wananchi, hivyo ni lazima bei zake ziendane na maisha ya kila mtanzania.

Novemba 7 mwaka huu, Mkurugenzi wa TRC, Masanja Kadogosa wakati wa hafla ya utiaji saini wa mkataba wenye thamani ya dola za kimarekani milioni 51 kati ya TRC na kampuni ya Sung Shin Rolling Stock Technology (SSRST) kutoka Korea Kusini, alisema safari za SGR kilometa 300 kati ya Dar es Salaam na Morogoro zinatarajiwa kuanza mwezi Februari mwakani.




Naibu Spika wa Bunge, Mussa Azzan 'Zungu', akizungumza wakati akizindua kitabu cha muongozo wa kuepukana na magonjwa yasiyoambukiza, katika viwanja vya Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), Muhimbili, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Peter Kisenge. **PICHA: PILLY KIGOME**

## Ahukumiwa kunyongwa kuua mtoto wa mkewe

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Tabora imewahukumu kunyongwa hadi kufa watu watatu waliokuwa wanakabiliwa na kesi mbili tofauti za mauaji, akiwamo aliyemuua mtoto baada ya kumkuta mama yake anatumia vidonde vya kupunguza makali ya Virusi vya Ukimwi (ARV).

Waliopewa adhabu hiyo ni Haruna Ndayanze, mkazi wa Kijiji cha Pozamoyo, Wilaya ya Kaliua aliyeua mtoto wa mkewe; Allya Shaban na Ally Mtoni Kambogo, wote wakazi wa Kijiji cha Igalula, Wilaya ya Uyui mkoani Tabora.

Adhabu hiyo ilitolewa juzi na Demetrio Nyakunga, Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Wilaya ya Tabora aliyekasimiwa mamlaka ya ziada ya kusikiliza mashauri ya Mahakama Kuu.

Katika shauri la kwanza, mahakama imemhukumu kunyongwa hadi kufa Haruna Ndayanze baada ya kumtia hatiani kwa kumuua Kusaga Magulu ambaye alikuwa mtoto wa mkewe aliyezaa na mwanamume mwingine.

Upande wa mashtaka, ukiwakilishwa na Mawakili Mwerito Ukongoji na Sabrina Silayo, ulidai mahakamani kuwa mshtakiwa alitenda kosa hilo Januari 25, 2020 katika Kijiji cha Pozamoyo wilayani Kaliua.

Ilidaiwa kuwa siku hiyo, mshtakiwa alitimiza nia hiyo ovu kwa kumkata kwa panga shingoni na mikononi mtoto wa mkewe aliyefahamika kwa jina la Kusaga Magulu.

Upande wa mashtaka uliopeleka mashahidi 12, ulidai sababu za mauaji hayo ni kutokana na mshtakiwa kumkuta mkewe, Stephania Alphoncy akimeza vidonge vya kupunguza makali ya virusi hivyo.

Hakimu Nyakunga aliwahukumu kunyongwa washtakiwa hao baada ya kuwakuta na hatia ya mauaji.

Katika hatua nyingine, Mahakama Kuu Kanda ya Tabora imemwachia huru Zengo Kulwa, mkazi wa Kijiji cha Izugawima wilayani Uyui aliyekuwa akituhumiwa kumua Joseph Elias, kutokana na kukosekana ushahidi wa kutosha kumtia hatiani.

# Maeneo matano yenye shida kimaadili yaanikwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MATOKEO ya utafiti wa hali ya uzingatiaji maadili katika utumishi wa umma kwa mwaka 2022 umeonyesha maeneo matano vinara wa vitendo visivyo vya kiadilifu.

Maeneo hayo yaliyolalamikiwa zaidi kwa kukithiri vitendo hivyo ni Jeshi la Polisi, Mahakama, ununuzi wa umma, mikataba na huduma za ardhi.

Hata hivyo, kiwango cha uzingatiaji wa maadili katika utumishi wa umma kwa mwaka huu kimeongezeka hadi kufikia asilimia 75.9 kulinganishwa na mwaka 2014 ambao kiwango kilikuwa asilimia 66.1.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora, Jenista Mhagama akitangaza jana matokeo ya utafiti huo jijini hapa, alisema maeneo hayo yaliyolalamikiwa yanashabihiana na matokeo yaliyotolewa katika utafiti wa kitaifa kuhusu rushwa, ulioendeshwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mwaka 2020.

"Utafiti huo pia ulibainisha kati ya taasisi zinazolalamikiwa kwa rushwa ni pamoja na Jeshi la Polisi, mahakama na usimamizi wa ardhi," alisema.

Waziri huyo alisema kuna maeneo yanahitaji kuboreshwa au kutiliwa mkazo ikiwamo ufuatiliaji wa kila mara wa uzingatiaji wa kanuni za maadili kwa watumishi wa umma.

"Kuna haja kuwa na mafunzo endelevu kwa watumishi ambao wako kazini, wale wanaoajiriwa kwa mara ya kwanza na elimu kwa umma na usimamizi wa uzingatiaji wa maadili katika utoaji wa huduma wakati wa majanga ya kitaifa kama vile UVIKO-19," alisema.

Kuhusu kiwango cha uzingatiaji wa maadili, waziri huyo alisema kimeongezeka kwa wastani wa asilimia 9.8 kwa mwaka 2022.

"Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha juhudi za serikali za kuchukua hatua mbalimbali za kuweka misingi imara ya usimamizi wa maadili, kuweka mazingira wezeshi na kuimarisha uwajibikaji katika utumishi wa umma," alisema.

Alimwagiza Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo kufanya kikao kazi cha pamoja na wadau kwa ajili ya kufanya majadiliano ya kina kuhusu matokeo ya utafiti huo na kuja na mikakati ya ufuatiliaji wa uzingatiaji wa maadili katika sekta zote kulingana na matokeo.

"Waajiri wahakikishe wanatenga bajeti ya mafunzo ya maadili na kuendesha mafunzo kwa watumishi wa umma walio kazini na wale wanaoajiriwa.

"Waajiri pia wanaweka na kuimarisha mifumo ya utoaji wa mrejesho ndani ya taasisi zao ili kuendelea kutoa fursa kwa wananchi kukemea vitendo vya ukiukwaji wa maadili," alisema.

## HABARI KITAIFA

# Mwalimu jela miaka 20 kwa unyanyasaji watoto

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Mufindi imemhukumu kifungo cha miaka 20 jela Jalio Mtanga (53) ambaye ni mwalimu wa Shule ya Msingi Nyololo baada ya kutiwa hatiani kwa makosa saba ya ukatili mkubwa wa kijinsia aliowafanyia wanafunzi saba wa shule hiyo.

Mwalimu huyo amehukumiwa baada ya ushahidi kuthibitisha kufanya kosa la ukatili mkubwa wa kijinsia ambalo ni kinyume cha kifungu cha 138 C cha Sheria ya Kanuni za Adhabu.

Ilidaiwa mahakamani hapo kuwa mshtakiwa huyo kwa nyakati tofauti, aliwafanyia ukatili huo watoto wa shule hiyo wenye umri kati ya miaka 10 na 16 ambao alikuwa akiwarubuni kwa kuwaambia wakusanye madaftari na kisha kupeleka ofisini kwake ambako ndiko alikuwa akitekeleza unyama huo.

Wakili wa Serikali Twide Mangula baada ya mshtakiwa kutiwa hatiani, aliiomba mahakama hiyo itoe adhabu kali kutokana na kukithiri kwa vitendo hivyo huku waathirika wakubwa wa vitendo hivyo wakiwa watoto wa kike.

Akisoma hukumu, Hakimu Mkazi Mwandamizi, Benedict Nkomola alisema kutokana na ushahidi uliotolewa mahakamani hapo, Mtanga anastahili kifungo hicho ili iwe fundisho kwake na jamii kwa ujumla.

Mshtakiwa alipopewa nafasi ya kujitetea, aliiomba mahakama impunguzie adhabu kwa kuwa ana familia inayomtegemea.

Hata hivyo, mahakama ilitupilia mbali maombi hayo na kumhukumu kutumikia kifungo hicho jela.



Makamu wa Rais wa Kampuni ya Mafuta na Gesi ya Equinor Norway, Nina Koch (kushoto), akijadiliana jambo na Waziri wa Nishati, January Makamba, walipokutana kwa mazungumzo kuhusu utekelezaji wa mradi wa kuchakata na kusindika gesi asilia (LNG) mkoani Lindi, jijini Dodoma juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NIT yajizatiti uzalishaji wa wataalamu usafiri wa anga

**Na Mwandishi Wetu**

CHUO cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kimeadhimisha Siku ya Kimataifa ya Usafiri wa Anga Duniani (ICAD) huku kipaumbele kikubwa kikiwa ni kuzalisha rasilimali watu ya kutosha ili kukidhi mahitaji katika sekta hiyo yenye upungufu mkubwa wa wafanyakazi wazawa.

Akizungumza katika Kampasi Kuu ya chuo iliyoko Mabibo mkoani Dar es Salaam wakati wa maadhimisho hayo juzi, Mkuu wa Shule Kuu ya Anga na Teknolojia, Deniss Mwageni alisema:

"NIT kama mdau mkubwa wa sekta ya usafiri wa anga, tunaadhimisha siku hii ya kimataifa ya usafiri wa anga duniani tukihakikisha tunaendelea kutoa mafunzo bora na stahiki yanayokidhi mahitaji ya sekta hii.

"Sekta hii ya anga nchini na duniani imekuwa ikihangaika kupata rasilimali watu ya kutosha, hivyo ni wajibu wetu kama taasisi kuhakikisha tunazalisha wahitimu wa kutosha kwenda kupunguza tatizo hili.

"Kwa sasa, mahitaji wa sekta ya anga kwa upande wa marubani pekee ni 1,898 ambapo kwa sasa tunao marubani 1,248. Kati yao, wazawa ni 608 na wageni ni 640. Na mpaka kufika mwaka 2025, mahitaji yatakuwa marubani 2,523."

Alisema kuwa ili kutatua tatizo la uhaba wa marubani, NIT iko katika hatua za mwisho za kuanza kufundisha kozi hiyo, tayari ikiwa imeshapata ndege mbili za mafunzo kwa msaada wa serikali.

Pamoja na hayo, Mkuu huyo Shule Kuu ya Anga alisema katika maeneo mengine, NIT imepata ithibati za mafunzo ya kozi mbili za usafiri wa anga (kozi za uhandisi wa matengenezo ya ndege pamoja na uendeshaji wa safari za ndege) kutoka Mamlaka ya Usafiri wa Anga ya Tanzania (TCAA).

"Upatikanaji wa ithibati hizi ni ishara tosha kuwa chuo chetu sasa kimeshafikia viwango vya kimataifa ambavyo vinahitajika katika uzalishaji wa wahandisi wa matengenezo ya ndege.

"Ni imani yetu kuwa uhaba wa wahandisi hawa utakuwa historia baada ya miaka michache ijayo," alisema Mwageni na kubainisha kuwa kwa sasa chuo kinaendelea na ujenzi wa majengo matano yanayojengwa katika kampasi kuu mkoani Dar es Salaam kupitia mradi wa Benki ya Dunia wa EASTRIP.

Alisema majengo mengine ambayo yanajengwa ni pamoja na majengo manne kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA).

Alisema katika kuhakikisha chuo kinakuwa na wakufunzi wa kutosha na wenye vigezo vinavyokubaliwa na TCAA, chuo kimewapeleka wakufunzi 13 nje ya nchi kuongeza ujuzi kwenye eneo la mafunzo ya anga.

"Tumepeleka wakufunzi wawili Marekani huku wakufunzi sita wakienda Ethiopia, wawili Uingereza, watatu wakienda Afrika ya Kusini na mmoja ameshahitimu na wengine kadhaa wamekwenda China.

"Vilevile, tupo kwenye mchakato wa maongezi na Shirika La Kimataifa la Usafiri wa Anga Duniani (IATA) na ICAO ili kuhakikisha mitihani ya leseni za kimataifa zinazotolewa na mashirika hayo zinafanyika chuoni hapa.

"Kwa namna ya pekee niwashukuru Benki ya Dunia kwa kufadhili kituo chetu cha umahiri ambacho ni cha muhimu sana kwa ustawi wa sekta ya uchukuzi na sekta ndogo ya usafiri wa anga nchini," alisema.

Kiongozi huyo alisema NIT ni moja ya vyuo vinne nchini vinavyotekeleza mradi huo wa kikanda kwa kuanzisha Kituo cha Umahiri cha Mafunzo ya Taaluma za Usafiri wa Anga na Operesheni za Usafirshaji (CoEATO).

# Wafungwa wapewa msaada wa magodoro siku ya Uhuru

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

UONGOZI wa Wilaya ya Singida kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo umetoa magorodo 74 na mablanketi 143 kusaidia wafungwa na mahabusu katika Gereza la Wilaya ya Singida ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Miaka 61 ya Uhuru wa Tanzania Bara.

Vifaa hivyo vilikabidhiwa jana na Mkuu wa Wilaya ya Singida, Paskas Mulagiri kwa Mkuu wa Gereza hilo, Mohammed Ng'anzi.

Mulagiri aliwashukuru wadau waliosaidia kutoa vifaa hivyo na kuwataka wengine wajitokeze kusaidia makundi mengine ya watu wenye uhitaji ambao wanakabiliwa na kero mbalimbali.

Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Dorothy Mwaluko, akiwasilisha mada ya uzalendo, amani na tunu za taifa katika mdahalo wa kuadhimisha Miaka 61 ya Uhuru, alisema kwa sasa kuna mmomonyoko mkubwa wa maadili, hasa kwa vijana waliozaliwa kuanzia miaka ya 1970.

"Watoto wetu ambao ndiyo tunasema ni taifa la kesho hawajui uzalendo, hawajui lipi zuri na lipi baya, vijana wengi wanaiga mambo ya ovyo tu na wanaitumia vibaya teknolojia," alisema.

Mwaluko pia alionyesha kuchukizwa na watumishi wa umma kwa kutohudhuria mdahalo huo uliofanyika Chuo cha Uhasibu Singida.

Alisema katika ofisi ya mkoa kuna watumishi 99 lakini ni mmoja tu aliyehudhuria mdahalo huo, watumishi wa Halmashauri ya Manispaa walikuwa wanane wakati wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida walikuwa 10.

"Pale sekretarieti ya mkoa nina wafanyakazi 99 lakini leo hapa yupo mmoja, ndiyo muone huu uzalendo tunaouzungumza upo wapi, " alisema huku akiwasimamisha wafanyakazi wa Manispaa ya Singida na wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida ambao walionekana wachache.

Mkuu wa Wilaya ya Singida, Mulagiri, akifungua mdahalo huo, alisema tangu uhuru hadi sasa yapo maendeleo makubwa yamefanyika nchini.

Asimilia kubwa ya watanzania wapo chini ya umri wa uhuru wetu, hivyo huenda huko nyuma hawajui hali ilivyokuwa na hivyo wanakuwa wanalalamika tu kuwa serikali hajafanya kitu wakati sio kweli, mambo mengi ya maendeleo yamefanyika," alisema.

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**Probate and Administration Cause No.175 of 2022**

**In the matter of the Estate of the late PIUS ALANUS MHUSU Of Kizota within Dodoma City**

**And**

**In the matter of an application for letters of administration by OSWAD MWAJOMBE.**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

All PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 09 Day of 01, 2023

**Dated at Dodoma this 07 day of 12, 2022**

RESIDENT MAGISTRATE

RIPOTI MAALUM

# Familia zinavyowageuza watoto kitega uchumi kupitia ukahaba

## •Ni sura nyingine ya ukatili wa kijinsia nchini

Na Halfani Chusi

"UJIANDAE utoke mapema leo, hatujui jioni tutakula nini. Hela uliyokuja nayo juzi imeisha, jitahidi leo urudi na hela mwanangu," mama mwenye umri wa makamo anasikika akitoa maelekezo kwa binti yake.

Ni majira ya saa 10 jioni, maeneo ya Mwananyamala wilayani Kinondoni mkoani Dar es Salaam, Nipashe inashuhudia aina nyingine ya ukatili dhidi ya watoto, safari hii ukifanywa na mzazi dhidi ya mwanawe.

Mama huyo (jina tunalo) anaendelea kutoa maelekezo kwa bintiye huyo, akitamka: "Baba yako akiniuliza umeenda wapi, nitamwambia 'nimemtuma kwa shangazi yake Kibiti', na wewe akikupigia simu umweleze hivyo hivyo, sawa mwanangu?

"Lakini usisahau khanga ya kujitanda unapokaribia kufika hapa nyumbani wakati wa kurudi ili hata akikuona, asije kujua kinachoendelea".

Mara moja Nipashe inaamua kufuatilia nyendo za binti huyo na kujiridhisha ana umri wa miaka 16 na amekuwa akitumikishwa kingono na mama yake mzazi ili kupata fedha za kukidhi mahitaji ya familia.

Inapotimu saa moja jioni, mwili wake akiwa ameutanda kwa khanga, binti huyo (jina tunalihifadhi) anaondoka nyumbani kwao Mwananyamala kwenda maeneo maarufu kwa starehe wilayani Kinondoni kusaka wateja.

Mara moja Nipashe inabaini maeneo hayo yana idadi kubwa ya wanawake wanaojihusisha na biashara ya ngono, wengi wao kimwonekano ni mabinti wenye umri mdogo na hata watoto.

Vilevile, ni mandhari yenye baridi kali, usalama mdogo wa mali za wasio wenyeji wa maeneo hayo huku mbu wakitawala makazi.

Majira ya saa nne usiku, akiwa pembeni mwa barabara inayopita karibu na klabu ya usiku wilayani Kinondoni, binti huyo anakunja khanga yake na kuiweka kwenye mkoba mdogo aliokuwa nao tangu alipoanza safari yake nyumbani Mwananyamala na kubaki na nguo za kusitiri maeneo maalum tu.

Nipashe iliyoguswa na mkasa huo, inashuhudia binti huyo akimfuata mmoja wa wanaume wanaoingia ndani ya klabu hiyo na kumkaribisha kwa rejesta ya mahali hapo, akimshika mkono wa kushoto na kusema:

"Karibu kaka nikuhudumie, umependeza! Tena wewe bonge nitakuboreshea huduma! Nina bei mbili - ya kinga na ya bila kinga. Ya kinga bei ndogo, bila kinga bei kubwa."

Baada ya mazungumzo mafupi, wawili hao wanaelewana na kuondoka eneo hilo kwenda wanakokojua kutimiziana haja zao za kimwili.




**USHUHUDA WA BINTI**

Asubuhi siku inayofuata, Nipashe inazungumza na binti huyo, akikiri familia yake kumtegemea katika kukidhi mahitaji, hasa chakula.

"Maisha yetu ni magumu sana, baba yangu ni teja (mraibu wa dawa za kulevya), mama yangu ndo hivyo hivyo, hajiwezi kabisa kiuchumi na mimi nimekatisha masomo yangu nikiwa darasa la sita kutokana na hali duni ya maisha," anasema.

Hata hivyo, ugumu wa maisha si sababu ya kuhalalisha vitendo hivyo kwa kuwa vinakinzana na Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 na mikataba ya kimataifa kuhusu haki za watoto ambayo Tanzania imeiridhia ukiwamo Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto (CRC) wa Mwaka 1989 na Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto (ACRWC) wa Mwaka 1990, yote ikizuia utumikishwaji wa watoto.

Binti huyo anaendelea na simulizi yake kwa Nipashe, akiwasilisha: "Kuna siku tunalala njaa, hapo mama sasa analazimisha niende nikadange (kufanya biashara ya ngono) lakini kwa kumficha baba asijue, mama huwa ananipa mbinu za kumfanya baba asijue kinachoendelea.

"Kuna muda unakutana na wahuni wanakuibia hata hicho kidogo ulichopata lakini wakati mwingine unatoka na mwanamume, baada ya kumaliza haja zake hatoi fedha.

"Kuna muda mwingine unakubaliana na mwanamume mtumie kinga, lakini mkifika guest (nyumba ya kulala wageni) anakugeuka, hataki kuvaa kinga, anakulazimisha kufanya hivyo hivyo wakati hamjapatana kwa bei ya kufanya bila kinga.

"Shida nyingine hutokea pale unapokutana mwanamume ambaye ametumia dawa za kuongeza nguvu za kiume, kumhudumia inakuwa shida kwa sababu mara nyingi kunatokea mchubuko unaosababisha maumivu makali.

"Kuna wakati unapatana na mwanamume, mkishafika eneo la tukio anakulazimisha kukuingilia kinyume na maumbile. Ukikataa anakutolea kitu cha kutisha kama bastola au kisu, mradi tu afanikishe haja yake.

"Kingine, unapatana na mwanamume mmoja lakini ukishafika naye eneo la kukutana kimwili, unavamiwa na wanaume zaidi ya watano na wote wanataka kufanya na wewe, wanapanga dili la kufanya hivyo, nimeshuhudia wenzangu wengi linawatokea hilo," anasimulia.

Nipashe inapohoji hali ya maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU), binti huyo anasema hana uhakika kama yuko salama ama la kwa kuwa hajapima afya yake.

**KAULI YA WAZAZI**

Nipashe inaingia sebuleni kwa mama mzazi wa binti huyo kupata undani wa madhila dhidi ya mwanawe.

Pasi na kujua Nipashe ina ushuhuda wa kina kuhusu kinachoendelea, mama huyo anayevuta sigara, anakana kumtumikisha kingono mwanawe, akisema:

"Hakuna ukweli wowote, hapa nyumbani kila mtu ni mpambanaji. Kama yeye (binti yake) anafanya mambo hayo, ni juu yake. Hata akidanga, atajua mwenyewe, na wewe mwandishi ushaanza 'chimbuchimbu' (udadisi) zako, nipishe mie niendelee kuvuta sigara yangu."

Hata hivyo, majibu ya mama huyo anayekiri kutojali makuzi ya mwanawe huyo, yanakinzana na Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 inayoelekeza wazazi na walezi kuwalinda watoto dhidi ya vitendo vyote vya ukatili.

Nipashe pia inazungumza na baba wa binti huyo (jina tunalo) ambaye anadai kutokuwa na taarifa za mwanawe kutumikishwa kingono, akiahidi kufuatilia nyendo zake.

ITAENDELEA KESHO

TANGAZO

SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR
SHIRIKA LA BIMA LA ZANZIBAR (ZIC)

# Mafanikio ya ZIC na miaka 61 ya uhuru

**WAKATI Tanzania inatimiza miaka 61 ya uhuru wa Tangayika, Shirika la bima Zanzibar (ZIC) limeongeza ufanisi katika utendaji wake wa kazi.**

Shirika hilo linashirikiana na wadau mbalimbali na kuondokana na utaratibu wa kufanya biashara kwa kusubiri kufikiwa na badala yake linawafuata wateja walipo ili kutambua mahitaji yao.

Katika kuwafikia wateja shirika limefungua matawi yake katika mikoa mbalimbali ya Tanzania ikiwemo Dar es salaam, Arusha, Tanga, Mbeya, Mtwara, Dodoma, Mwanza na Shinyanga.

Mkurugenzi mwendeshaji wa shirika hilo Nd.Arafat Ali Haji, anasema hali hiyo inaongeza imani kwa wateja juu ya shirika hilo na imekuwa ndiyo chachu ya mafanikio ya shirika hilo kongwe la bima linalomilikiwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Lengo la kufanya kazi pamoja na taasisi za kibenki na Mitandao ya simu ni kuongeza mapato ya shirika hilo na kupunguza utegemezi wa kupata biashara kutoka sehemu moja.

Nd. Arafat amesema kutokana na wingi wa wawekezaji wanaofika visiwani Zanzibar, shirika hilo limejipanga kutoa huduma kwa wawekezaji kutoka nchi mbali mbali ili waweze kuwekeza na kulinda uwekezaji wao kwa kukata bima zinazotolewa na ZIC.

Shirika hilo limeanzisha bidhaa ambazo zitawapa unafuu watalii watapokuwa Zanzibar. Mtalii akikata bima ya safari shirika hilo linamuhakikishia atakapopata dharura yoyote iwe ya kiafya, msiba au kupoteza vitu vyake shirika la bima litamuhakikishia usalama wa mali zake.

Anasema hatua hiyo inawahakikishia watalii wanaofika Zanzibar kuwa salama na kuwapa imani wanatembelea eneo sahihi hasa ikizingatiwa kuwa utalii ni sehemu kubwa ya ajira kwa wazanzibari na watanzania.

Nd. Arafat anasema katika kuunga mkono jitihada za Serikali, Shirika la bima la Zanzibar linahakikisha watalii wanabaki salama na idadi yao kuongezeka ili kuongeza ukusanyaji wa kodi na kasi ya ukuaji wa uchumi wa Zanzibar.



*Mkurugenzi Mwendeshaji wa Zanzibar Insurance Corporation muda mfupi baada ya kupokea tuzo katika hafla ya upokeaji tuzo za wakurugenzi/watendaji bora 100 kwa mwaka 2022*

Mipango ya shirika hilo ni kuwekeza katika majengo ya kibiashara ili kuongeza thamani ya shirika na ukubwa wa mtaji wa kutoa huduma kubwa zaidi.

Akizungumzia changamoto ya urasimu wa ulipaji wa fidia kwa wateja wa bima, Mkurugenzi huyo anasema utaratibu wa sasa umebadilika na ndani ya siku 10 wateja wao wanauhakika wa kulipwa fidia baada ya kupata majanga na kulipwa kinachostahiki.

Anasema katika kulitekeleza hilo pia wanakumbana na changamoto ya madai hewa ambayo yanatengenezwa kwa lengo la kujipatia fedha.

Mkurugenzi huyo anasema, matarajio ya shirika katika kuongeza utoaji wa huduma linakusudia kubuni bidhaa mpya zitakazoendana na mahitaji ya wateja wake.

# MAADHIMISHO YA MIAKA 61 YA UHURU



*Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi*
*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi*






*Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan*
*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*

Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Shirika la bima Zanzibar **(ZIC)** tunaungana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mhe. Dr.Samia Suluhu Hassan n**a Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar **Mhe**. **Dr. Hussein Ali Mwinyi** na Watanzania wote katika kusherehekea Maadhimisho ya **Miaka 61** ya Uhuru wa Tanzania. **1961 - 2022**

***Uhuru Wetu ni Tunu Yetu, Tuulinde Tuutunze na Tuuheshimu***

61 MIAKA **YA UHURU**

**HEAD OFFICE;**
**(Maisara) Mpirani, P.O.Box:432, Zanzibar, Tel:+255 24 2232676 / 2233867 /2239504**
**Fax: +225-24 2232422, Email: zichq@zic.co.tz**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maboresho yahitajika zaidi katika viwanja vya michezo

**ILI** wanamichezo wafanye vizuri katika mashindano mbalimbali wanayoshiriki ndani na nje ya nchi, ni lazima wawe wamefanya maandalizi katika viwanja vyenye ubora unaohitajika kulingana na mahitaji ya mchezo husika.

Mchezaji au timu inayofanya mazoezi kwenye uwanja wenye sifa, huchangia kukuza kipaji na ubora wake, na mwisho wa siku, matokeo chanya yanayotarajiwa hupatikana.

Huwezi kuona timu inafanikiwa kwa kutofanya maandalizi yake kwenye viwanja vyenye sifa zinazostahili, na endapo ikatokea hivyo, basi itakuwa imebebwa au wamebebwa na neno bahati.

Ni kweli bahati huchukua nafasi katika michezo kwa sababu katika upande wa soka tumewahi kushuhudia timu inayotawala mpira kwa muda mrefu, ikashindwa kufunga mabao pale wanapotengeneza nafasi, na mpinzani wake akawa makini kwa kutumia vyema nafasi moja au mbili ilizopata, ikaibuka na ushindi.

Idadi kubwa ya timu zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, hazija viwanja vyake binafsi, baadhi hutumia viwanja vya kukodi vinavyomilikiwa na taasisi mbalimbali na klabu nyingine zenyewe hutumia viwanja vya shule, hali ambayo husababisha kusimama kwa programu za mazoezi pale wamiliki wanapokuwa na shughuli zao binafsi, au wanapokuwa wametoa ruhusa kwa watu wengine kutumia viwanja hivyo.

Hongera kwa Azam FC, Ihefu SC, JKT Tanzania, Mtibwa Sugar, Fountain Gate Academy, Gwambina FC na wengine ambao wamejaribu kujenga viwanja vyao kwa ajili ya kutumia kwenye michezo yao ya nyumbani.

Wakati kukiwa na kanuni maalumu inayozitaka timu zinazoshiriki kuwa na viwanja vyake, kanuni hiyo ikiwa na zaidi ya miaka mitano sasa, bado zipo klabu zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara au Ligi ya Championship, zikiwa hazina hata uwanja wa mazoezi, hali ya kuwa biashara yake kubwa ni kucheza mpira. Ni ngumu kwa timu kupata mafanikio wakati mambo ya msingi ambayo yamekuwa yakinadiwa na viongozi pale wanapokuwa kwenye kampeni wakijinadi watajenga viwanja, wengine wakidiriki kutaja na siku atakazoleta mabadiliko, kwa kukosa kitendea kazi muhimu.

Kama Ihefu na Gwambina zimeweza kujenga uwanja, kwa nini timu nyingine zinashindwa kupambana kuhakikisha zinapata miundo mbinu hiyo na kujiondoa katika gharama ya kulipia viwanja vya kukodi?

Umefika wakati viongozi waliopewa dhamana ya kuzisimamia klabu hizi wakatimiza ndoto za wanachama na mashabiki wao kwa kuacha alama siku watakayoondoka, kwa kujenga viwanja ambavyo vitasaidia kuendeleza wachezaji wao kuanzia wa timu za watoto hadi wakubwa, alama ambayo itabakia kwenye vitabu vya kumbukumbu vya klabu hiyo husika kwa muda wote. Pia tunalikumbusha Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kukaa tena na wadau wanaomiliki viwanja kuingia mikataba maalumu itakayosaidia timu au shirikisho hilo kufanya matengezo yatakayosaidia kuboresha viwanja husika na kutimika kwa michezo yote.

Kukosekana kwa viwanja bora mikoani, kunawanyima haki mashabiki wa timu husika kuzishangilia na kuwashuhudia wachezaji wao mubashara wanapocheza na badala yake, timu hulazimika kuhamia kwenye kiwanja kingine kilichoko mkoa wa jirani kucheza mechi zake za nyumbani.

Mbali na kupoteza haki ya kuwa nyumbani, lakini timu hukosa mapato kwa sababu huonekana kama mwenyeji naye yuko ugenini, tukae chini upya tufanyie kazi utekelezaji wa maboresho ya viwanja kwa vitendo na si kutoa taarifa za kufungia viwanja.

Huku umaarufu wa mchezo wa ngumi ukirejea kwa kasi, bado hali imekuwa ni mbaya kwa mabondia wa hapa nchini kufanya mazoezi katika maeneo ambayo si rasmi ambayo hayawasaidii kwenye kujiimarisha vizuri. Lakini mazingira hayo hayavutii kupata mabondia chipukizi kwa sababu ya uchakavu wa vifaa au maeneo ambayo hutumika kujifua.

Tatizo hili pia liko kwa wanariadha, hawa ndio wanakosa sehemu sahihi za kufanyia mazoezi kulingana na mchezo wanaoshiriki, ama wanafanyia mazoezi barabarani au kwenye sakafu ambazo hazina ubora unaotakiwa kufuatana na mchezo wao.

Bila miundo mbinu sahihi, bado safari ya mafanikio kwa wanamichezo nchini itaendelea kuwa ngumu hata kama watapata makocha na vifaa vyenye ubora.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Timu ndogo 'zisinyongwe' mashindano Kombe la FA

**LIGI** Kuu imesimama wiki hii kupisha mashindano ya Kombe la Shirikisho la Soka Nchini (TFF), maarufu kama Kombe la FA, ambalo husaka bingwa atakayeiwakilisha Tanzania Bara katika michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Tofauti na Ligi Kuu ambayo mpaka timu ipande daraja, michuano hii inazishirikisha kuanzia madaraja ya chini kuliko hata za juu.

Karibuni kila mwaka huwa tunaona kuna baadhi ya timu za madaraja ya chini zinajitutumua wakati mwingine kufanya maajabu kwenye michuano hii, ikiwa ni pamoja na kuwaangusha wakongwe, lakini mbele ya safari zinatolewa kutokana na kukosa uzoefu pamoja na viwango vidogo vya wachezaji wao.

Ofisa Habari wa TFF, Clifford Ndimbo, amewataka mashabiki wa soka walio karibu na maeneo ambayo michuano hiyo inachezwa kujitokeza kwa wingi kwenda kuangalia mechi hizo.

Ndimbo aliongeza tayari wameshawapa semina waamuzi kwa ajili ya kuwapiga msasa ili pamoja na mechi zingine, lakini wachezeshe kwa haki na kwa viwango vinavyotakiwa michuano ya Kombe la FA.

Licha ya kuwa waamuzi wamekuwa wakifanya makosa mengi yanayoitwa ya kibinadamu hata kwenye Ligi Kuu, lakini hatutarajii sasa kuona yanajirudia katika michuano hiyo hasa kwa timu ndogo ambazo ndizo zinajitutumua.

Kuna dhana timu ndogo zinajaza kwani hata kama zikisonga mbele hazina uwezo wa kucheza michuano yoyote ya kimataifa, si kwa viwango tu bali hata uwezo wa kumudu kusafiri.

Kwa maana hiyo baadhi wanaona kama zifanyiwe njama, zifungwe zibaki timu zenye uwezo zitakazoweza kumudu kusafiri kwenda nje ya nchi.

Huu utakuwa ni uonevu mkubwa. Waamuzi wanatakiwa kuchezesha kwa haki bila kuzibeba timu kubwa, kongwe, zenye uwezo wa kifedha, au za Ligi Kuu dhidi ya timu ndogo.

Ushindi unatakiwa uende kwa timu zilizojipanga vema kwenye mechi husika na si kuangalia jina la timu.

Hii ni michuano ambayo pia huleta wachezaji wapya kwenye tasnia ya soka nchini kutoka mitaani na kusajiliwa kwenye timu mbalimbali za Championship na Ligi Kuu Tanzania Bara.

Ndiyo michuano iliyobaki kuwapata wachezaji chipukizi, wenye vipaji ambavyo vimejificha badala ya Kombe la Taifa ambalo kwa sasa halipo na kama lipo halina umaarufu kama zamani.

Na kwa kuwa ni kipindi cha dirisha dogo, timu za Ligi Kuu ukiondoa labda Simba, Yanga na Azam, zinaweza zikawaona baadhi ya wachezaji ambao wanaweza kuwaongeza kwenye vikosi vyao.

Kutokana na hilo nawaomba tu waamuzi wachezeshe kwa haki ili tuone vipaji murua, badala ya 'kuzinyonga'.

Timu ndogo inaweza kuwa na wachezaji wazuri, lakini kutendo cha kutoichezesha kwa haki kinaitoa timu hiyo mapema wakati watu walitaka kutazama tena uwezo wa wachezaji, kinaweza kuwakera na kuwapa msongo wa mawazo wachezajivijana wakaona kumbe soka si mchezo wa haki unaoweza kuwapa maendeleo, hivyo kuamua kuachana nao wakaenda kufanya kazi zingine.

Ni ukweli usiopingika kuwa wapo wachezaji wengi vijana wameachana na soka kutokana na tabia ya waamuzi kuzionea timu zao, wakati wao wanataka kuonekana na 'kutoka', lakini wanabaniwa kwa kutochezeshwa kwa haki.

Afadhali kwenye Ligi Kuu na Ligi ya Championship, kuna wachezaji wazoefu na waliokomaa kiakili, hivyo hata wakikutana na mambo haya wanajua jinsi gani ya kufanya kwa sababu wanakutana nayo sana kwenye mazingira tofauti.

Haki ni haki, hata kama ushindi unakwenda kwa timu ambayo haiwezi kusafiri kwenda hata Kenya, lakini ipate haki yake na viongozi wao ndiyo waseme kuwa hawawezi kucheza michuano ya kimataifa na kusafiri, siyo wengine kuwasemea kwa kuwachezesha vibaya, kuwahujumu ili wafungwe. Timu zote ni sawa, na zichezeshwe kwa haki ili apatikane mshindi halali.

# Vinara wa kupinga ukatili wapewa tuzo

**Na Romana Mallya**

SHIRIKA la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika (WiLDAF) limetoa tuzo kwa vinara 16 wanaotumia majukwaa yao kupinga ukatili wa kijinsia nchini.

Tuzo hizo zilitolewa juzi na miongoni mwa washindi ni waandishi wa habari, viongozi wa dini na kimila pamoja na waathirika wanaoleta mabadiliko ndani ya jamii.

Akizungumza wakati wa utoaji wa tuzo hizo, Mkurugenzi wa WiLDAF, Wakili Anna Kulaya alisema zimelenga kutoa hamasa kwa kila mmoja kutokufumbia macho vitendo vya ukatili wa kijinsia na kuchukua hatua stahiki ili kuokoa maisha ya wanawake na wasichana.

Alisema wameziandaa kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo wakiwamo Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu na Afya ya Uzazi (UNFPA), Ubalozi wa Denmark na Ireland pamoja na Mfuko wa Fedha za Msaada wa Kisheria (LSF).

Alitaja vinara 16 wanaopambana na ukatili wa kijinsia na maeneo yaliyoshindaniwa kwenye mabano kuwa ni Sheikh Abballah Sheiza (kiongozi wa dini) na Gerehuida Gegasa (kiongozi wa kimila).

Wengine ni Abdul Lutungu (msanii), Averine Kitomari (mwandishi wa habari), Imani Luvanda (kinara anayetumia mitandao ya kijamii katika kutokomeza ukatili), Lightness Bayo (kinara anayetetea haki za wafanyakazi wa ndani), Kheir Simai (kinara anatokomeza ukatili dhidi ya watu wenye ulemavu) na Vicky Kimaro (kinara anayetetea haki za afya ya uzazi), Zaituni Njovu (kinara anayetumia ubunifu kutokomeza ukatili).

Aliwataja wengine ni Faustina Urassa (kinara mwathirika anayeleta mabadiliko katika jamii), James Yuster (kinara anayetetea haki za watoto), Tesha Singolyo (kinara anayeokoa watoto dhidi ya ukatili) na Salama Kikudo (kinara anayekuza haki za kiuchumi kwa wanawake vijana).

Wakili Kulaya alisema tuzo hizo wamezitoa kwa miaka mitatu kuanzia mwaka 2020.

"Sote tunashuhudia kuongezeka kwa wimbi la mauaji na vitendo vya ukatili kwa wanawake na watoto. Pamoja na mambo mengine kichocheo kikubwa ni jamii kukaa kimya na kutokuchukua hatua," alibainisha.

Mmoja wa majaji wa tuzo hizo, Aginatha Rutazaa ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji la Tusonge Community Development, alisema nia kubwa ambayo inahitajika ni kuweka nguvu ya pamoja kama wanaharakati kuishawishi serikali na watunga sera kuwa ipo haja ya kuwa na sheria moja ya kutokomeza ukatili wa kijinsia.

Alisema hiyo itasaidia kuondoa mkanganyiko uliopo sasa wa kutumia sheria mbalimbali na kusababisha haki kupotea hasa kwa wanaotendwa vitendo hivyo.

Mshindi katika kipengele cha mwaandishi wa habari kinara wa kupambana na vitendo vya ukatili wa kijinsia, Averine Kitomari alisema ushindi wake unaonyesha kazi ya waandishi wa habari katika kuelimisha na kufichua vitendo viovu ni kubwa ndani ya jamii.

0000000000000000000



Mkurugenzi wa Shirika la WiLDAF, Anna Kulaya (kushoto) na Meneja wa Shirika linalojishughulisha na kutokomeza ukeketaji na ndoa za utotoni la NAFGEM-Tanzania, Honorata Nasuwa (kulia), wakimpongeza mhanga wa ukatili na Muasisi wa Shirika la Songambele Initiative, Faustina Urassa, baada ya kupewa tuzo wakati wa hafla ya usiku wa tuzo za Vinara 16 wa mabadiliko, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# CTI yahimiza malighafi za ndani uzalishaji wa bidhaa

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKISHO la Wenye Viwanda Tanzania (CTI), limehimiza Watanzania kutengeneza bidhaa mbalimbali kwa kutumia malighafi za ndani na zenye ubora ili kuachana na uagizaji wa bidhaa nje ya nchi.

Ushauri huo ulitolewa jana na Mwenyekiti wa CTI, Paul Makanza, wakati wa ufunguzi wa mkutano mkuu wa mwaka wa shirikisho hilo.

Alisema Tanzania ina malighafi nyingi ambazo zinaweza kutumika kutengeneza bidhaa za aina mbalimbali na zenye ubora wa hali ya juu, hivyo kusaidia kuondokana na utegemezi wa kuagiza bidhaa nyingi nje ya nchi hali ambayo inaweza kudhoofisha viwanda vya ndani.

"Kwenye Mkutano Mkuu wa Wanachama wa CTI, tukiwa wadau wa viwanda tunaangalia kwenye malengo endelevu ya maendeleo (SDG) tunafanya nini. Vitu kama kuondoa njaa na umaskini tunaongelea pia namna sisi wenye viwanda tunaweza kupunguza uzalishaji wa hewa ya kaboni katika shughuli zetu za viwandani," alisema Makanza.

Alisema wamezungumzia umuhimu wa kuzingatia ulinzi wa mazingira na kuondoa kaboni na kutumia nishati safi kuhakikisha wafanyakazi wanakuwa kwenye mazingira rafiki ya kufanya kazi na kuepukana na ajira za watoto.

Makanza alisema ni muhimu kuacha kuajiri watoto kwa sababu kamapuni nyingi za nje haziwezi kufanya biashara na mtu anayewatumikisha watoto.

Aliishukuru serikali kwa kuanzisha kitengo cha kushughulikia mpango kazi wa serikali wa kuboresha mazingira ya biashara kwa lengo la kuondoa vikwazo vinavyoongeza gharama za kufanyabiashara maarufu kama Bule Print. "Tunaishukuru sana wizara imeanzisha kabisa kitengo cha utekelezaji wa Blue Print ambacho kinaainisha changamoto na kuzipatia ufumbuzi na wanatuambia wamefikia hatua gani nini kimefanyika nini bado, ilimradi changamoto zinafahamika na zinafanyiwa kazi tuna imani sana na serikali kwa sababu huwezi kuzimaliza kero zote kwa wakati mmoja," alisema.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara katika Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Christopher Mramba, alisema mpaka sasa tozo, ada na ushuru uliofutwa na serikali zimefikia 232 ambazo zilikuwa kero kwa wafanyabiashara.

Alisema wafanyabiashara wamekuwa wakiiambia serikali tozo zinazowakwaza na kisha serikali hufanya tathmini ama kupunguza au kufuta tozo husika kwani wakati mwingine inaweza kuwa inatozwa na mamlaka zingine.

"Wafanyabiashara wanatuambia kwamba tozo hii ni kubwa sana au hii ni kero na inasababisha usumbufu sana kwa hiyo serikali inafanya tathmnini kujiridhisha na wanachosema na ikibaini kuwa ni kweli inazifuta na lengo ni kuwawekea mazingira mazuri wafanye biashara na serikali ipate kodi yake," alisema Mramba. Alisema ni kweli serikali ilifanya tathmini na kubaini kuwa baadhi ya tozo, adana ushuru zilikuwa zinasababisha usumbufu mkubwa hata wa muda pia kwa wafanyabiashara kuzunguka kwenye taasisi mbalimbali hali ambayo inawapotezea muda wa kufanyakazi.

"Kuna taasisi tulibaini hazina umuhimu kwasababu unakuta kazi zake zinafanywa na taasisi zingine hivyo zikafutwa ili kuondoa usumbufu kwa wafanyabiashara, na Blue Print ndiyo kazi yake kuangalia tozo, ada au ushuru ambao unaonekana ni kikwazo kwa wafanyabiashara unafutwa," alisema.

# Shehena mafuta kupikia yanaswa njiani yakipelekwa bandari bubu

**Na Maulid Mmbaga**

JESHI la Polisi Kikosi cha Wanamaji limekamata majahazi matano yakiwa yamebeba shehena ya mafuta ya kupikia yakiwa kwenye madumu 2,352 yenye ujazo wa lita 20, yakitokea Zanzibar kwenda katika bandari bubu ya Kunduchi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kamanda wa Kikosi cha Polisi Wanamaji, Kamishna Msaidizi (ACP) Moshi Sokoro, majahazi hayo na madumu ya mafuta yalikamatwa Desemba 6, mwaka huu, Kunduchi wilayani Kinondoni katika Bahari ya Hindi.

ACP Sokoro alisema jahazi la kwanza lenye namba za usajili Z.2523 likiongozwa na nahodha Issa Baka (26) mkazi wa Bububu, Zanzibar akiwa na wenzake wanne, lilikamatwa likiwa na madumu 500.

Pia alisema jahazi la pili lenye namba za usajili Z.3145 likiongozwa na nahodha Ramadhani Hamisi (42) mkazi wa Uzi, Zanzibar akiwa na wenzake watatu, lilikamatwa wakiwa na madumu 351 huku la tatu lenye namba za usajili Z. 2946 likiongozwa na Mwalimu Hamisi (40) mkazi wa Uzi, Zanzibar na wenzake wawili, lilikamatwa likiwa na madumu 351.

"Kikosi kiliendelea na operesheni na majira ya usiku wakafanikiwa kukamata majahazi mengine mawili, ambayo ni Sv Thamarat likiongozwa na Ramadhani Eliasi (30) mkazi wa Mwanakwerekwe, Zanzibar akiwa na wenzake wanne, likiwa limebeba madumu 650.

"Lingine lenye namba za usajili Z. 3223 likiongozwa na nahodha Juma Shaibu (51) mkazi wa Mahonda Zanzibar, akiwa na wenzie watatu, lilikamatwa likiwa na madumu 500," alisema Sokoro.

Pia alibainisha kwamba upelelezi wa awali ulionyesha kuwa mzigo huo ulitakiwa kushushwa katika bandari ya Mbweni ambako taratibu za kulipa ushuru wa forodha zingekamilika na badala yake, watuhumiwa walibadili mwelekeo na kwenda katika bandari bubu ya Kunduchi ili kushusha mizigo hiyo.

Kamanda huyo alisema Jeshi la Polisi linaendelea kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na idara zingine za serikali kuhakiki mzigo huo na baadaye taratibu zingine za kisheria zitakuchukuliwa.

Sokoro aliwapongeza wananchi wote ambao wanachukia uhalifu wa aina zote na kuchukua hatua ya kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi ili kutokomeza uhalifu.

"Jeshi la Polisi linatoa onyo kwa wafanyabiashara wasio na uadilifu, kufuata taratibu za mamlaka ya mapato TRA, la sivyo watakamatwa, na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria kwa hatua zaidi," alisema Sokoro.

# DMI yawa kituo mahiri kusini mwa Sahara

**Na Joseph Mwendapole**

CHUO cha Bahari Dar es Salaam (DMI), kimefanyiwa ukaguzi wa ubora wa viwango na kuonekana kuwa kituo cha ubora (center of excellence) katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini mwa jangwa la Sahara.

Hayo yalisemwa jana na Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo hicho, Kapteni Ernest Bupamba, wakati wa mahafali ya 18 ya chuo hicho yaliyofanyika kwenye viwanja vya chuo hicho, jijini Dar es Salaam.

Mgeni rasmi kwenye mahafali alikuwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete, ambaye alimwakilisha Waziri wa Ujenzi, Makame Mbarawa. Katika mahafali hayo, wahitimu 904 walikabidhiwa vyeti vyao wakiwemo 11 waliopata shahada za uzamili.

Alisema katika kutimiza majukumu yake kwa ubora yenye viwango, chuo kimeendelea kutoa mafunzo ya ubaharia kwa viwango vya kimataifa hasa mkataba wa kimataifa wa elimu ya mafunzo ya ubaharia wa mwaka 1978 na mabadiliko yake.

Kwa kukidhi vigezo vya elimu ya juu ya ufundi, alisema chuo kina ithibati husika ambayo hutolewa na Baraza la Elimu ya Ufundi Tanzania (NACTVET).

Kapteni Bupamba alisema kwa kuzingatia vigezo vya ubora wa viwango vya kimataifa, chuo kimeendelea kupanua wigo wa kozi zake, hivyo kupata ongezeko la udahili mwaka hadi mwaka.

Alisema kwa udahili wa mwaka 1981, chuo kilikuwa na wanafunzi 12 tu katika kozi ndefu na hadi Novemba, mwaka huu, kimedahili wanafunzi 2,542 na aliishukuru serikali kwa kutatua baadhi ya changamoto zinazokikabili chuo hicho.

Bupamba alisema moja ya changamoto zilizotatuliwa ni kuanza kufanya kazi kwa Mfuko wa Elimu na Mafunzo ya Bahari (MET FUND) ambao mwaka 2020/21 ulifadhili wanafunzi 36, mwaka 2021/22 wanafunzi 173 na mwaka 2022/23 wanafunzi 229.

Alisema mfuko huo umesaidia kupata 'Live Radar' kwa gharama ya Sh. milioni 200 na wizara imesaidia DMI kupata 'Full Mission Engine Simulator' na mwaka huu wa fedha unaoendelea chuo kinatarajia kupokea 'simulator' mbili za kisasa kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi.

Naibu Waziri Mwakibete alisema wizara itazifanyia kazi changamoto mbalimbali zinazokikabili chuo.

Alisema anatambua jitihada kubwa zilizofanywa na chuo katika kukabiliana na changamoto mbali mbali ikiwemo suala la meli ya mafunzo, uhaba wa madarasa, ofisi, na vifaa vingine vya kufundishia zimekuwa changamoto sugu kwa chuo hiki.

"Kama hatua ya awali ya utatuzi wa changamoto husika, ningependa sasa kuishauri Menejimenti ya chuo iandae muhtasari ikibainisha changamoto na mapedekezo kuhusu namna gani bora Wizara isaidie katika kumaliza changamoto zote kulingana na uharaka, uzito au athari za changamoto husika.

"Napenda kuwahakikishia kwamba, mara baada ya kupokea muhtasari wa changamoto hizo Ofisi yangu itazishughulikia mapema iwezekanavyo ili nanyi muweze kuboresha huduma zenu maana ni jukumu letu sote kwa pamoja kuhakikisha kwamba shughuli za bahari zinatekelezwa katika mfumo endelevu kwa lengo la kupata maendeleo endelevu kwa taifa letu kupitia uchumi wa bluu kama ambavyo imekuwa ikisisitizwa mara kwa mara na viongozi wakuu wa Serikali," alisema Mwakibete.

Alitoa wito kwa wahitimu kutumia ujuzi walioupata kwa manufaa yao na manufaa ya taifa kwa ujumla na waweke maslahi ya taifa mbele wakitambua kuwa dhana ya uchumi wa bluu ni pana na ina fursa nyingi ikilinganishwa na sekta zingine.



Makamu Mwenyekiti wa umoja wa wazaliwa wa vijiji vya Suguti na Kusenyi, wilayani Musoma, mkoani Mara, waishio maeneo mbalimbali nchini, uitwao Suguti Diaspora, Kusaga Gombania (kulia), akizungumza katika mkutano wa mwaka wa umoja huo, jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Mwenyekiti wa umoja huo, Wakili Said Chiguma (wa pili kulia), Katibu Joseph Jandwa (wa pili kushoto) na Mweka Hazina, Belias Bunini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wazazi wapewa somo ukatili kijinsia

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WAZAZI wametakiwa kutenga muda wa kuwasikiliza watoto wao kwa faragha ili kujua unyanyasaji wanaopitia unatokea wapi na kuwasaidia mapema.

Meneja wa Shirika la Kikristo la Kuhudumia Wakimbizi Tanzania (TCRS), Rehema Samwel, alitoa rai hiyo juzi wakati wa mafunzo ya kupinga ukatili wa kijinsia yanayoendelea kwenye Tarafa ya Mikese wilayani Morogoro yenye kaulimbiu 'Kila Uhai Una Thamani- Tokomeza Mauaji na Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto'.

Samwel alisema kupinga ukimya kwa watoto mapema kutasaidia kuweka wazi ukatili wanaopitia na kuwaepusha nao kabla ya kuota mizizi itakayowasababishia madhara makubwa kwao.

Alisema wako watoto wanaopitia kwenye ukatili wa kubakwa na kulawitiwa bila wazazi wao kujua mambo ambayo baadaye husababisha athari ya kuwa na watoto wenye tabia hizo zisizopendeza kwenye jamii hata kuwa na tabia mbaya wanapokuwa na familia zao.

Samwel aliihimiza jamii kuvunja ukimya ili kutokomeza ukatili wa kijinsia kwa wanawake, vijana wa kike na wa kiume kwa sababu bila kufanya hivyo wanaweza wakakumbana na hali ngumu katika kupambana nao baada ya kuota mizizi.

Pia alisema kwa kushirikiana na serikali, wameandaa mafunzo ya kupinga ukatili wa kijinsia yatakayokamilika siku ya kilele cha maadhimisho hayo kiwilaya kesho yenye lengo la kuipa mwanga jamii juu ya madhara ya ukatili wa kijinsia na kujiweka tayari jinsi ya kuupinga.

Alisema tayari mafunzo hayo yameshawafikia watu 954 kwenye Tarafa ya Mikese wilayani Morogoro wakiwamo wanaume 286, wanawake 332, watoto na vijana 317 na wenye ulemavu 19.

Pia alisema wametoa mafunzo kwa makundi mbalimbali zikiwamo kamati za ulinzi wa mama na mtoto (MTAKUWA) kwa lengo la kuhakikisha wanakabiliana na kesi za ukatili dhidi ya mama na mtoto, wanafunzi shuleni, vikundi vya ujasiriamali vikiwamo vya vijana, wanawake na watoto.

Samwel alisema mafunzo hayo ya kupinga ukatili wa kijinsia yamefanyika kwenye tarafa ya Mikese katika kata za Mikese, Tomondo, Tawa na Kiroka.

Ofisa Ustawi wa Jamii Kata ya Tomondo, Piencia Mushi, akitoa mada kuhusu unyanyasaji wa kijinsia kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Tomondo aliwasisitiza wanafunzi hao kuzingatia na kuitumia elimu ya kupinga ukatili wa kijinsia wanayopewa kwa lengo la kupambana na ukatili wa aina mbalimbali ambao una nafasi ya kuwarudisha nyuma katika maendeleo kielimu.

Mada zingine zilizotolewa kwenye mafunzo hayo ni pamoja na utelekezaji wa watoto, ajira hatarishi, unyanyasaji wa kijinsia na ukatili wa kijinsia ukatili dhidi ya wanawake, ndoa za utotoni na madhara ya ndoa za utotoni.

# Wakubaliana kupima VVU kabla ya ndoa

**Na Shaban Njia,** SHINYANGA

WAKAZI wa Lyamidati, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, wameweka makubaliano ya pamoja kwa kila anayetaka kuoa au kuolewa kuhakikisha anapima maambukizi ya virusi vya Ukimwi (VVU) ili kuepuka kusambaza baada ya kuibuka wimbi la wanawake wanaouza miili yao.

Diwani wa Lyamidati, Veronica Nduta, alisema juzi kuwa wamefikia uamuzi huo kutokana na vijana wengi wa eneo hilo kuwa na uhusiano wa karibu na wanawake kutoka maeneo ya mjini wanaofanya biashara ya ngono kipindi cha mavuno.

Alisema wakati wa mavuno, vijiji vya kata hiyo huvamiwa na wanawake kutoka mjini wanaouza miili yao kwa wanaume wenye familia zao pamoja na vijana baada ya kufanikiwa kupata mavuno.

Nduta alisema lengo la kuweka makubaliano hayo ni kupambana na maambukizi hayo kwa vijana na wakati wa mavuno wanatoa elimu ya kujikinga na VVU ikiwamo matumizi ya kinga wakati wa tendo. Alisema wanawake hao baada ya msimu kwisha wanaondoka na mazao na kuacha maradhi.

Alisema wakati wa kuandaa mashamba, kulima na kuvuna, familia inashirikiana ipasavyo lakini wakati wa kufanya uamuzi wa kuuza mazao, anapanga baba pekee na fedha inayopatikana mwanamume anaongeza mke mwingine au kwenda kwenye starehe na watoto kukosa chakula na mahitaji mengine.

Ofisa Kilimo wa Kata, John Shilinde, alisema mazao yanayolimwa kwa wingi katika kata hiyo ni mpunga, mahindi, viazi vitamu, choroko na dengu na kwamba kila msimu kinababa baada ya mavuno wanaongeza wake na kutelekeza familia.

Mratibu wa Ukimwi Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Happiness Misaeli, alisema wastani wa maambukizi ya VVU umepungua kutokana na elimu wanayoendelea kutoa katika kata zote kwa kushirikiana na shirika lisilo la kiserikali la Rafiki-SDO.

Misaeli alisema, makundi wanayoyafikia ni yale ya vijana wenye umri wa miaka 15 hadi 24 ambayo yako hatarini na kuyapatia elimu ya matumizi ya kondomu, ujasiriamali na kuwaandaa kuwa baba na mama bora na maeneo yenye mikusanyiko kama Mwakitolyo na Tinde ambayo yanaongoza kwa maambukizi hayo.

## HABARI KITAIFA

# Mgogoro wa kisiasa wakwamisha hatimiliki

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

MGOGORO unaotokana na viongozi kutuhumiana kujinufaisha kisiasa, unadaiwa kukwamisha mchakato wa kutafuta hatimiliki ya ardhi inayotumiwa na Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) cha Nuru ya Maendeleo ambacho kinahudumia wakulima wa vijiji vitatu vya kata ya Kahe, Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro.

Akizungumza jana madhara yatokanayo na mgogoro huo, Mwenyekiti wa Nuru ya Maendeleo SACCOS, Madina Mshana, alisema maslahi ya kisiasa kutangulizwa mbele, badala ya kuhuduma wananchi kumechangia kuathiri shughuli za kiuchumi za wanachama wake, zaidi ya 1,000 waliosajiliwa.

Mshana alisema kwa muda mrefu wamefuatilia upatikanaji wa hati hiyo na kuelekezwa walipie Sh.100,000 lakini Mwenyekiti wa Kijiji hicho, amekataa kutia saini hati hiyo, jambo ambalo limewalazimu kuomba serikali kuingilia kati ili kupata ufumbuzi.

"Kwa zaidi ya miaka 15 sasa, tunamiliki eneo la ardhi ambalo tulipewa kihalali na viongozi wa serikali ya kijiji waliotangulia. Kwa miaka kadhaa, tumekuwa tukihangaika kuomba uongozi mpya uliopo madarakani kutia saini hati ya kumiliki ardhi ya kijiji, bila mafanikio.

"Eneo hilo tayari limeendelezwa, lakini kwa sababu ya maslahi binafsi ya kisiasa, uongozi wa sasa hautaki kutambua kilichofanywa huko nyuma na serikali zilizopita. Hawajui kwamba wanachofanya ili kujinufaisha binafsi, wanaumiza wananchi walio wengi. Tunaomba serikali pamoja na Mrajisi Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Kilimanjaro, waingilie kati ili jambo hili lifike mwisho na wananchi waendelee kujikwamua kiuchumi kupitia rasilimali yao," alisema.

Kutokana na mgogoro huo kuathiri chama hicho, Mkazi wa Kijiji cha Mawala, David Laizer, alielekeza kilio chao kwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, akiomba kuingilia kati mgogoro huo ili kuwezesha wananchi kupata hati, baada ya kufuata taratibu zote za kisheria. Alipoulizwa kuhusu tuhuma hizo, Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Oria Kahe, Raymond Mrisha, alisema si kweli kwamba anakwamisha suala hilo, isipokuwa watu wanajenga taharuki na kutaka kuonekana wanafanya kazi tofauti na wengine.

Diwani wa Kahe, Aloyce Momburi, akizungumzia mgogoro huo, alikiri kuwa eneo hilo ni mali halali ya chama hicho na kwamba hajajua sababu za Mwenyekiti wa Kijiji cha Oria Kahe, kushindwa kuridhia wanachama hao kupata hati miliki ya eneo hilo.

# Diwani awa mbogo wajawazito kutozwa fedha

**Na Zanura Mollel,** LONGIDO

DIWANI wa Orbomba, Longido mkoani Arusha, Ndiono Laizer, ameishutumu idara ya afya ya halmashauri hiyo, kufumbia macho malalamiko kuhusu wajawazito kutozwa gharama za matibabu, kinyume cha maelekezo ya Wizara ya Afya.

Inaelezwa kuwa wanawake wanaojifungua katika zahanati na vituo vya afya, hususani Kituo cha Afya cha Longido, wanatozwa kati ya Sh. 100,000 hadi 150,000 ili kupata huduma hiyo.

Laizer aliishutumu idara hiyo juzi kukiuka sera na maelekezo ya serikali kuhusu huduma za afya kwa wajawazito, wakati alipokuwa akiwasilisha taarifa ya kata yake katika kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani.

"Mimi mwenyewe nimefuatwa hadi nyumbani na wananchi wangu na kuelezwa juu ya jambo hili. Wananchi wanalia na mmekaa kimya, hapana! Wakati wote serikali imekuwa ikisema kwamba huduma ya wanawake wajawazito kujifungua hutolewa bure katika vituo vya afya, sasa Longido ni tofauti?"alihoji

Aidha, diwani huyo alisema kuwa pamoja na kuwapo duka la dawa la serikali katika Kituo cha Afya Longido, wagonjwa huuziwa dawa, huku wakielezwa kuwa wanafanya hivyo kutokana na gharama za ununuzi wake kuwa kubwa.

Hoja ya diwani huyo iliungwa mkono na Mwenyekiti Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira, Alais Mushao, ambaye ni diwani wa Mundarara, aliyesema ni kweli hata yeye amepokea malalamiko hayo na kuwasilisha madai hayo kwa mwenyekiti wa halmashauri hiyo.

"Pamoja na kwamba mnatoza fedha hizo, hamtoi stakabadhi. Lazima mjue kwamba kujifungua ni huduma ya dharura, sasa ni kwa nini vifaa visiwepo kwa sababu ni kitu kinachotokea muda wowote. Tuambieni kama ni huduma ya bure au ya kulipia," alisisitiza Mushao.

Akijibu malalamiko hayo, Mkuu wa Divisheni ya Huduma za Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe wa Wilaya hiyo, Dk. Seleman Mtenjela, alisema miongozo na taratibu za serikali, huduma ya wajawazito, wazazi na watoto wenye umri chini ya miaka mitano, hutolewa bure kwa wale wasiokuwa na bima.

"Nimepokea rasmi malalamiko haya na nina kwenda kufuatilia kama kuna utozaji huo wa fedha kwa wajawazito ili kupata huduma ya kujifungua. Kwa wale wenye bima, hutumika kuchangia gharama za huduma, lakini inapotokea mjamzito amefika kituoni kujifungua, na kuna baadhi ya vifaa havipatikani, atalazimika kununua," alifafanua Mtenjela.




Mkurugenzi Mtendaji wa Shirikisho la wenye Viwanda nchini (CTI), Leodegar Tenga (kushoto), akizungumza kwenye Mkutano Mkuu wa mwaka wa shirikisho hilo, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Wataja mwarobaini uvamizi wa shoroba

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

MPANGO kazi mahusisi uliotengenezwa na wadau wa sekta binafsi nchini ili kulinda ikolojia na uvamizi wa shoroba za wanyamapori na mimea katika Milima ya Usambara, unatajwa kuwa mwarobaini wa udhibiti wa shughuli za binadamu.

Kwa mujibu wa Mhifadhi Mkuu wa Kituo cha Utalii cha Magoroto, Mathias Manyanya, mkakati huo umeundwa na kuanza kutekelezwa mara moja, baada ya majadiliano kati ya Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF) na Shirika la Misaada la Marekani (USAID) linalofadhili mradi wa maliasili.

Aidha, Mhifadhi Manyanya alisema kuwa wakati wa majadiliano na watu hao, ilibainika kuwa ushoroba unaounganisha Misitu ya Nilo na Magoroto iliyopo Wilaya ya Muheza, umeanza kuharibiwa kwa kujengwa nyumba, kulima na kufuga, hivyo kusababisha viumbe hai wakiwamo ndege, kushindwa kupita wakati wa misimu yao ya kuhama kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

"Ni kweli tumeanza huo mradi, ambao wawekezaji wa sekta ya utalii, kwa kushirikiana na wakulima na wafugaji, wameweka mkakati utakaowezesha ushoroba wa mimea na wanyama kwenye Milima ya Usambara kulindwa ili usiharibiwe kutokana na wingi wa shughuli za kila siku za binadamu.

"Mkakati huu sisi watu wa Magoroto, utatusaidia sana kupaza sauti zetu kwa serikali ili mawazo yetu, ambayo tunadhani kama yatafanyiwa kazi, yatatuondolea kero tulizonazo na kutuwezesha kufanya shughuli za uhifadhi kwa ufanisi na kuwa na tija kwa taifa," alisema.

"Tuna kero nyingi ikiwemo ya wanakijiji wanaotuzunguka katika hifadhi, kukata miti ovyo, kuna ndege, ambao walikuwa wakipita katika njia zao kipindi hiki cha mwisho wa mwaka, lakini sasa hawapo tena kutokana na uharibifu wa mazingira unaofanywa na wananchi," aliongeza.


Milima ya Usambara ni sehemu ya Milima ya Tao la Mashariki ambayo inaanzia kusini mwa Kenya hadi kaskazini mwa Tanzania. Milima hiyo inainuka juu ya tambarare zinazozunguka na kama safu za pwani na hupata mvua za monsuni zinazonyesha katika Bahari ya Hindi.

Kutokana na hali hiyo, Manyanya alisisitiza kwamba tatizo hilo limewafumbua macho na kuamua kuanzisha vitalu vya kuotesha miche ya miti ya asili ili kuwapatia wananchi waipande katika makazi yao na mashamba ili kurudisha mandhari ya uhifadhi kuzunguka eneo hilo.

Akizungumzia mkakati huo, Meneja Mradi wa Tuhifadhi Maliasili ulioko chini ya USAID, Max Rugaimukamu, alisema mradi huo unalenga kuongeza ufahamu kwa wadau wa sekta binafsi, juu ya maliasili nchini.

"Kwa hapa Mkoa wa Tanga, mradi huu umelenga kuongeza ufahamu kwenye sekta binafsi, juu ya masuala ya uhifadhi wa maliasili na wanyamapori katika maeneo mawili, ambayo ni Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Amani na Msitu wa Hifadhi wa Nilo. Nia yetu ni kudumisha shughuli zetu bila kuathiri ushoroba wa wanyamapori, kati ya mapori hayo mawili,"alieleza.

Hifadhi ya Mazingira Asilia Amani, ndiyo hifadhi kongwe kuliko hifadhi asilia zote nchini. Hifadhi hiyo ina ukubwa wa hekta 8,380 na ni moja kati ya maeneo ya mfano yaliyohifadhiwa vizuri nchini kwa kutumia mfumo wa uhifadhi shirikishi, baina ya serikali na wananchi wanaoishi na kuzunguka katika hifadhi hiyo.





# NHC yatangazia kiama wadaiwa sugu

**Na Oscar Assenga,** TANGA

SHIRIKA la Nyumba la Taifa (NHC), limetangaza kiama kwa wapangaji wenye madeni 'sugu' kujiandaa kisaikolojia kuondoka kwa nguvu katika nyumba wanazoishi iwapo watashindwa kulipa malimbikizo hayo ifikapo mwishoni mwa mwezi huu.

Operesheni ya kuwaondoa wapangaji hao katika Mkoa wa Tanga, ilitangazwa jana na Meneja wa NHC Mkoa, Mussa Kamendu, wakati akizungumza na Nipashe akibainiosha kuwa mpango huo utatekelezwa kwa kuwatumia madalali.

"Hatutanii wala hatutishii ila kama watashindwa kulipa mpaka mwishoni mwa Desemba, mwaka huu, mwanzoni kabisa mwa mwaka ujao watalazimika kuondoka kwenye nyumba za NHC. Tayari tumeingia makubaliano na madalali ambao watatekeleza operesheni hiyo inayokwenda sambamba na kukusanya madeni hayo," alisema.

Kamendu alisema kwa mujibu wa sheria ya uendeshaji wa shirika hilo, mpangaji anayedaiwa kodi ya pango ataondolewa katika nyumba baada ya kupewa notisi (ilani) ya kumjulisha kusudio hilo ndani ya siku 30 kwamba shirika litavunja mkataba, iwapo deni lake hatalipwa ndani ya kipindi hicho.

Alisema baada ya kupita muda huo shirika huwa linampa kazi dalali ambaye wameinga naye mkataba kwa kumpatia orodha ya watu ambao katika siku 30 ambazo wamewapa hawajalipa madeni yao na madalali wanatoa notisi siku 14.

"Deni lao likishaenda kwa dalali, sisi kazi yetu ni kusubiri akusanye. Mpangaji yeye anabaki yeye na dalali wanaendelea na operesheni ya kudai na ikishapita siku 14 na kama hajalipa, kinachofuata anatolewa kwa nguvu kwenye nyumba kwa kukamatiwa mali zake ambazo dalali atakaa nazo kwa kipindi fulani.

"Baada ya mali zake kukamatwa, atamjulisha aliyekamatiwa vitu vyake alipe deni ili kuweza kufidia kodi anayodaiwa na kama hataweza kulipa, dalali atauza hivyo vitu ili kupata pesa ya kulipa deni la nyumba,"alisema.

Meneja huyo, alisema katika Mkoa huo, dalali aliyepewa kazi hiyo ni Kampuni ya Cops Auction Mart, ambayo itakusanya madeni yote na kuwaondoa kwenye makazi yao wapangaji walioshindwa kutii tangazo hilo.

Meneja huyo, alisema kwamba kwa Mkoa huo, malimbikizo ya madeni mpaka kufikia mwezi Novemba mwaka huu, ni zaidi ya Sh. milioni 105, huku wadaiwa wakubwa wakiwa ni watu binafsi na taasisi za serikali.




Ofisa Utumishi Mwandamizi wa Manispaa ya Temeke, Grace Mtisho, akikata utepe kuzindua makubaliano ya Kituo cha pamoja cha Biashara kati ya Danube Home na Furniture Centre, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkurugenzi Mkuu wa Furniture Centre, Prasad Kumar na (wa pili kulia) ni Meneja wa kampuni ya Danube Home, Mahfooz Gafoor. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kilio cha wananchi huduma za afya chasikika

**Na Anjela Mhando,** MWANGA

SERIKALI imesikia kilio cha wananchi wa wilaya ya Mwanga mkoani Kilimanjaro, waliokuwa wakilalamikia mara kwa mara kukosekana kwa vifaa tiba katika vituo vya afya, baada ya kuipatia Wilaya hiyo Sh.milioni 400 ya kutatua tatizo hilo.

Kukosekana kwa huduma hiyo, kulikuwa kukisababisha usumbufu mkubwa kwa wagonjwa kufuata huduma hiyo hospitali ya wilaya Usangi, Hospitali Teule ya St. Joseph ya Moshi na Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kilimanjaro ya Mawenzi.

Akizungumza jana wakati wa maadhimisho ya miaka 61 ya Uhuru wa Tanganyika, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Mwajuma Nasombe, alisema baada ya ununuzi kukamilika, vifaa hivyo vitasambazwa kwenye vituo vyote vya afya vilivyoko wilayani hapa.

"Katika kuendeleza na kuyalinda matunda ya Uhuru wa Tanganyika (sasa Tanzania Bara), Rais Samia Suluhu Hassan amefanya maboresho makubwa katika sekta ya afya kwa kuboresha miundombinu ya afya, akiipatia halmashari yetu Sh. bilioni moja kwa ajili ya ujenzi wa jengo la utawala.

"Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imetupatia Sh. milioni 400 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za afya pamoja na kurahisisha utoaji wa huduma bora za afya wilayani hapa," alisema.

Aidha, Nasombe alisema wakati wakiadhimisha miaka 61 ya Uhuru, serikali kuu imeipatia halmashari Sh. bilioni mbili kwa ajili ya ujenzi wa hospitali mpya ya wilaya.

"Katika mwaka wa fedha 2021/22, tulipokea fedha Sh. bilioni moja kwa ajili ya kuanza ujenzi wa hospitali ya wilaya lakini pia Disemba 4, mwaka huu, tumepokea Sh. bilioni moja kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa jengo la mama na mtoto na jengo la wagonjwa wa nje," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Mwanga, Abdallah Mwaipaya, akizungumza katika maadhimisho hayo, alisema wakati nchi inapata uhuru, hali ya upatikanaji wa huduma ya afya haikupewa umuhimu stahiki na watu wengi waliishi kwa kutegemea miti shamba na waganga wa asili.

# Wazembe utunzaji wa miti sasa kukiona

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

WATENDAJI wa vijiji watakaoshindwa kulinda miti inayooteshwa katika taasisi za umma, vyanzo vya maji na maeneo oevu katika Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, wamekalia kuti kavu.

Hatua hiyo ni baada ya Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Upendo Wella, kutangaza kupimwa watumishi hao kwa kazi hiyo.

Jana, Wella alisema hatasita kuagiza kuchukuliwa hatua za kiutumishi kwa watendaji hao kama katika maeneo yao itabainika miti ambayo serikali na wadau wametumia gharama kubwa kuiotesha imekufa.

Wella alitishia kufanya hivyo, alipoongoza kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya hiyo kupanda miti katika Kituo cha Afya Chekimaji na Kituo cha Afya Longoi, vilivyoko ukanda wa tambarare.

"Ni muhimu kwa viongozi wetu hasa watendaji wa vijiji na wenyeviti wa vijiji kusimamia miti hii kutunzwa hadi kukua. Tunao viongozi wa vijiji, vitongoji, watendaji wa kijiji na kata, halafu miti inakufa. Kazi yenu ni nini sasa? Na kuna zile kamati za mazingira za vijiji, hawa wote nilazima wasimamie utunzaji wa miti iliyopandwa hadi ikue.

"Tukikuta miti imeharibiwa, itabidi tumuwajibishe kiongozi wa eneo hilo hasa huyu mwajiriwa wetu ambaye ni VEO (Mtendaji wa Kijiji) na WEO (Mtendaji wa Kata). Hii nguvu tuliyoitumia leo isipotee bure ili tusije wajibishana,"alisisitiza Wella.

Akionyesha kukerwa na viongozi kushindwa kuwajibika, Wella alisema kumekuwa na tabia ya miti kupandwa sehemu mbalimbali, lakini kutokana na kukosa uangalizi wa uhakika hushindwa kukua na hivyo kusababisha kila mwaka miti kurudiwa kupandwa tena katika maeneo hayo.

Awali, Mkurungenzi Mtendaji wa Halmashari hiyo, Dionis Muyinga, akizungumza na wananchi hao aliwashauri wananchi kuendelea na kazi ya upandaji miti kwenye maeneo yao, huku akiwasihi kuacha ukataji miti ovyo ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi yanayoitesa nchi yetu na dunia kwa sasa.

Mwenyekiti wa Mazingira wa Kata Masama Rundugai, Ramadhan Msangi, akizungumzia kampeni hiyo ya upandaji miti, alisema viongozi wa serikali wanatakiwa kuwa wakali kuhusu usimamizi wa mazingira, kwa kuwa ni suala nyeti linalopigiwa kelele kimataifa.



## Chamwino waombwa kupokea wawekezaji

**Na Peter Mkwavila,** CHAMWINO

WAKAZI wa wilaya ya Chawino mkoani Dodoma, wametakiwa kuwa tayari kuwapokea wawekezaji ambao wamekuwa wakijitokeza kuwekeza kwenye sekta mbalimbali zinazowanufaisha na kusaidia kuinua uchumi wao.

Diwani wa Buigiri wilayani hapa, Kenneth Yindi, alisema hayo jana alipokuwa akimtambulisha kwa wananchi mwekezaji wa shule ya Msingi na Awali ya Maki Brilliant.

Alisema kutokana na ujio wa makao makuu ya serikali mkoani Dodoma, wananchi hao wa Buigiri wanatakiwa kufungua milango kwa wawekezaji pindi wanapohitaji kufanya uwekezaji kwenye maeneo yao.

Yindi alisema kuwa kata hiyo bado ina mahitaji mengi ya uwekezaji katika sekta za elimu, afya, kilimo, maji na miundombinu mingineyo inayohitajika kwa ajili ya maendeleo ya wananchi.

"Hapa ninachotaka kusisitiza kwa wananchi wangu wahakikishe wanafuata sheria zote za uwekezaji pindi wanapofuatwa na wawekezaji kutoka maeneo yao, ukizingatia kuwa serikali inapenda maendeleo kwa wananchi wake na si vingnevyo," alisema.

Ofisa Masoko na Mawasiliano wa Maki Brilliant, Josephine Uriyo, aliwataka wazazi na walezi kuchukua tahadhari dhidi ya shule zinazochipuka kama uyoga ambazo hazitambuliwi na serikali.

Alisema kutokana na serikali kuweka makao yake Dodoma, wazazi na walezi wenye watoto wanaohitaji kusoma wanatakiwa kuepukana na shule hizo ambazo zinaweza kuwapotezea fedha kutokana na kukosa viwango.

Kadhalika, alisema wataendelea kuunga mkono jitihada za serikali katika kuboresha sekta ya elimu ili taifa lipate viongozi watakaoitumikia nchi kwa maslahi ya wengi.

Alisema shule hiyo imefanikiwa kufikia viwango vyote vinavyotakiwa na kuwataka wawekezaji wengine kuhakikisha wanawatimizia matakwa ya wananchi ikiwamo kulipa fidia pale wanapohitaji maeneo kwa ajili ya kuwekeza badala ya kuingia kwenye migogoro isiyo ya lazima.

# Watanzania wapewa mbinu kuepuka maradhi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIBU Mkuu Wizara ya Afya, Prof. Abel Makubi, amewataka Watanzania kujenga tabia ya kufanya mazoezi na kupunguza matumizi ya pombe na sigara kupita kiasi ili kujiondoa kwenye hatari ya kupata magonjwa yasiyoambukiza ikiwemo kisukari na shinikizo la damu.

Prof. Makubi alitoa rai hiyo jana jijini hapo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya kumaliza kufanya mazoezi yaliyoandaliwa na wizara hiyo ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 61 ya Uhuru wa Tanzania Bara.

Alisema lengo la mazoezi hayo ni kuhamasisha jamii kuwa na tabia ya kufanya mazoezi mara kwa mara na kuepuka matumizi ya pombe na uvutaji wa sigara ambayo imekuwa sababu kubwa ya kuongezeka kwa magonjwa yasiyoambukiza nchini.

Pia alisema takwimu za wagonjwa wa maradhi yasiyoambukiza nchini zimekuwa zikipanda kila mwaka hali ambayo inatishia nguvu kazi ya taifa.

"Mwaka 2017 takwimu za wagonjwa walioripoti katika hospitali zetu ilikuwa takribani milioni 2.5 lakini hadi mwaka 2021 imeongezeka hadi milioni 3.5 sawa na ongezeko la asilimia tisa.

Hawa ni wale tu walioripoti katika hospitali na vituo vya afya. Lakini wapo wengine ambao labda walikwenda kwa waganga na wengine wako majumbani, hivyo hali inaonekana bado ni tishio kwa taifa," alisema.

Pia, alisema kufanya mazoezi na kuzingatia ulaji wa vyakula visivyokuwa na mafuta unaweza kusaidia kupunguza kasi ya ongezeko la wagonjwa nchini.

"Wenzetu Ulaya hata kama anatoka katika familia yenye asili ya magonjwa haya lakini wanayachelewesha kwa kufanya mazoezi na kuzingatia aina ya vyakula na wanaweza kupata katika umri wa mika 60 hadi 70. Hapa kwetu unakuta mtu wa umri ya miaka 30 anapata.

"Kutokana na hali hii wananchi wanapaswa kubadili mtindo wao wa maisha kwa kuanza kufanya mazoezi angalau kwa siku nne za wiki ili kujikinga na magonjwa haya yasiyo ya kuambukiza," alisema.

Kadhalika, alisema suala hilo si la Wizara ya Afya pekee yake bali linahusisha wananchi wote pamoja na wizara zingine za kisekta.

"Tayari tulishazungumza na wizara zingine kama wizara ya Ujenzi pale wanapojenga miundombinu ya barabara kuhakikisha kunawekwa maeneo ya wafanya mazoezi wakiwamo waendesha baiskeli," alisema.

Vilevile, aliwataka viongozi wa dini, siasa na makundi yote nchini kuhamasisha jamii kufanya mazoezi ili kulinda afya zao na kujenga tabia ya kupima afya kila mwaka ili kujitambua na kupata ushauri kwa wataalam wa afya.



Ofisa Masoko na Mawasiliano wa shule ya Awali na Msingi ya mchepuo wa kiingereza ya Maki Brilliant, kata ya Buigiri, Wilaya ya Chamwino, mkoani Dodoma, Josephine Oriyo, akizungumza na waandishi wa habari, wilayani humo jana, kuhusu umuhimu wa wazazi na walezi kuwajibika katika kufuatilia maendeleo ya watoto wao wanapokuwa majumbani. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Askofu Mkuu ageukia utunzaji mazingira

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

ASKOFU Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Dodoma, Beatus Kinyaiya, amekazia waraka wa Baba Mtakatifu Fransisco wa Laudato kuhusu utunzaji wa mazingira kwa kuwataka waumini wote na watu wenye mapenzi mema kutunza mazingira.

Alisema hayo kwenye Ibada ya Misa Takatifu ya kutoa Sakramenti ya Kipaimara kwa vijana 180 katika Parokia ya Mwenyeheri Maria Theresa Ledochowsca, Kiwanja cha ndege jijini hapa.

Askofu Mkuu Kinyaiya aliwahimiza waamini na watu wote kutambua wajibu wa msingi wa kutunza, kujali na kuhifadhi mazingira ikiwa ni sehemu ya kuheshimu kazi ya uumbaji wa Mwenyezi Mungu.

"Tutunze dunia hii ambayo ni mama yetu. Mungu aliiumba akatukabidhi sisi wanadamu tuitunze lakini kwa sababu ya uvivu wetu tunaiharibu dunia. Tunashindwa kuijali kwa sababu ya uzembe wetu. Mtu anakunywa maji chupa anaitupa popote pale anapojisikia. Dunia imekuwa si nzuri kama ilivyokuwa kwa sababu ya mwanadamu kutoijali," alisema.

Sambamba na hayo, alisisitiza suala la amani katika familia, jamii na taifa kwa ujumla kama ambavyo Yesu Kristo alitaka amani itawale kwa kila mtu duniani kote.

"Aliyofundisha Yesu katika ujio wake pamoja na mambo mengine ilikuwa kutuhamasisha sisi tuwe watu wa amani. Kwa hiyo kama jumuiyani hakuna amani kuna migogoro na vita ya maneno ni chanzo cha matatizo katika jamii," alisema.

Askofu Mkuu Kinyaiya alisema migogoro na migongano mingine katika jamii inasababishwa na ulafi wa mali pamoja na uvivu kwa baadhi ya watu kutotoka kujishughulisha ili kujipatia mali za halali, jambo linalosababisha kukosekana kwa amani ndani ya jamii.

Kinyaiya amewataka vijana waliopata sakramenti hiyo waimarishwe wa mapaji saba ya Roho Mtakatifu kutambua kuwa wanakuwa watu wazima kiimani.

Alisema licha ya umri wa vijana hao kuwa ni wadogo, kanisa linaamini wanaelewa mambo ya msingi yawapasayo kufanya kutokana na mafundisho ya msingi ambayo wamepewa kutoka katika Katekisimu na Biblia yanayowasaidia kusimama kiimani.

"Wewe mwenyewe uishi yale Mungu anayokuamuru uishi, yaani maadili na mafundisho ya kanisa. Lakini pia uwasaidie wengine kuelewa na kuishi lakini utawasaidia endapo wewe mwenyewe unaelewa," alisema.





## ACT kufanya tathmini maoni maridhiano siasa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

CHAMA Cha ACT Wazalendo kimesema kamati kuu ya chama hicho inatarajia kufanya kikao cha uchambuzi wa kupitia maoni ya wanachama kuhusu mustakbali wa maridhiano ya kisiasa Zanzibar.

Katibu Mkuu wa Chama hicho, Ado Shaibu, alisema jana kuwa kamati hiyo itafanya hivyo baada ya chama kukusanya maoni kuhusu maridhiano ya kisiasa kutokana na kuteuliwa kwa Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Thabit Idarous Faina.

Shaibu aliyasema hayo visiwani hapa wakati akizindua kampeni za uchaguzi mdogo wa jimbo la Amani kujaza nafasi ya ubunge baada ya aliyekuwa mbunge kufariki dunia.

Alisema uteuzi wa mkurugenzi huyo unatilia shaka nia ya upande wa pili uliounda maridhiano hayo ya kisiasa ambayo ndiyo tunu ya kuwaweka pamoja Wazanzibari na kuwaletea tija ya kiuchumi, kijamii na mshikamano.

"Tunawapongeza sana viongozi wa chama hiki Zanzibar kwa kuchukua hatua ya mapema ya kuzunguka mikoa yote ya Pemba na Unguja kuwashirikisha wanachama wetu ili watoe maoni yao juu ya wanavyoouona mwenendo huo maana kuna watu wanachezea shilingi chooni," alisema.

Alisema kamati kuu itaketi, itafanya uchambuzi kuhusu maoni hayo na itatoa mwelekeo na mwafaka utapatikana huku akisisitiza kuwa hawatakubali abadani mpaka mkurugenzi aondolewe katika nafasi hiyo.

Pia alisema uchaguzi huo mdogo ni jukwaa maridhawa na fursa muhimu ya kutuma ujumbe maalum kwa watawala wa Zanzibar kuwa hawaridhiki na wale wanaochezea maridhiano na hawaridhiki na maisha ya Zanzibar, hivyo kumpa kura kwa wingi mgombea kupitia ACT.

Alisema katika uchaguzi huo wanataka haki itendeke na anaeshinda ndie atangazwe.

Alisema pia kamati kuu ya chama hicho itaketi hivi karibuni na kufanya uchambuzi wa kina kuhusu ripoti ya kikosi kazi cha Rais ili kutoa uamuzi wao kuwa ni mambo gani wanayaunga mkono na yapi wana wasiwasi nayo.

Mjumbe wa kamati kuu ya chama hicho, Ismail Jussa Ladhu, alisema karibu wanarudi upya katika harakati zao za kisiasa, hivyo wenye mioyo myepesi wakae pembeni.

# Kishindo mapokezi Dk. Mwinyi Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, anatarajiwa kupokewa kwa kishindo visiwani Zanzibar akitokea Dodoma baada ya kuchaguliwa kushika wadhifa huo.

Akizungumza na waandishi wa habari katika Ofisi Kuu ya CCM Kisiwandui, Katibu wa Itikadi na Uenezi ya Kamati Maalum ya CCM Zanzibar, Catherine Peter Nao, alisema mapokezi hayo ni ya kishindo na hayajapata kutokea kwa Zanzibar kiongozi huyo atakapowasili kesho akitokea Dodoma.

Nao alisema mapokezi ya makamu mwenyekiti huyo ambaye ni Rais wa Zanzibar, yataanzia Uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume hadi Kisiwandui ambako atakabidhiwa rasmi ofisi.

"Uchaguzi wa chama umefanyika na umemalizika kwa amani na usalama na viongozi wakuu wa chama wamepatikana. Kinachofuata sasa ni mapokezi na utendaji wa kazi kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2025," alisema.

Baada ya kukabidhiwa ofisi, alisema Dk. Mwinyi atadhuru kaburi la Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Hayati Abeid Amani Karume, ambalo liko katika maeneo ya ofisi kuu ya CCM Kisiwandui. Baada ya hapo atakwenda kwenye sherehe za pongezi zitakazofanyika katika viwanja vya Maisara mjini Unguja ambako atazugumza na wana CCM, wapenzi na wananchi watakaofika viwanjani hapo.

Nao alisema atakapowasilii katika sherehe hizo, Dk. Mwinyi atapokewa kwa fashfash maalum na kutakuwa na burudani mbalimbali zitakazohanikizwa na msanii maarufu nchini, Daimond na kundi lake la Wasafi.

Katibu huyo wa itikadi na uenezi, aliwataka wanachama wa CCM na wananchi mbalimbali kujitokeza kwa wingi katika mapokezi hayo.

Mjumbe wa kamati ya maandalizi ya mapokezi hayo, Rashid Msaraka, alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kusimamia uchaguzi wa chama hicho na hatimaye kupatikana kwa viongozi mbalimbali akiwamo Makamu Mweyekiti wa CCM Zanzibar.

Msaraka ambae pia ni Mkuu wa Wilaya ya Mjini Unguja, alisema hii ni mara ya kwanza Zanzibar kuwa na Makamu Mwenyekiti wa chama aliyezaliwa baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964. Watangulizi wake wote walizaliwa kabla ya Mapinduzi hayo.



Katibu Mkuu wa Chama cha ACT Wazalendo Bara, Ado Shaibu (kulia), akimnadi Mgombea Ubunge wa Jimbo la Amani Zanzibar, Muhammed Khamis Shau, wakati wa uzinduzi wa kampeni za chama hicho, katika viwanja vya Masumbani jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Wataalamu wapiga kambi matibabu saratani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Huduma za Tiba katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, Hafidh Sheha Hassan, amewataka wananchi kufika katika hospitali hiyo kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa saratani.

Akizungumza juzi na waandishi wa habari ofisini kwake hospitalini hapo, alisema timu ya wataalamu hao kutoka taasisi inayohusiana na matibabu ya magonjwa ya kansa (HCG) nchini India, imeweka kambi katika hospitali hiyo kwa ajili ya kufanya uchunguzi na kutoa matibabu bure.

Alisema timu hiyo inashirikiana na wataalamu wazalendo wa matibabu ya saratani katika hospitali hiyo, wameweka kambi ya kuchunguza na kutoa matibabu ya maradhi ya saratani. Alisema hatua hiyo itasaidia wananchi kufanyiwa uchunguzi na kujua hali ya afya zao na wale watakaobainika kuanza matibabu.

Mkurugenzi huyo alisema saratani ni miongoni mwa maradhi mabaya ambayo husababisha watu wengi kupoteza maisha, hivyo ni vyema wananchi wakajenga utamaduni wa kupima afya zao mara kwa mara.

Alisema iwapo mtu atabainika mapema kuwa na dalili za maradhi hayo, ni rahisi kupata matibabu na kupona kuliko kusubiri mpaka ugonjwa kufika hatua mbaya.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, asilimia kubwa ya wananchi hawana uelewa juu ya maradhi hayo, hivyo kupitia kambi hizo husaidia kutoa elimu kwa jamii kujua dalili na pale wanapobaini au kuwasikia wenzao kuhimizana kwenda kufanya uchunguzi hospitali mapema kabla ya tatizo halijawa kubwa.

Aidha, aliwataka wananchi wanaposikia matangazo kama hayo, wasidharau na badala yake ni vyema kujitokeza kwa wingi ili kwenda kujua afya zao.

Daktari bingwa wa maradhi ya saratani Zanzibar, Dk. Zena Kassim Mohammed, alisema watu wengi wanasumbuliwa na ugonjwa huo huku kundi kubwa likiwa la vijana.

Alisema saratani ya matiti, waathirika wakubwa ni vijana wa kike kuanzia umri wa miaka 20 hadi 30 na saratani ya tezi dume inawaathiri zaidi wanaume kuanzia umri wa miaka 40, hivyo ni vyema jamii kujiwekea utaratibu wa kupima afya zao ili kuwa na uhakika.

Akizungumzia matibabu, alisema bado Zanzibar iko nyuma, hivyo ni vyema serikali kuweka mikakati juu ya kutoa huduma bora na zinazostahiki kwa wagonjwa hao.

"Wagonjwa wa maradhi hayo hawapati matibabu yanayostahili kwa sababu bado tunakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo vifaa tiba na mambo mingine ambayo huchangia kwa kiasi kikubwa kushindwa kufikia ufanisi wa utoaji wa huduma hizo," alisema.

Dk. Indoo Ammbulkar kutoka HCG, alisema wameamua kutoa huduma Zanzibar kwa sababu wamebaini asilimia kubwa ya maradhi hayo hukumba vijana ambao ndio nguvu kazi na tegemeo kubwa la kuchochea maendeleo ya nchi. Alitumia fursa hiyo kuiomba serikali ya Zanzibar kuwekeza zaidi katika utoaji wa huduma za afya kutokana na vijana wengi kukumbwa na maradhi ambayo husababisha kupoteza nguvu kazi ya taifa.



**HAMISA**

UKURASA 15

JUMAMOSI DESEMBA 10, 2022

Nipashe
MWANGA WA JAMII

BT
BURUDANI TELE



# ‘NASTAHILI KUCHEKWA’

UKURASA WA 18

YUKO WAPI ?

# FREDDIE KASHEBA-4

## Mchawi wa gita 'kombora', akalivunja na kuzikwa nalo



**Na Adam Fungamwango**

TUNAENDELEA na simulizi yetu kuhusu safari ya mwanamuziki nguli nchini Tanzania Freddie Ndala Kasheba aliyezaliwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo mwaka 1946 na kufariki nchini Tanzania Oktoba 22, 2004.

Kiongozi huyo, mtunzi na mpangaji wa muziki, anakumbukwa sana na mashabiki wa muziki nchini kwa staili yake aliyokuja nayo ya kupiga gitaa la nyuzi 12 ambalo lilibatizwa majina mengi kama dazani au kombora.

Aina yake ya upigaji pia ilivutia watu wengi.

### Alivyoleta upinzani na Maquis

Pamoja na kwamba Maquis ilipata upinzani wakati Kiki alipokwenda OSS na mtindo wake wa Masantula, lakini walinyanyasika sana wakati Ndala Kasheba alipochukua usukani wa kuliongoza kundi la OSS kwa mtindo wa Dukuduku.

Alililetea heshima kubwa na mashabiki wengi kutokana na umahiri wa upigaji wa gitaa lake dazani, utunzi na upangaji wa muziki.

Alitunga na kutoa vibao vilivyojipatia umaarufu kama 'Bakambi Nkela', 'Njiba', 'Ashura', 'Ntale', 'Mwaipungu', 'Mpakamanga', 'Tatu Said', 'Taifa Stars', 'Mpenzi Saleh', 'Takadiri', 'Kupenda Upofu', 'Maudhi ya Roho', 'Garba', 'Mwanakwetu', 'Aziza' na nyingine nyingi.

Ni wakati bendi hiyo ikiwa kwenye kilele cha mafanikio makubwa, ikinyang'anyana mashabiki wa Maquis.

Kuna wakati Maquis walikuja na mtindo uliojipatia umaarufu waliouita 'ogelea piga mbizi'.

Ilikuwa ni patashika nguo kuchanika. Kasheba alikaa na wenzake wakatoka na njia ya kuwazima wapinzani wao. Wakaja na mtindo wa 'Chunusi'.

Katika ufafanuzi wao kwenye gazeti la Uhuru na Mfanyakazi wakati huo, kulikuwa na maandishi ambayo walikuwa wanayaandika.

"Ole wao wachezaji na bahari, kuna chunusi. Usicheze na bahari." Hapa walikuwa wanawatahadharisha wale wanaoogelea na kupiga mbizi kwenye bahari ya Maquis. Kikachorwa kikatuni kikimuonyesha Kasheba kama bonge la jitu refu lililokuwa katikati ya bahari, lakini maji yamemfika magotini tu, akiwatafuta wale wote wanaocheza baharini.

Akajiita yeye ni chunusi. Na tangu wakati huo moja kati ya majina ambayo alikuwa nayo mpaka anafariki ni chunusi na hata kwenye nyimbo zake anapoanza kupiga solo waimbaji wanaanza kutamka 'huyo, huyo chunusi.'

Kitendo hiki kiliwainua sana na kuzoa mashabiki wengi kutoka Maquis kiasi kwamba hadi wakasalimu amri na kuachana na mtindo wa 'ogelea piga mbili' wakaja na mtindo wa 'Zembwela.'

Aina yake ya upigaji wa gitaa la nyuzi 12 ilianza kuigwa na wapigaji wa bendi mbalimbali kwa baadhi ya nyimbo.

Hata bendi kubwa nchini, Juwata Jazz Band 'Msondo Ngoma', DDC Mlimani Park na hata Mwenge Jazz zilijaribu kupiga baadhi ya nyimbo zao kwa kutumia magitaa ya nyuzi 12, badala ya sita kama ilivyo kawaida na magitaa yote ya solo.

Hata hivyo, mwenyewe alipohojiwa wakati wa uhai wake alisema ni kweli wapiga solo wa bendi nyingi walikuwa wanamuiga kupiga gitaa la solo kwa kutumia nyuzi 12 kwa baadhi ya nyimbo zao, lakini hawazimalizi nyuzi, badala yake wanapiga baadhi ya nyuzi, tofauti na yeye mwenyewe muasisi ambaye amekuwa akizichambua na kuzimaliza zote kwa kila wimbo mmoja.

> "Aina yake ya upigaji wa gitaa la nyuzi 12 ilianza kuigwa na wapigaji wa bendi mbalimbali kwa baadhi ya nyimbo.

### Avumishiwa kifo, akazoa kwa wimbo

Mwaka 1984 aliumwa na kulazwa kwenye Hospitali ya Aga Khan, ambapo tayari kulikuwa na uvumi kwamba amefariki dunia, ndipo alipotoka akatunga kibao cha 'Dunia Msongamano' akisema watu wengi hufurahia wanaposikia fulani kafa.

Mwaka 1985 alimaliza mkataba wake na bendi ya OSS 'Dukuduku' akaelekea nchini Burundi kwa mara nyingine na alirejea na kuunda bendi yake mwenyewe aliyoiita Zaita Musica mwanzoni mwaka miaka ya 1990.

Jina lake na aina ya muziki aliokuwa akiupiga, iliifanya bendi hiyo kujizolea mashabiki wengi kwa muda mfupi tu.

Alirekodi nyimbo kadhaa zilizojipatia umaarufu na kupendwa sana kama 'Umbea', Happy Birthday Ashura', 'Nimlilie Nani', 'Mama Papa', 'Mama Mtilie', pamoja na nyimbo ambazo zilichukuliwa na mwanamuziki Tshala Muana kwenda kuzirekodi tena upya 'Dezodezo' na 'Kokola'. Kama vile haitoshi kuna wimbo ambao ulikuwa ukipendwa kuliko zote na kupigwa kila siku kwenye redio, 'Kesi ya Khanga'.

Baadaye mwanzoni mwa miaka ya 2000 alipatana na Kiki, baada ya mikwaruzano wa kikazi, hasa kwa jinsi mmoja alivyoondoka OSS na mwingine kuingia, wakaungana kama walivyokuwa kwenye bendi ya Fauvette, wakaiita bendi hiyo Ya Capital 'Wazee Sugu'.

Iliendelea kuwa beandi tishio iliyokuwa ikipiga kwaeanye kunbi mbalimbali na kwenye mahoteli ya kitalii hadi walipopata nafasi ya kwenda nchini Uingereza na kubahatika kurekodi nyimbo mbalimbali ikiwemo 'Nzibola' ambao unajilikana zaidi kama 'Kitambaa Cheupe' uliotungwa na Kikii, huku solo likicharazwa na mwenyewe, Ndala Kasheba.

## UDAKU T



# HARMONIZE AJITOA

SERIKALI ina mkono mrefu, ni msemo unaotumika mara nyingi kama onyo kwa wale wanaotaka kushindana na serikali, bila kutambua inaweza kumshika sehemu na kupiga kelele.

Ndivyo, baadhi ya wasanii wa Bongo Fleva wamejikuta wakibanwa na serikali na kushindwa kupumua baada ya baadhi kuimba nyimbo zinazokiuka maadili.

Hivi karibuni, Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya nchini, Gerald Kusaya, kuonya wasanii wanaohamasisha matumizi ya bangi kupitia tungo za nyimbo zao.

Aliahidi atawachukulia hatua za kisheria dhidi ya vitendo hivyo.

“Kama kuna Msanii anadhani anaweza kupata umaarufu kwa kupitia nyimbo za kuhamasisha matumizi ya dawa za kulevya hatutomuacha, sheria itachukua mkondo na ipo siku nitawaita ili muone kitu gani tumekifanya kwa Wasanii wanaotaka kupata umaarufu kwa kutumia Dawa za Kulevya.” Alisistiza.

Hata hivyo, wapenzi wengi haraka walivamia ukurasa wa mwanamuziki Harmonize, na kuelezea hisia zao kuhusu wimbo wake mpya unaoitwa ‘Weed Language’ ambao unaelezea majina tofauti ya mmea wa bangi sehemu mbalimbali duniani.

Watu wengi wamekwenda mbali na kuelezea kauli ya kamishna Kusaya ilikuwa ikilenga wimbo huo.

Wengine walihoji hata kikohozi cha msanii huyo kiko sahihi, hasa kutokana na aina ya ukohoaji wake ambao unafanana kabisa na watu wanaotumia mmea huo ambao umewekwa katika kundi la dawa za kulevya.

Hata hivyo, Harmonize ni kama amewasikia watu waliokuwa wakiulenga wimbo wake, baada ya juzi kuomba radhi kutokana na maudhui ya wimbo wake mpya wa Weed Language ambao umeonekana kukiuka maadali na tamaduni za Kitanzania.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Harmonize pamoja na uongozi wameandika kuomba radhi Watanzania kutokana na usumbufu waliopata kutokana na wimbo huo.

Aliahidi kuuondoa haraka wimbo huo katika mitandao ya kijamii na kueleza watajitahidi kutunga nyimbo zitakazoendana na maadili na tamaduni za Kitanzania.

Swali ambalo limekuwa gumu kulijibu ni kwamba wakati wakiandika mashairi ya nyimbo hiyo hawakujua kuwa bangi ni haramu? Au alikuwa akitingisha kibiriti na sasa baada ya kuona kimejaa anagundua ni kosa?

Kilichobaki ni kusubiri jibu la Kamishna Kusaya kama atakubaliana na ule msemo kuwa ‘mtoto akinyea mkono usiukate’ na kutaka kuanza maisha mapya.

## INSTA-TWITTER

Tuffolow/ Tu-tag
**@burudanitele**





**@ wemasepetu**
Sisi apa hatuhitaji kura za ndio wala usaidizi, tunataka kupendana tu.



**@tabumtingita**
Asubutuu wee acha uwake na nilipiganie penzi langu mpaka namfundisha kublock. Mtaniulia kiposongo wangu roho yangu, sikieni naomba mdili na mimi chondee uyu niachieni mwenyewe nipambane nae mnampiga mineno mizito mpaka juzi kazimia kweli.

**@hamisamobetto**
Chukua kwa kunufaika kwa usawa, vinginevyo utaendelea kupoteza.



**@stevenyerere2**
Jivunie hicho hicho ulicho nacho



**@jenniferkyaka**
Usipojifunza kutoa sadaka,Mungu atakigawa unachokipata katika njia usiyoitarajia, ghafla utaibiwa, utapoteza, utadhulumiwa, utafanyia anasa yani mali yako itatawanyika bila malengo,jifunze kutoa sadaka.



BASI SAWA

## Nabindu Stani naye aibuka na 'Ushuhuda'




Mwimbaji staa wa muziki wa Injili ambaye anaishi nchini Canada, Nabindu Stani, amesema wimbo wake mpya unaoitwa 'Ushuhuda' umetokana na maono ya kweli ya mtoto wake.

Akizungumza na BT mwishoni mwa wiki, Nabindu amesema mtoto wake Joshua alifunguliwa ulimi na ufahamu wake baada ya kufungwa muda mrefu na kusababisha hofu ndani ya familia.

"Namshukuru Mungu kwa kunipa wimbo huu wa Ushuhuda ambao tayari upo kwenye chaneli yangu ya YouTube. Huu ni wimbo ambao umebeba maono ya kweli kwa mtoto wangu Joshua ambaye ameteseka muda mrefu lakini Mungu amemfungua na sasa amepona kabisa," amesema Nabindu.

## Poshy Queen anafurahia kuwa singo



MPAMBAJI wa video za muziki nchini,Poshy Queen amesema anaweza kumlea mtoto wake licha ya mzazi mwenzake kuwa mbali.

Amesema baba mtoto wake bado anawasiliana naye na kwamba licha ya kupata talaka miaka miwili iliyopita bado anafurahia maisha yake.

"Nafurahia maisha bila ya ndoa kwa sababu naweza kufanya kila kitu, namlea mtoto wangu bila shida na siwezi kupata mawazo juu ya hilo," amesema Poshy.



## WHOZU ATAMBA MWAKANI WEMA KAJAA

MSANII wa muziki wa Bongo Fleva, Whozu ametamba kwamba ana uhakika atampa ujauzito staa wa filamu Wema Sepetu ili apate furaha katika maisha yake.

Whozu amesema kama isingeharibika ujauzito hali ingekuwa tofauti kwa sasa kutokana na wao wawili kuwav na hitaji moja pekee, nalo ni kupata mtoto.

"Ujauzito wa kwanza uliharibika kwa bahati mbaya halafu wanafikiri ni uongo, pale lazima niweke awe mdogo wake Lora, naomba Mungu awe wa kiume na mama yake ni Wema Sepetu labda nife," amesema





## Amber Lulu anaogopa wanyakuzi

MWIMBAJI wa Bongo Fleva, Amber Lulu amesema hataki kumwonyesha mpenzi wake kwa kuhofia kunyakuliwa na warembo wengine.

Amesema yeye huwa ana wivu kiasi ambacho hataki kuona mpenzi wake anashawishika na kushiriki kimapenzi na wengine.

"Sio mara moja kunikuta suala mpenzi wangu kujihusisha na marafiki zangu, ndio maana sitaki kabisa kumweka hadharani kwa sababu kuna wengine wanasubiri mwenzao awe na mtu ili amchukue," amesema Amber Lulu.

## BENDI ZILIZOCHANUA, ZIKANYAUKA

**Na Adam Fungamwango**

MAUA huwa yanachanua na kuwa mazuri yakivutia kwa macho kutokana na rangi mbalimbali ilizonazo. Pia huwa na harufu nzuri ambayo husababisha viumbe vingi akiwemo binadamu kuvutiwa nayo.

Kwa bahati mbaya sana maua hayana maisha marefu. Hayana muda mrefu wa kuchanua. Maua halisi, ambayo si ya plastiki huwa yanachanua na kunyauka kwa muda mfupi sana. Wengine asubuhi hadi jioni, kuna ya siku moja, mbili tatu. Yapo yanayovumilia, lakini sidhani kama yanayovumilia yanaweza kuvuka wiki moja.

Miaka ya mwanzo ya 1990 zilianzishwa bendi ambazo ziliitwa au kujiita ndogo, lakini zilitoa upinzani mkubwa kwa bendi kubwa.

Zikarekodi nyimbo ambazo zilizotokea kupendwa na mashabiki wengi wa muziki, zikishindana na zile za bendi kubwa.

Leo tuziangalie bendi au vikundi vilivyoundwa miaka ya 1090 na sababu ilikuwa ni upatikanaji wa vyombo vya muziki ambavyo sasa vilianza kuingia kwa urahisi kutokana na sera mpya ya soko huria, lakini baada ya muda mfupi tu zikatoweka.

**Chezimba Band**

Ni moja kati ya bendi maarufu sana iliyoanzishwa miaka hiyo. Ilikuwa ikipiga zaidi kwenye hoteli za kitalii, ingawa ikawa inashuka kidogo mpaka kwa walala hoi, hasaa baada ya kupata umaarufu na mashabiki wengi.

Nyimbo zao zilizotia fora na kukongo nyoyo za mashabiki wa muziki wa dansi ni 'Kijogolo sina Nyumba' na 'Macho Nyanya Mshumaa'.

**The Tatunane band**

Ilikuwa ni bendi iliyopiga muziki tofauti kidogo na bendi zingine. Yenyewe ilipiga muziki wa asili kutoka kwenye makabila mbalimbali ya Tanzania, wakitumia vyombo vya kisasa vya dansi pamoja na vya asili.

Ilirekodi nyimbo nyingi nzuri, ikiwa na kina Omari Naliene, Madi Tumbo, Charles Muhuto, Abdallah Omari. Mara nyingi bendi hii haikuwa inakaa sana nchini. Ilikuwa na tripu za kwenda nje ya nchi hasa bara Ulaya kama kwenda Kariakoo.

**Orchestra Cobash**

Lilikuwa ni kundi kama la 'zing zong' yaani wanamuziki wanaotoka kwenye bendi zao, wanakusanyika, wanarekodi nyimbo, wanaziuza na kila mmoja anarejea kwenye bendi yake.

Cobash ilikuwa ni kifupi cha wanamuziki Comson Mkomwa, Bashekanako Roy, Shabaan Yohana 'Wanted'. Walifanya fujo kwa kurekodi nyimbo zilizotesa sana kipindi hicho kama 'Bojo Kasilo' ulioimbwa katika lugha ya Kihaya na 'Maneno ni Sumu' ambao Wanted alikung'uta solo la 'kinyama'.

**Djakabe Stars**

Bendi hii iliundwa na aliyekuwa mwanamuziki Belesa Kakere baada ya Shirikia la Bima kumrudisha ofisini badala ya kuwa jukwaani. Alifanya kazi za kiofisi, lakini akiunda kundi hilo la Djakabe ambapo alimchukua pia mwimbaji wa muziki wa Bima Taarab, mwanadada Mariam Nylon akamfundisha na kuimba kwa ustadi muziki wa dansi. Moja ya wimbo ambao Kakere na Nylon 'Yanichoma sana kama Mshale.'

**Makondeko Group Band**



Baada ya wimbo wa 'Kila Munu Ave na Kwao' akiwa na CTU Les Mwenge, uongozi wa mwanasiasa Dk Alex Khalid uliunda bendi ya Makondeko Group, akamchukua Harila Tongolanga kuwa kiongozi wa bendi.

Na kweli waliyoyafanya yamebaki kuwa simulizi hadi leo. Walitoka na vibao kama 'Kila Munu Ave na Kwao' sehemu ya pili 'Saidaru', 'Sanura', na nyingine nyingi.

FILAMU

## Ndugu wa Mume: Kachimba kisima kaingia yeye

**Na Adam Fungamwango**

ROHO mbaya haijengi popote pale na usilazimishe jambo ambalo unalitaka wewe bila kuangalia faida ya wengine.

Mara nyingi watu hufanya ubaya, lakini matokeo yake kwa nguvu za Mwenyezi Mungu, wengi wao huwa unawarudia wenyewe.

Kwenye maisha ndani ya jamii huwa tunayaona sana. Na hapa tuaangalie kwenye filamu hii iitwayo 'Ndugu wa Mume.'

Imechezwa na wasanii kadhaa ambao ni Time Saidy, Imani Kidile, Mashaka Omari, Latifa Mtumwa, Princess Heena, Ali Hoza, Baraka Tweve, Neema Maganga, Cesilia Deo, Victoria Sylvester, Ally Kunambi, Khamisi Hammy na wengineo.

Picha linaanza kwa kumuonyesha kijana Hoza ambaye ana kazi yake nzuri, na uwezo mkubwa kimaisha akizozana na dada yake Jesca juu ya kumrudia mpenzi wake wa zamani Eva.

Kuna mtu anawaambia mtu huyo hataki hata kumuona. Upande wa pili wa shilingi kuna makahaba mawili. Wamempokea mgeni kutoka mkoani. Amekuja mjini kutafuta. Wanataka wamuingize kwenye kazi hizo. Neema anakataa kwa madai amelelewa kwenye mazingira ya watu wenye hofu ya Mungu. Wenzake wanamtimua. Anatafuta kazi huku na huko. Anaangukia kwa Hoza.

Alipata kazi katika mazingira ya tabu sana. Na hata mwanzo wa kazi yake ndani humo ulikuwa wa tabu. Ni kwa sababu Hoza alimkubalia lakini kulikuwa na hausigeli mwingine. Alimkubalia kwa ajili ya kusaidia. Kitendo kile Jesca hakupendezewa nacho. Aliona baadaye inaweza kuwa hatari kwa shoga yake Eva ambaye alikuwa mpenzi wa kaka yake. Na ndivyo ilivyokuwa. Kila kunapokucha Hoza alionekana kumuelewa Neema na kumpenda. Mwisho wakawa wapenzi kweli. Palinoga hapo. Lilikuwa penzi la kweli. Jesca na shoga yake Eva waliumia. Waliwekana vigenge kuwa wamkomeshe. Dhamira yake ilikuwa ni kumuwekea sumu Neema afe.

Ni wakati ambao ndugu wa Neema alikuwa amekuja kumtembelea ndugu yake. Aliona kitendo cha Jesca kumuwekea sumu dada yake. Alichofanya alibadilisha sahani. Wakati Jesca akidhani Neema anakula chakula chenye sumu, kumbe yeye ndiyo alikuwa akikila.

Tumbo lilianza kumuuma na haraka daktari wa familia akaja. Alipopimwa alionekana amekula chakula chenye sumu. Bahati nzuri alipona. Nani aliweka? Swali lilikuwa gumu. Ndugu wa Neema ndiye aliyesimulia mchezo mzima jinsi alivyouona ukichezwa. Jesca alishidwa kukataa. Dhamira ilikuwa ni kumuua wifi yake Neema. Kisa Eva aje kukaa pale. Hoza ikabidi amueleze kitu alichomficha dada yake siku nyingi kuwa haiwezekani kwa sababu Eva alimfumania na rafiki yake ndiyo maana alimuacha.

BONGO FLEVA

# 'NASTAHILI KUCHEKWA'



KILA siku ndivyo hali inavyozidi kuwa mbaya kwa penzi la mastaa Harmonize na Kajala, kiasi ambacho inaonekana ni dhahiri limekufa kwa mara ya pili.

Wawili hao walikuwa katika mapenzi motomoto baada ya kurudiana mapema mwaka huu.

Mapenzi ya Harmonize na kajala yaligonga vichwa vya habari kutokana na matukio mengi waliyoyafanya kama ishara ya kustawi kwa mahaba yao.

Hata hivyo, siku chache zilizopita hali hiyo ilibadilika na kusababisha kajala, kuingia kwenye uwanja wa mitandao ya kijamii na kukiri anastahili kuchekwa.

Wakati akikiri jambo hilo, mwigizaji huyo mkonwe ameondoa utambulisho wake katika ukurasa wa Instagram inayumuonyesha kuwa meneja wa Harmonize, hivyo kuashiria hana mpango naye tena.

Haijafahamika ni sababu gani wawili hao wapo katika mgogoro na kisha kuamua kila mmoja kuwa mbali na mwenzake.

Katika ujumbe wake Kajala, ameonekana kujilaumu na kujifananisha na mkosaji ambaye anastahili kubezwa na kudharauliwa.

"Mimi kama mwanamke na binadamu nimeumbwa kupenda na kusamehe pia,ila kwenye hili nastahili kuchekwa, nastahili kubezwa na kudharauliwa pia," ameandika Kajala.

Akaongeza "Sipo hapa kujitetea wala kutia huruma ni kweli nilifanya makosa na nimeyagundua makosa yangu, mimi siyo mkamilifu. Hakika nimekosea familia yangu, ndugu zangu, na marafiki zangu. Kutenda kosa si kosa, kosa kurudia kosa, nimekusamehe mpenzi wangu wa zamani sasa nipo tayari kwenda mbele,"



## BATA LA WIKI

Je una kiwanja cha burudani piga -0717336368

**Waluguru Original**
Kama kawaida yao, leo Jumamosi watafanya vitu vyao katika ukumbi wa Terminal Pub uliopo Msamvu, kesho Jumapili watamalizia wikiendi yao ukumbi wa F2 Florida mjini Morogoro.

**Mjengoni Classic Band**
Bendi hii ya jijini Arusha, leo Jumamosi itafanya makamuzi yake katika ukumbi wa Kokoriko Annex, kesho Jumapili itamalizia wikiendi katika ukumbi wake wa nyumbani wa Mjengoni Club Orasiti jijini humo.

**Twanga Pepeta**
Leo Jumamosi bendi hii kongwe itatoa burudani ndani ya ukumbi wa G-7 uliopo Kinyerezi, kesho Jumapili kama kawaida itamalizia wikiendi katika ukumbi wa Gwambina Lounge, zamani TCC Club Chang'ombe.

**Town Classic Band**
Jumamosi ya leo kikosi kizima cha wana Town Classic kitashuka ndani ya ukumbi wa Buga Lounge Kimara Korogwe, kesho Jumapili bendi hiyo itatoa burudani katika ukumbi wa Twist Baa Tabaka Bima.

**Orchestra Sikinde Original**
Bendi hii mpya leo Jumamosi inafanya vitu vyake katika ukumbi wa Shabaha Mbezi Beach, kesho Jumapili kama kawaida itakuwa katika ukumbi wa Nefaland Manzese Argentina.

**FM Academia 'Wana Ngwasuma'**
Wakiwa chini ya rais wao, leo Jumamosi kama kawaida yao watatoa burudani katika ukumbi wa Mawasiliano Park Ubungo, uliopo kando ya Barabara ya Sam Nujoma, jijini Dar es Salaam.

**Tukuyu Sound Band**
Vijana hawa machachari, kesho watamalizia wikiendi yao ndani ya ukumbi wao wa nyumbani Mawasiliano Park, uliopo Ubungo kando ya Barabara ya Sam Nujoma.

**Orchestra Sikinde Original**
Bendi hii mpya leo Jumamosi inafanya vitu vyake katika ukumbi wa Shabaha Mbezi Beach, kesho Jumapili kama kawaida itakuwa katika ukumbi wa Nefaland Manzese Argentina.

**Kimokimo Band**
Wakiwa chini ya mwimbaji wa siku nyingi aliyepitia bendi mbalimbali, Khadija Kimobitel, kila Ijumaa huwa ndani ya ukumbi wa Mariot uliopo eneo Extertanal jijini Dar es Salaam.

**Maina Band**
Bendi hii inayoongozwa na mwimbaji mkongwe, Liston Maina, leo Jumamosi itafanya makamuzi ya nguvu katika ukumbi wa Regancy Park, Mikocheni.







# WAREMBO HAWA NOMA

LICHA ya burudani na warembo kuwa ni mambo pekee yanayoweza kumfanya mwanaume kutuliza akili, lakini ikizidi inaweza kuleta athari.

Sasa wanasoka wa Ujerumani wanalalamikiwa kufanya vibaya kutokana na kula bata kwa sana, huku wakionekana wakitanua na warembo.

Viongozi wa soka Ujerumani wametupia lawama vitendo vilivyo fanywa na baadhi ya wake na wapenzi wa wachezaji wa soka wa timu hiyo kwenye hoteli ya kifahari ya Zulal Wellness Resort nchini Qatar.

Wanasema sababu hizo za wachezaji kupenda kula bata na warembo ndiyo sababu ya kutolewa mapema kwenye michuano ya Kombe la Dunia 2022.

Inadaiwa warembo hao walikula bata vya kutosha na wachezaji huku baadhi yao wakipiga picha wakiwa kwenye mabwawa ya kuogelea ya kifahari ndani ya Zulal Wellness Resort iliyopo Kaskazini mwa nchi ya Qatar.

Kwa mujibu wa ripoti ya Bild, rais wa DFB, Bernd Neuendorf na makamu wake Hans-Joachim Watzke ni miongoni mwa walio hudhuria kikao hicho.

Wamebaini kuwa tabia za marafiki na familia za wachezaji kuwa ndiyo sababu iliyopelekea kuondoa utulivu kambini.

Warembo hao waliruhusiwa kuwa na wachezaji usiku kwa siku mbili kisha kutengana kwenye hoteli hiyo ya hadhi ya nyota tano.

Zulal Wellness Resort iko umbali wa kilomita 111 kutoka Doha yenye ukubwa wa hekta 28 vyumba 120.



# Amber Heard akata rufani

MWIGIZAJI nyota wa Marekani Amber Heard, amekata rufani katika kesi ya kashfa aliyomfungulia mume wake wa zamani, Johnny Depp.

Kulingana na gazeti la New York Post, mwigizaji huyo mwenye umri wa miaka 36 aliwasilisha rufaa hiyo mapema mwezi huu, akidai kwamba hukumu iliyotolewa haikuwa ya haki kwa sababu rekodi za matibabu ambazo alielezwa kuwa alidhulumiwa hazikujumuishwa.

Jaji Penney Azcarate wa jimbo la Fairfax katika mji wa Virginia, hapo awali alitupilia mbali ushahidi huo na kusema kuwa ni tetesi.



## Perry ahimiza upendo kwa wazazi wa kiume

MSANII wa vichekesho kutoka Nigeria, Samuel Animashaun Perry, maarufu kama Broda Shaggi, ametoa wito kwa wazazi wa kiume wa Kiafrika kufuata mila ya kukumbatia watoto wao.

Kulingana na mcheshi huyo, kuonyesha mara kwa mara upendo kutoka kwa baba huwa na jukumu kubwa katika maisha ya watoto wao.

"Akina baba wa Kiafrika tafadhali wakumbatieni watoto wenu! Wapendeni, ni muhimu sana," ameandika Broda.

## D'Banji hata wewe unahusika?

MWANAMUZIKI wa Nigeria, Oladapo Oyebanji, maarufu kama D'banj, amekamatwa na kuzuiliwa na kikosi cha kuzuia na kupambana na rushwa nchini humo.

Kulingana na mtandao wa Premium Times, mwimbaji msanii huyo alikamatwa Jumanne, Desemba 6, baada ya wahudumu wa ICPC kumsogelea na kumlazimisha kujisalimisha.

D'banj alikamatwa kwa tuhuma za kuweka fedha kwa njia ya ulaghai zilizokusudiwa kwa mradi wa N-Power kwenye akaunti zake binafsi.

Mradi wa N-Power ni mpango wa uwezeshaji ulioanzishwa na serikali ya Nigeria mwaka 2016 ili kushughulikia masuala kama vile ukosefu wa ajira kwa vijana na kuongeza maendeleo ya kijamii.





## Kanye West kibano tena

KAMPUNI ya Twitter imeisimamisha tena akaunti ya rapa Kanye West, miezi miwili tu baada ya kurejeshwa kutoka ana na kukiuka sheria za mitandao ya kijamii.

Mmiliki wa Twitter, Elon Musk, alifurahia kurejea kwa rapa huyo, ambaye sasa anajulikana kama Ye, kwenye jukwaa mwezi Oktoba.

Katika tweet yake iliyochapishwa Desemba 1, Musk alisema "Nilijaribu niwezavyo, pamoja na hayo, alikiuka tena kanuni yetu ya kupinga uchochezi. Akaunti yake itasitishwa.' Ameandika Musk.

West amefungiwa baada ya kuandika kupitia mtandao kuwa ni mfuasi sugu wa Hitler na chama chake cha Nazi.

## Portable hujui kuna vita vya Ukraine

MWIMBAJI mwenye utata kutoka Nigeria, Portable ameathiriwa na tatizo la ukosefu wa nishati ya mafuta kwa ajili ya gari lake.

Kwa sasa Nigeria inakabiliwa na uhaba wa mafuta unaozidi kuwa mbaya kila kukicha.

Katika video ya mwimbaji huyo anaonekana kwenye gari lake akitokwa na jasho jingi akiwa kwenye foleni ya kununua mafuta.



MAKALA

# Mwanafasafa anayebeba historia ndefu inayoshikamana na safari kuu ya uhuru

**Na Prof. Nikolai Kosukshin**

JULIUS Kambarage Nyerere, ni kiongozi wa tabaka la kina Mahatma Gandhi (India), Sun Yatsen (China), Gamal Abdel Nasser (Misri), Kwame Nkrumah (Ghana) na Leopold Sedar Senghor (Senegal), waliopata nafasi katika historia duniani.

Amekuwa na haiba, akiainisha maoni na matarajio ya watu. Mbali na kuongoza serikali, ana mchango nje ya hapo kuendeleza dhana asili ya ujamaa na mahiri katika kuainisha maendeleo.

Sasa, historia kubwa, hasa baada ukoloni wa Afrika, inahusishwa sana na jina lake. 'Enzi ya Nyerere' ni kipindi cha harakati za watu wa Afrika kupigania uhuru, ujenzi wa utaifa, kutafuta njia za maendeleo na kuanzisha misingi ya kidemokrasia, ikiwamo Tanzania.

Alizaliwa mwaka 1922, kijijini Butiama mkoani Mara. Baada ya elimu ya sekondari, alijiunga na Chuo Kikuu cha Makerere, nchini Uganda na masomo zaidi ya historia na sosholojia, kati ya miaka 1949 hadi 1952, katika Chuo Kikuu cha Edinburgh, Uingereza.

Nyerere alipenda siasa na alifahamiana na viongozi wapigania uhuru Afrika Magharibi, ikiundwa chini ya ushawishi wa Ujamaa wa Magharibi maarufu 'Fabian Socialism'.

Aliporudi nyumbani, akajiunga na chama cha Waafrika, Tanganyika Tanganyika African Association (TAA) kwa muda, kisha akaajiriwa kufundisha shule za Tabora na kisha Pugu, Dar es Salaam.



Ni mwaka 1969 Mwalimu Julius Nyerere, alipozuru nchini, akisalimiana na Mkurugenzi wa Taasisi ya Masomo Juu ya Afrika, V. G. Solodovnikov, katika hafla na mabalozi walioko Moscow, iliyoandaliwa kwa heshima yake. **PICHA ZOTE: KITUO CHA UTAMADUNI RUSSIA.**

**AANZA UONGOZI**

Mwaka 1954, chama Tanganyika African National Union (TANU) kilipoanza rasmi kupigania uhuru na nyendo zake zilipoiva, akawa Waziri mkuu hadi uhuru ulipopatikana tarehe kama ya leo, mwaka 1961, kisha baada ya mwaka, mfumo ulipobadilishwa, akawa Rais.

Muda mfupi baadaye, Nyerere akaanza kutambulika kwa jina la heshima 'Mwalimu' na mwaka 1964, Tanganyika na Zanzibar zikaungana, hata akawa Rais wa Tanzania alikotumikia hadi 1985, alipostaafu kwa hiari, akikabidhi kijiti kwa Mzee Ali Hassan Mwinyi.

Tangu mwanzo, TANU ilitoa wito kwa wananchi kufanya kazi kwa bidii kuinua kiwango cha maisha yao, pia kuondoa umaskini na maendeleo-duni yaliyorithiwa toka ukoloni.

Ikiongozwa na Nyerere, TANU ilibuni na kupitisha mipango ya maendeleo ya nchi tangu zama za kupigania uhuru, Nyerere akipendekeza wazo Ujamaa wa Kiafrika, baadaye ikawa nyenzo ya kutafuta maendeleo kwa nchi huru.

Nadharia za Nyerere zilidhihirisha mahitaji ya haraka kwa wakulima, wafanyakazi wa mijini, tabaka dogo la wasomi.

Mnamo Mei 1960, alichapisha andiko lake 'Mwelekeo wa Uzalendo wa Kiafrika'.

Ilikuwa inaeleza umuhimu wa mapinduzi ya kijamii na kuundwa jamii yenye msingi wa ustawi wa wote, badala ya wachache kujilimbikizia mali, ikiwa ni hitaji la fikra ya kijamaa katika mawazo na matendo, jambo alilolisisitiza kwenye mkutano kuhusu 'Ujamaa wa ki-Pan-Afrika' (Pan-African Socialism), uliofanyika Aprili 1962, jijini Dar es Salaam.

Katika hotuba yenye jina 'Ujamaa: Msingi wa Ujamaa wa Kiafrika' ni kati ya nadharia zenye ushawishi mkubwa zilizoundwa na wana-itikadi wa harakati wa ukombozi wakati huo.



Mwalimu Julius Nyerere, alipewa shada la maua kwenye kaburi la V. I. Lenini, kiongozi, muasisi wa Muungano wa Kisovieti (USSR.

**MISINGI UJAMAA**

Viunganishi muhimu vya Ujamaa, vilibainishwa katika kutekeleza nadharia, Ujamaa wa Kiafrika, ikinadiwa kushikilia maendeleo ya kijamii duniani.

Nadharia ya Nyerere, inashikiliwa na kazi za Azimio la Arusha na Sera ya Ujamaa na Kujitegemea ya TANU, hata akatokea kuithamini sana; Biblia kwa ajili au imani na Azimio la Arusha, zikawa miongozo yake muhimu ya kazi. Akasisitiza jamii zijitegemee kiuchumi na kijamii, kuwezesha mazingira endelevu kuokoa.

Kanuni za uongozi zilitungwa na kujumuishwa katika Azimio la Arusha, zikitamka miiko ya kiongozi wa TANU au serikali kumiliki hisa katika kampuni; kuwa mkurugenzi katika asasi binafsi kupokea, mishahara miwili au zaidi; kumiliki nyumba za kupangisha.

Baadaye wigo ulipanuliwa kujumuisha maofisa wote wa juu na kati, serikalinmi na kwenye chama. Uhuru ulipopatikana tu, Nyerere akasisitiza kujengwa maadili ya taifa yanayozingatia mila za nchi, kukifafanuliwa maana ya ujamaa, pia dira yake.

Katika nadharia ya Ujamaa, mtu aliwekwa kuwa kigezo kikuu cha maendeleo, mipango ya maendeleo ikiwekwa ipimwe kwa mahitaji yake halisi.

Utekelezaji wake, kukaundwa vijiji vya ujamaa vinavyowaangalia wakulima wenye malengo mahsusi, wakihamishiwa kwenye maeneo yenye rutuba waishi na kufanya kazi pamoja, yote yakifanywa kwa wakati muafaka, kuongeza tija ya kilimo na kuinua kiwango cha maisha.

Vijiji vililengwa viwe shule za siasa na utamaduni kwa nchi na jamii, ushiriki wake ukitarajiwa kuwa wa hiari. Hata hivyo, kuna walakini ulishuhdiwa katika utekelezaji huo.

Mwaka 1973, Kamati ya Utendaji ya Taifa ya TANU, ilipitisha uamuzi kuwahamishia wakulima kwenye makazi mapya ya vijiji vya ujamaa hadi ifikapo mwisho wa mwaka 1976, ikiitwa 'Opereshení Vijiji vya Ujamaa.'

Mwaka 1981, idadi ya vijiji vilivyosajiliwa vilifika 8,180, vikiwa na wakazu milioni 14 au asilimia 90 ya wakazi wote wa vijijini. Lengo kuu la kuundwa makazi hayo, lilikuwa kuhakikisha utoshelevu wa chakula.

Nyerere mwenyewe alikadiria matokeo chanya. Katika chapisho lake 'Azimio la Arusha, Miaka Kumi Baadaye' akifafanua nchi kukabiliwa na matatizo mengi yanayopaswa kurekebishwa, ikiwa na mwongozo 'lakini, tunasonga mbele katika mwelekeo sahihi.'

"Ndani ya miaka kadhaa, Tanzania itakumbana na matatizo ya kiu-

INAENDELEA UK. 22

MAKALA



Rais Julius Nyerere akiwa na marais wanaharakati wenzake wa ukombozi Afrika. Kutoka kushoto ni, Kenneth Kaunda wa Zambia na kulia kwake, Jommo Kenyatta (Kenya) na Milton Obote (Uganda). **PICHA: MTANDAO.**

# Mwanafasafa anayebeba historia ndefu inayoshikamana na safari kuu ya uhuru

INATOKA UK. 21

chumi 'jitihada zetu, zinapaswa kuwa sawia na shida zetu. Hatuwezi kutarajia matokeo mazuri ya kazi yetu yapatikane kwa haraka haraka," ananukuliwa Nyerere katika maandiko yake.

"Tunapaswa kuwa tayari kupata ujira kwa juhudi zetu katika kupanua kujitosheleza kitaifa na kulinda uhuru wetu kwa vitendo. Kuna wakati wa kupanda na wakati wa kuvuna. Ninaogopa kwamba kwetu, wakati wa kupanda bado haujaisha," ananena.

**MAISHA YA KUSTAAFU**

Nyerere baada ya miaka 24 ya urais, alijiuzulu, akibaki anashikilia wadhifa Mwenyekiti wa chama tawala, CCM na miaka mitano baadaye akaiacha nafasi hiyo.

Ndipo akaamua kurejea nyumbani kijijini Butiama, kutekeleza taaluma aliyoipenda zaidi, ukulima, vilevile akishiriki shughuli mbalimbali za kisiasa, kitaifa na kimataifa.

Kimsingi, Tanzania imepata kiongozi bora, baada ya miaka 75 ya kutawaliwa na wakoloni, kwanza Wajerumani na kisha na Uingereza, hazina za taifa zilifilisiwa sana.

Moja ya madhila ya ukoloni, ni vifo vingi vya magonjwa yanayotibika vilotokea, hata kiwango cha vifo vya watoto wachanga kilifikia 250 kwa uzazi wa watoto 1000.

Pia, ni asilimia 26 tu ya ardhi inayofaa kwa kilimo ndiyo iliyokuwa inalimwa, iliachwa. Maeneo makubwa hayakufaa kwa makazi kwa sababu ya wingi wa wadudu warukao aina ndorobo katika maeneo hayo.

**MAFANIKIO YAANZA**

Kwa sasa Tanzania imo katika nchi zenye kiwango bora cha elimu katika mataifa yanayoendelea. Elimu ya msingi ni ya lazima na inatolewa bure, idadi ya wanafunzi elimu ya sekondari na vyuo vikuu imeongezeka maradufu.

Tanzania inasifiwa kuwa na programu zilizofanikiwa za elimu ya watu wazima, vifo vimepungua na kuna magonjwa yanayotokomezwa kabisa.

Takriban, watu wote wanapata huduma ya matibabu bure, majisafi na salama yanasambazwa umri wa kuishi umeongezeka kutoka wastani miaka 40 hadi 52, huku vifo vya watoto vimepungua.

**MJENZI WA TAIFA**

Nyerere alimwachia mrithi wake, Mzee Mwinyi, nchi ikiwa ni yenye utulivu usio wa kawaida, janga la ukabila linalotatiza nchi nyingi hasa Kiafrika, Tanzania ikiwa na nafasi ndogo sana katika hilo.

Kazi kubwa mkubwa iliyoachwa ni katika kuendeleza lugha ya taifa Kiswahili, hata kuna wakati alitafsiri kwa Kiswahili michezo ya kuigiza iliyotungwa na msanii William Shakespeare.

Pia, kuna mafanikio ya heshima ya Tanzania kimataifa, kwa jamii bora kupigania uhuru wa kiuchumi na umoja kitaifa, huku mchango wa Julius Nyerere, haukosekani; asiyechoka kupigania uhusiano wa kiuchumi kati ya mataifa tajiri ya Kaskazini na nchi za Kusini zinazoendelea.

Uhuru na Umoja, ilikuwa kaulimbiu ya TANU, iliyoasisiwa hadi kupata uhuru na Muungano wa Aprili 1964, kukashuhuhiwa muuugano wa Tanganyika na Zanzibar.

**AKUZA DIPLOMASIA**

Uhuru wa Tanzaniam, ulifungua milango ya uhusiano kidiplomasia, barani Afrika, uswahiba na makomredi wa mbali, ikiwamo ilichokuwa Muungano wa Jamhuri za Kisovieti (USSR) mwaka 1969, Nyerere, alitembelea nchi hiyo.

Kauli ya pamoja baada ya mazungumzo kati ya Tanzania na USSR, ilieleza kushabihiana maoni ya matatizo kimataifa, ikiwamo mapambano dhidi ya ukoloni na ubeberu.

Mnamo Machi, 1977, ilifanyika ziara ya ujumbe wa USSR nchini Tanzania, hata kukatiwa saini makubaliano ya kibiashara, kitamaduni na kisayansi. Mnamo mwaka 1987, Julius Nyerere alipewa Tuzo ya Kimataifa ya Amani ya Lenin.

**KITOVU CHA UKOMBOZI**

Dar es Salaam, makao makuu ya makundi ya wanaharakati wapigania ukombozi wa kama FRELIMO (Msumbiji), MPLA (Angola), ANC (Afrika Kusini) na vikosi vya kitaifa vya ukombozi Kusini mwa Rhodesia (sasa Zimbabwe), walipata mafunzo katika kambi zilizoko Tanzania.

Kuanzia mwaka 1977 hadi 1985, Nyerere alikuwa Mwenyekiti wa Kundi la Nchi za Mstari wa Mbele. Kuanzia mwaka 1988 hadi 1990, alikuwa Mwenyekiti wa Tume ya Ushirikiano wa Nchi zilizo katika Ukanda wa Kusini wa Dunia (Kusini-Kusini).

Tangu Machi 1996, alikuwa Mpatanishi Mkuu wa Kimataifa katika msugano wa kikabila nchini Burundi na hadi siku mwisho wa maisha yake, Nyerere alidumu kupigania amani yaa Afrika nakutatuzi matatizo yote kwa mazungumzo.

Mwishoni mwa mwaka 1997, katika kuadhimisha miaka 75 ya kuzaliwa kwake, Nyerere, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), kilifanya mkutano wa nadharia wa kimataifa juu ya mada: 'Tafakuri juu ya Uongozi katika Afrika: Miaka Arobaini baada ya Uhuru'. Mengi yalimuenzi Nyerere kwa mchango wake katika ukombozi wa bara la Afrika na uimarishaji wa Tanzania kama taifa.

**KIFO CHAKE**

Miaka miwili baadaye, Oktoba 14, 1999, alfajiri, katika Hospitali ya Mtakatifu Thomas, jijini London, katika mwaka wa 77 wa maisha yake, Julius Nyerere, alifariki.

Katika taarifa ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), juu ya tukio la kifo cha Rais wa kwanza wa Tanzania, aliiambia dunia kwamba, Julius Nyerere alikuwa 'jabali la karne ya 20'.

**●Mwandishi ni mwanazuoni wa Historia na Profesa Mtafiti-Mwandamizi katika Taasisi ya Elimu juu ya Afrika ya Akademia ya Sayansi ya Russia. (Russian Academy of Sciences).**

MAKALA

# Simulizi za mashuhuda uhuru zilizobeba historia walivyoshiriki vita vya Nyerere

**Na Neema Hussein,** MPANDA

NI wiki mbili zilizopita, Nipashe ilipata fursa maalum na wazee walioshuhudia uhuru wa nchi na hali ilivyokuwa. Hapo anaanza, Mzee Thomas Yamboboto (81), mzaliwa wa Mpanda amesoma Shule ya Msingi Usevya katika Halmashauri ya Mpimbwe na baadaye aliendа kusoma Karema Seminari, mkoa wa Rukwa, mwaka 1954.

Anaeleza kabla ya Tanganyika kupata uhuru,

walipata habari za harakati za Mwalimu Julius Nyerere, kupitia taarifa za mapadri wa Kizungu waliowafundisha, wakisema " huko Dar es Salaam, kuna kijana mmoja ameanzisha Chama cha TANU, anadai uhuru sijui kama ataweza!"

Anaeleza, baada ya kutoka Karema Seminari, alijiunga na Mgodi wa Urwira Mpanda akifanya kazi. Wakati huo alisikia harakati za Mwalimu Nyerere zilizomtisha kutokana na ushujaa wake.

Anasema wazungu hao aliofanya nao kazi mgodini, walimtamkia:"Nyinyi mnasema 'huru huru huru,huru mtapata wapi?!' yaani mtu mmoja tu 'huru huru huru!' Mwalimu Nyerere 'Iko bongo nyingi sana; lakini nyingine yote pumbavu sasa kama nyingine yote pumbavu, halafu inasema huru huru huru itapata?"

Anasema, akiwa kwa mwajiri huyo, Mwalimu Nyerere, alifanya ziara Mpanda mwaka 1959 na akafika kuhamasisha wananchi kudai uhuru, wengi walikusayika .

Pia, anafafanua alitamani kumuona Mwalimu Nyerere kuwa mtu wa aina gani na akishiriki kumpokea stesheni ya treni, watemi wengi walikuwepo, milio ya bunduki na vigelegele vilitawala.

Hapo gari lilisukumwa, dereva aliambiwa alizime hadi Uwanja wa Kashauriri na walipofika Mwalimu Nyerere alianza kuhutubia, kukiwapo Wazungu wengi waliohudhuria mkutanoni, wakawa wanampiga picha.

Mzee Yamboboto anakumbusha kauli ya Nyerere: "Wananchi sisi tunadai uhuru, tupate uhuru. Hawa waliotutawala waondoke, kwa sababu kutawaliwa. Ni sawa na nusu utumwa na hawa mnaowaona rangi nyeupe, maana alikuwa hasemi wazungu, alisema hawa mfalme wao ni Malkia wa Uingereza.

"Kwa hiyo wananchi tujiunge wote tuwe kitu kimoja, ili tumuondoe mkoloni kwanza nasikitika tumetoka Tabora, tumekuja na garimoshi lenyewe linatumia moto wa kuni, uliona wapi gari itumie moto wa kuni inatembea kama kinyonga? Ndio maana mmenisubiri muda mrefu, lakini tukipata uhuru tunaondoa hizo kuni, tunaweka injini za mafuta."



Wazee waliokuwapo enzi ya Uhuru. **PICHA:MTANDAO**

Mzee Uzebius Mguluchuma, mwalimu mstaafu aliyesoma Shule ya Msingi Karema, ansema kipindi hicho kulikuwapo walimu wawili Waafrika waliofundisha shule hiyo, wakiwa na mwamko wa siasa.

Anasimulia walimu hao hawakupendwa na Wakoloni, lakini waliwaambukiza wanafunzi kupenda siasa na masuala la ukombozi.

Mzee Mguluchuma, anataja mkutano wa kwanza wa TANU uliofanyika hadharani, walimu hao waliwaruhusu wanafunzi kwenda kusikiliza eneo la Misunkumilo.

Mzee Thomas Ngozi, mzaliwa wa Mpanda, naye alisoma Shule ya Msingi Kampuni na baadaye, aliendelea na shule ya kati (middle school) Karema. Akiwa masomoni walimpata mwalimu mwanasiasa, kwa jina Leo Pinda.

"Huyu Mwalimu alikuwa akituambia, lazima tupate uhuru, lakini kulikuwa na Padri alikuwa akimpinga. Padri huyo alikuwa anaitwa Emil Jobido, ndio alikuwa Mkuu wa Shule.

"Alikuwa akiingia darasani anapinga, maana yeye alikuwa mzungu, lakini akiingia yule Mwafrika Leo Pinda anafundisha anasema 'lazima tuikomboe nchi yetu tupate uhuru' na akatuambia Mwalimu Nyerere ndio anatuongoza katika hilo.

"Baada ya masomo mpaka nilipomaliza darasa la nane, tulihamia Milala, ndio nilipomaliza masomo yangu mwaka 1956. Baada ya hapo nilikuwa Karani wa Baraza (mahakama) wakati huo watemi ndio walikuwa wanahukumu, wanasikiliza mashauri, walikuwa wao ndio watawala.

"Nakumbuka waliposikia tunakaribia kupata uhuru waliufunga mgodi wa Kampuni, wakihofia sisi Watanzania tutatajirika tukishapata uhuru na vifaa vilivyo kuwa pale wakavipeleka Uganda," anasema Mzee Ngozi.

Thomas Siwezi, anachangia akisema alimfahamu Nyerere kwa siasa zake alipozianzisha na mpaka kufikia kumuona pale kwenye mikutano yake na hata mpaka uhuru kupatikana chini ya Mwalimu Nyerere.

"Mwalimu Nyerere ni mtu mwema sana, lakini zamani tulikuwa tunakata kadi za chama cha TANU kwa kificho usionwe na wakoloni, mpaka tulipopata uhuru.

"Siku hiyo ya kupata uhuru, sisi ndio tulikuwa tunaitwa kwenye kiwanja kupeleka pombe kwenda kuuzia hapo kwa ajili ya kuandaa sherehe ya kupata uhuru. Kwa hiyo, usiku walipokuwa wakiteremsha bendera, tulikuwa kiwanjani tumepeleka pombe.

"Kwakweli Nyerere amefanya kazi nzuri sana bila matatizo yoyote na mpaka kupata uhuru mpaka leo hii tunasema tunaishi kwa ajili ya Mwalimu Nyerere," anasema Mzee Siwezi.

## SIKU YA UHURU

"Siku ya uhuru nilikuwepo na tayari nilikua nimeshakua Mwalimu hapa Mpanda, maana ualimu nilianza mwaka 1959 wakati inateremshwa bendera mimi na walimu wenzangu pamoja na wanafunzi tulifika hapo bomani kwenye mnara ambao upo pale mpaka sasa hivi.

"Tulikaa pale kusubiri bendera ya mkoloni iteremshwe na baadae waweze kutoa ishara kwamba sasa tumekuwa huru basi mizinga ilipigwa pale eneo la bomani.

"Wananchi walishangilia, walipiga vigelegele mno na kelele nyingi za kushangilia na kila mtu aliongea maneno kwa kabila lake, sasa nilikuwa sijui wengine walikuwa wanaongea nini," anasema Mzee Mguluchuma.

Mzee Ngozi anaendelea:" Nachokikumbuka kikubwa, sherehe zilifanyika katika Uwanja wa Kashauriri, palikuwa pana shamrashamra, ngoma, vigelegele na gwaride lilifanyika hapo,"

Michael Edward Lusambo, maarufu Mandevu, anakumbuka baada ya uhuru, kuna vitu viliongezeka ikiwemo watoto kupata vikombe shuleni.

Akawa mwanachama wa TANU vijana mstari wa mbele: Anafafanua: "Mimi nakumbuka sana kulikuwa na nyimbo baada ya uhuru zilikuwa zinaonyesha kwamba sisi Watanzania tulikuwa tumeburuzwa na walilipokea kwamba waliburuzwa."

Pia, anakumbuka nyimbo walizoimba, akidokeza mojawapo 'TANU yajenga nchi' na za kumsifu

Mwalimu Nyerere amewatoa utumwani.

"Baada ya uhuru huo sasa tukapata shule, maana kulikuwa hakuna, tukaendelea mara kilimo kikaongezeka hivyo tuliendelea kujua kwamba siasa ya Mwalimu Nyerere ndio ufunguo wa maisha. Pia, tukaelewa wazi hata wazee wa mila na mpaka leo mimi ni Mwenyekiti wa Kuhifadhi Mila na Desturi za Kitanzania," anasema Mzee Lusambo.

## MUUNGANO 1964

Mzee Ngozi anasema muungano ulipofanyika jijini Dar es Salaam, Mwalimu Nyerere wa Tanganyika na Abeid Karume wa Zanzibar, waliona waungane.

Mzee Ngozi anasema, pia Azimio la Arusha lilileta mwongozo na msimamo mzuri kwa viongozi wawe na nidhamu ya uongozi, akifafanua: "Bila ya Azimio la Arusha, ubinafsi ungeshamiri sana."

Anasema wengi hawakupata elimu, hivyo waliopata ajira ni waliokuwa na elimu na Mwalimu Nyerere alipata wakati mgumu kuongoza nchi kuelekea uhuru,

kutokana na mkoloni kutoacha kitu, ikilinganishwa na makoloni jirani kama Kenya, baadaye ilipotimu.

"Kwa hiyo Mwalimu alianza 'from the ground' yaani chini kabisa, ndio akaamua kwamba afuate siasa ya Ujamaa na Kujitegemea," anasema Mzee Ngozi.

Mzee Lusambo anasema 'Opresheni ya Vijiji vya Ujamaa' ilikuwa na lengo kuwahamisha watu wakae pamoja wahudumiwe kirahisi.

"Azimio hilo watu waliliona ni gumu hata mimi niliona nigumu kwa sababu nilihamishwa kwangu nikapelekwa huko, lakini baada ya kugundua baada ya kukaa pamoja tulipata shule, tukapata elimu na mimi pia nashukuru watoto wangu sa hizi wanasoma na shule zinazidi kuongezeka," anasema.

Mzee Yamboboto anazungumzia Muungano wa TANU na Afro Shirazi kwamba: "Kipindi vyama hivyo vinaunganaa bahati nzuri na mimi nilikua jeshini. Sisi tulikuwa makamisaa, kwa hiyo tulialikwa kwenye kile kikao kilichofanyika katika ukumbi wa Diamond Jubilee, Dar es Salaam.

"Kuvunja Chama cha TANU na kuvunja Chama cha Afro Shirazi, kuanzisha Chama cha Mapinduzi CCM, lakini Mapinduzi sio ya kumwaga damu ni ya kuleta maendeleo,"anasema Mzee Yamboboto.

MAKALA

## TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Kutoka kutumia vibatari, chemli, karabai hadi umeme

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Tanzania Bara inasherehekea miaka 61 ya Uhuru ilioupata kutoka kwa Uingereza mwaka 1961 wakati huo ikiitwa Tanganyika, nchi imepitia mambo mengi kisiasa, kiuchumi na hata kiteknolojia.

Leo hii kuna watu wanalalamika mgao wa umeme. Ni kweli wana haki kwa sababu kizazi cha sasa wanatumia zaidi umeme kwa ajili ya kujipatia kipato kwani kutokana na maendeleo ya teknolojia kuna kazi nyingi ambazo zinahitaji nishati ya umeme, lakini miaka ya 1961 hadi katikati tu ya miaka ya 1990 hata mijini tu, hakukuwa na nyumba nyingi zenye umeme.

Hata jiji kubwa kama Dar es Salaam, achilia mbali mikoa mingine, lilikuwa na nyumba chache sana zenye umeme na mara nyingi nyumba ya aina hiyo ndiyo watoto hupenda kwenda kucheza nyakati za usiku.

Ukiona nyumba yenye umeme, mara nyingi huwa ni ya mfanyabiashara wa duka, na si wote kwani wengine walikuwa wakitumia pia taa aina ya karabai.

Karabai ni taa ambayo unaweza kusema kwa wakati ule ndiyo ilikuwa ya thamani zaidi kuliko aina mbili zilizobaki, kibatari na kandili maarufu kama chemli.



Taa aina ya kibatari au koroboi



Taa aina ya kandili au chemli.

Mijini sehemu zingine ambazo zilikuwa na umeme ni zile za starehe kama baa, hoteli, kumbi za muziki, ukiacha zile nyumba chache za wafanyabiashara.

Wakati huo umeme haukuwa na kazi nyingi sana kama ilivyo sasa ambapo kila zaidi ya taa, na mambo mengine kama kuchezesha disco, muziki wa dansi na vitu vingine vichache, tofauti na sasa ambapo hata vitu vidogo tu vya kawaida kama saluni vinahitaji nishati hiyo.

Hakukuwa na watu ambao waliuhitaji kwa ajili ya kuangalia televisheni kwa ajili ya taarifa ya habari, mpira wala tamthilia Kwa sababu hazikuwepo.

Wala hakukuwa na mtu ambaye aliuhitaji kwa ajili ya kuchaji simu. Kwa sababu hazikuwepo. Kama nilivyosema huko nyuma kulikuwa na nyumba chache sana zilizokuwa na umeme, ambazo ndizo angalau unaweza ukaona feni na friji.

Feni na friji zilikuwa ni vitu adimu na yeyote anayekuwa navyo nyumbani kwake ambako lazima kutakuwa na umeme ili vifanye kazi anachukuliwa kama mtu mwenye uwezo mkubwa.

Unaweza kuuliza kama miji yenye joto kama Dar es Salaam watu walikuwa wanapoza wapi joto. Ni kwamba kulikuwa na watu ambao kazi yao ilikuwa ni kuuza maji ya baridi. Walikuwa wananunua barafu viwandani na kujaza maji, wakiuza mitaani. Lakini pia hata juisi ziliuzwa kwa njia hizo. Unakwenda sehemu unamkuta mtu na ndoo yake ya plastiki ana kikombe kikubwa, anachota na kukumiminia kwenye glasi, chochote unachohitaji kama ni juisi au maji.

Kutokana na kuwa na uhaba wa nyumba nyingi kuwa na umeme wakati huo, kulikuwa na aina tatu ya taa ambazo zilikuwa zinatumiwa sana wakati huo, kabla ya umeme kwa sasa kuenea karibuni kila nyumba nchini, lakini pia hata kama kutakuwa na tatizo la umeme, zipo taa zenye mwanga mkali ambazo zinatumia betri na zingine za kuchaji.

**TAA YA KOROBOI AU KIBATARI**

Kibatari ni jina la kiajemi ni taa ndogo ya kopo au chumba yenye utambi inayotumia mafuta ya taa au dizeli kuwaka.

Wakati huo kulikuwa na mafundi waliokuwa na karakana ndogo zisizokuwa rasmi za kutengeneza vibatari.

Waliokota makopo yoyote yale yawe ya maziwa, mafuta, samli au bidhaa zingine za kwenye makopo na kutengeneza vibatari.

Vilitumika majumbani na ndivyo wateja wengi kwa sababu, wananchi waliweza kuhimili kuvinunua kutokana na bei yake kuwa ndogo na hali zao za maisha.

Hata wananchi wa vijiji waliweza kununua vibatari na kuweka mafuta au dezili kwa ajili ya matumizi ya nyumbani nyakati za usiku na hata kusomea.

Tatizo lake ilikuwa ni moshi mweusi ambao kwa sasa wengi ndiyo wameanza kujua kuwa ulikuwa na athari, lakini kwa wakati ule ilionekana ni kawaida tu.

**TAA YA KANDILI AU CHEMLI**

Hii ni taa ambayo ilitumiwa na watu wenye uwezo kidogo. Wafanyakazi ambao walikuwa wakilipwa mishahara, wafanyabiashara au wenye uwezo kifedha hawakutumia vibatari ambavyo vilionekana kuwa ni vya watu wa hali ya chini.

Wajihi wa taa hiyo unaonekana kwenye picha. Ni kwamba kulikuwa na chupa ya glasi ambayo ilikuwa wazi katikati, na hii ilifunika sehemu ambayo kuna utambi unaowaka ili kutotoa moshi. Chini kuna tanki la kuwekea mafuta. Inasemekana aina hii ya taa ilianzia nchini Misri.

**TAA YA KARABAI**

Ni taa ilikuwa na mwanga mkali wakati mwingine kuliko hata umeme kwa wakati ule. Kwa sasa kuna aina ya glopu ambazo zina mwanga mkali na kufanana kabisa na karabai, tofauti na miaka ile ambapo glopu zake nyingi zilikuwa na mwanga wa kijani.

Karabai ilitumiwa na wavuvi kuvulia samaki kutokana na mwanga wake kuvutia samaki wengi, hasa wakati wa giza.

Aina hii ya taa ilikuwa adimu sana kuiona majumbani. Mara chache ilipokuwa inaonekana ni madukani na si yote.

Utambi wake ni kama kifuko kidogo hivi cha wavu mweupe ambacho kinachomwa na kupampu kama jiko la stovu na mwishoni unatokea mwaka mkali.

Na ndizo taa zilizokuwa zinatumika mara nyingi wakati huo hata wakati wa sherehe za kijamii majumbani au misiba kutokana na aina yake ya mwanga mkali. Taa hizo zilipatikana kwa kuazima au kukodisha.

**TUMA MESEJI 0716 350534**



Taa aina ya karabai

# Tanzania ya kwanza kwa kusimika intaneti ndani ya hifadhi za taifa

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

TANZANIA imeweka rekodi ya kuwa nchi ya kwanza barani Afrika, kusimika huduma ya mtandao wa intaneti katika hifadhi zake za taifa, baada ya kufunga na kuongeza kasi ya mawimbi yake kwenye mkongo wa taifa kufikia mps 100.

Kasi hiyo ya mawimbi ya intaneti, ndiyo ambayo inatumiwa na nchi zilizoendelea kuwavuta watalii kutangaza vivutio na uzuri wa hifadhi za taifa.

Jana, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, akizungumza wakati wa uzinduzi wa data kileleni katika Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro (KINAPA), alisema mradi huo ulianza kutekelezwa mwezi Julai na utakamilika mwishoni mwa Desemba, mwaka huu.

"TTCL (Shirika la Mawasiliano Tanzania) mmefanya sana kazi nzuri ya kizalendo, leo TTCL ina sura mpya,tumekusudia kuzungumza na dunia tukiwa kileleni na kuiambia dunia, roof ya dunia (paa) ipo Mlima Kilimanjaro.

Tanzania inakuwa nchi ya kwanza katika Bara la Afrika, kusimika huduma ya intaneti katika kilele cha Mlima Kilimanjaro. Takwimu zinaonyesha, tutakapofika kileleni, tutakuwa tuko juu kabisa duniani. Mita 5,895 kutoka usawa wa bahari. Tunataka tuvunje rekodi ya dunia," alisema.

Kwa mujibu wa Waziri Nape, awamu ya kwanza ya mradi huo ilihusisha usimikaji wa Mawasiliano hayo katika Kituo cha Horombo na awamu ya pili ni usimikaji katika kilele cha Uhuru cha Mlima Kilimanjaro, Desemba 13, mwaka huu.

Vituo vingine vilivyosimikwa mawasiliano hayo ni lango la Marangu, Kituo cha Mandara, Horombo, Kibo, Gilman's ,Stella na Uhuru.

"Shirika letu la TTCL, limefanikisha kujenga miundo mbinu ya mawasiliano ya intaneti kuanzia Marangu hadi Mandara (kilomita 9.5), Marangu hadi Horombo (kilomita 13),Horombo hadi Kibo (kilomita 14), Kibo hadi Uhuru (kilomita 5.2) na Kibo hadi Barafu, na hivyo kufanya eneo lenye huduma hii kuwa kilomita 44.7," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa TTCL, Peter Ulanga, akieleza kuhusu utekelezaji wa mradi huo alisema: Nina imani kubwa kabisa hapa tulipo tuna uwezo wa kuiambia Tanzania na Dunia, kwamba nchi hii imepiga hatua nyingi sana za matumizi ya kutumia mkongo wa taifa na kutumia teknolojia za kidigitali.

"Sina taarifa ya sehemu nyingine yeyote yenye mkongo wa mawasiliano duniani, ambao umefika umbali huo. Inatupa moyo sisi Watanzania, kwamba tunaweza kufanya jambo ambalo linagusika duniani. Tunaweza kujipambanua kama watu wenye uwezo, na tutahakikisha tunachukua changamoto kubwa zaidi kuweza kufikisha yote hayo," alisema.

Kwa mujibu wa mkurugenzi mkuu huyo, ifikapo mwaka 2023, TTCL itaendelea na mradi huo wa kusimika mawasiliano ya intaneti katika Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi.



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba (kushoto), akiagana na Waziri Ofisi ya Uratibu wa Sera wa Korea, Moon-Kyu Bang, baada ya kumalizika kwa mkutano kati yao, jijini Dodoma jana. Katika mazungumzo yao, Tanzania na Korea zimeahidi kuendeleza ushirikiano katika masuala ya kidiplomasia, kiuchumi na kijamii. **PICHA: WFM**

# NGO zatakiwa kushirikisha wenye ulemavu

**Na Frank Monyo**

TAASISI zisizo za kiserikali zimetakiwa kuzingatia ushiriki wa watu wenye ulemavu, ili wajitokeze kwenye uchaguzi na kutumia haki ya kuchagua viongozi bora wanaoamini watawaletea maendeleo.

Msajili wa Jumuiya Zisizo za Kiserikali Zanzibar, Ahmed Abdullah, alisema hayo jana wakati wa maadhimisho ya miaka mitano ya Mtandao wa Ushiriki Tanzanzia wenye mashirika wanachama 22.

Mtandao huo lengo lake ni kuwasemea vijana, wanawake na watu wenye ulemavu katika mambo mbalimbali ya kijamii.

"Bado kuna umuhimu wa kushirikisha watu wanaoishi na ulemavu kwa sababu unapoona kipindi cha uchaguzi ushiriki wa watu wenye ulemavu unahitaji kuzingatiwa," alisema.

"Watu wenye ulemavu katika kipindi cha uchaguzi wanatakiwa kutumia haki ya demokrasia kuwachagua viongozi bora na viongozi ambao wanawaamini na watashirikiana nao kuwapa mkutano vipaumbele kama Watu wenye ulemavu," aliongeza.

Alisema wapo katika kuhakikisha wanajenga dhana nzuri ya utawala bora, lakini pia kusaidia ukuaji wa demokrasia nchini.

Mwenyekiti wa Mtandao wa Ushiriki Tanzania, Israel Ilunde, alisema katika kuhakikisha wanakuwa na uchaguzi bora, wamehakikisha kumekuwa na mabadiliko ya kisera, kimfumo na kitaasisi.

Alitoa wito kwa jamii pamoja na wadau wengine wa maendeleo na serikali, kuunga mkono asasi za kiraia pale ambapo zinaanza kufanya kazi muhimu za kusaidia jamii ili kujenga nguvu za pamoja.

"Jamii pamoja na wadau wengine wa maendeleo na serikali tunaomba mziunge mkono asasi za kiraia pale ambapo zinaanza kufanya kazi muhimu za kusaidia jamii, ili waweze kupunguza mzigo ambao wanaufanya kwa kutumia nguvu ndogo kuwa pamoja , kujenga nguvu za pamoja kupitia mitandao," alisema Ilunde.

## Wizara yaandaa mkakati wa kuinua wanasayansi chipukizi

**Na Elizabeth Zaya**

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imesema itaendelea kutengeneza mazingira mazuri ya kuhakikisha kazi za kisayansi zinazobuniwa na wanasayansi chipukizi zinaendelezwa.

Makamu Mkuu wa Chuo cha Ardhi, Prof. Evaristo Liwa aliyasema hayo jana katika hafla ya utoaji tuzo kwa wanafunzi waliofanya vizuri katika maonyesho ya kazi za kibunifu za kisayansi yanayoratibiwa na Taasisi ya Wanasayansi Chipukizi (YST) katika shule za sekondari Tanzania Bara na Zanzibar.

Prof. Liwa ambaye alimwakilisha Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Aldof Mkenda alisema amefurahishwa kuona vijana wadogo wakibuni miradi mikubwa na mizuri.

"Wamenishangaza na hili ni jambo kubwa ambalo tukiliendeleza litatupatia wanasayansi wengi na wazuri wa kutatua matatizo katika nchi yetu.

"Kama waziri angekuwapo hapa, angetoa tamko kubwa, asingevumilia kuwaacha vijana hawa hivihivi kutokana na kazi nzuri walizofanya, hii ni hazina kubwa," alipongeza.

Alisema waziri amemtuma awaeleze kuwa wizara itaendelea kutengeneza mazingira mazuri ya kuendeleza kazi zao za ubunifu ili zitumike kutatua matatizo kwenye jamii.

"Serikali itafanya kwa sehemu yake, lakini ninawaomba wadau wengine wajitokeze wadhamini kazi hizi, tunataka zifanye kazi, tusiziache tu," Prof. Liwa aliagiza.

Mwanzilishi Mwenza wa YST, Dk. Gozibert Kamugisha alisema kwa miaka 12 mfululizo wamekuwa wakiibua vipaji vya wanafunzi kutoka katika mikoa mbalimbali kwa kuwawezesha kubuni miradi tofauti ya kisayansi inayolenga kutatua matatizo kwenye jamii inayowazunguka.

Alisema tayari kazi hizo zimeanza kuleta matokeo chanya kwa kuwavutia wanafunzi wengi kupenda masomo ya sayansi.

Alisema wale wanaofanya vizuri zaidi wamekuwa wakipata zawadi za udhamini wa masomo ya vyuo vikuu, kupewa medali, fedha taslimu na wengine kupelekwa nje ya nchi kushiriki na kushindania tuzo za miradi ya kisayansi.

"Na kote huko wamekuwa wakifanya vizuri, lengo letu ni kuhakikisha tunatengeneza wanasayansi wengi na tunataka kila mwanafunzi kabla ya kumaliza kidato cha nne awe amebuni kitu chochote chenye tija katika jamii, hiyo ndiyo sayansi tunayoitaka," alisema.

Ofisa Mtendaji wa Shirika la Karimjee Jivanjee Foundation ambao ni wadhamini wakuu wa maonyesho hayo, Caren Rowland alisema hadi mwaka jana shirika hilo limedhamini wanafunzi 37 kwenda vyuo vikuu na mwaka huu watafanya hivyo kwa wanne watakaoshinda katika maonyesho hayo.

Alisema lengo ni kujenga msingi kwa wanafunzi hao kuwa na ari ya kitaaluma na kupenda masomo ya sayansi.

# HABARI PICHANI



Sehemu ya wahitimu wa Taasisi ya Ustawi wa Jamii, wakiwa kwenye mahafali ya 46 chuoni hapo, Kijitonyama, Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA.**



Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, Fatma Nyangasa (kulia), akiteta jambo na Mkuu wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Prof. Shadrack Mwakalila, wakati wa Kongamano la Maadhimisho ya Miaka 61 ya Uhuru wa Tanganyika, chuoni hapo, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Wafanyakazi wa mkandarasi wakiendelea na ukarabati wa Barabara ya Sokoine, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: IMANI NATHANIEL**



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu Zanzibar, Jamali Kassim Ali, akimkabidhi tuzo Mhasibu Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, CPA Johnson Gamba (kulia), baada ya kuibuka mshindi wa pili katika kundi la mikoa kwa uandaaji wa hesabu kwa mwaka 2021. Tuzo hizo zilitolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA), Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Wakili Mwandamizi wa GGML, David Nzaligo (kushoto), akitoa maelezo kwa Kamishna wa Polisi Operesheni na Mafunzo, Awadhi Juma (kulia), alipotembelea ofisi ya kampuni hiyo mkoani Geita, mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# HADITHI

MAWENI ni moja kati ya vijiji nchini ambavyo vipo mbali na makao makuu ya mkoa. Kutokana na kuwa vipo kilometa nyingi, miundombinu yake na mawasiliano yamekuwa hafifu, kitu ambacho kimewapa baadhi ya viongozi wa kijiji kiburi kufanya wanavyotaka. Wameingia mkataba wa kitapeli na kinyonyaji na tajiri aliyejifanya mwekezaji, kuwanyang'anya mashamba wanakijiji na kumuuzia. Badala yake wanakijiji wanalima kwenye ardhi aliyouziwa mwekezaji huyo. Mazao yaliyopatikana anayachukua na kuwalipa wanakijiji hao pesa kidogo ambayo haiwatoshi kujikimu kwa msimu mzima. Tajiri, watoto wake na viongozi wa kijiji pia wamekuwa na tabia ya kunyanyasa kijinsia watoto wa kike. Mary, mmoja wa wasichana warembo kijiji hapo ni mmoja ya waliopata shida hiyo. Hawana kwa kupeleka malalamiko, wala wa kumlilia, isipokuwa Mungu tu. Fuatana na mtiririko wa kisa hiki.

# Mtake Msitake-9

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**




Kulikuwa na habari nyingi tofauti, kila mmoja akisema lake. Kila mmoja akidai analosimulia yeye ni sahihi kiasi cha kuwachanganya wapokeaji wasijue ukweli ni upi.

Kama kawaida ya maneno ya kusikia kila anayepokea na kwenda kulisimulia kwa mwingine ni lazima kitiwe chumvi lau kidogo ili kumnogesha anayeambiwa.

Vyovyote itakavyokuwa ukweli ukabaki pale pale kuwa Adel amemwagiwa kitindikali machoni na amelazwa kwenye hospitali ya mkoa, hali yake ilielezwa kuwa ni mbaya sana. Hata hivyo hakuna yeyote ambaye ametajwa kufanya tukio hilo wala kutaja mahali alipomwagiwa. Madaktari hawajasema lolote, lakini uvumi unasema kuwa huenda akawa haoni tena, au akapoteza macho yake.

Ingawa alikuwa mgeni lakini hali ya taharuki ilionekana kijijini hapo, hasa ikizingatia wanaodaiwa kufanya hivyo ni wanakijiji.

Wa kwanza ni Mary, wa pili Enock ambaye ni mchumba wa Mary na wa tatu ni Usonzo, tajiri mwekezaji ambaye naye amekufa na kuoza kwa binti wa watu Mary.

"Usonzo nimekuja, naomba unisaidie kwa hili." Ilikuwa ni sauti ya Mary akiwa kwenye ofisi za mwekezaji Usonzo.

Mwenyewe aliona ni bahati ya mtende. Msichana mrembo kama yule ambaye siku zote alikuwa akimtongoza, lakini alikuwa anamkataa kata kata. Leo kaenda mwenyewe kwa mguuni mwake ofisini kwake kusaidiwa.

Aliangua kicheko. Kilionekana ni kicheko cha furaha kilichochanganyikana na cha ushindi.

"Umekuja leo kijana eee, mtoto matata sana wewe, unayekataa hata matajiri. Haya kuna nini leo?"

"Naomba unisaidie kuniokoa kwenye hili janga, vinginevyo naweza kufungwa." Aliongea kwa sauti ndogo ya woga.

"Wewe sema, usizunguke mrembo." Usonzo akaunguruma.

"Mimi ndiye niliyemwagia Adel Adam tindikali, yule kijana mgeni na madaktari wamethibitisha kuwa amekuwa kipofu. Hatoona tena milele. Sasa taarifa zimeshafika kwa Mwenyekiti wa Kijiji mzee Chale, nimesikia kesho nitaitwa. Naogopa atakwenda kupeleka taarifa hizi kituo cha Polisi mkoani." Aliongea kwa woga na unyeyekevu mkubwa.

**"Nataka umzuie mzee Chale asilipeleke suala hili Polisi. Akilipeleka nimekwisha. Wewe ni rafiki yake, unaweza ukafanya lolote lile, ndiyo maana nimekuja kwako."**

Usonzo alikuwa ameshazipata taarifa hizo, ingawa alikuwa hajui mgeni huyo alimwagiwa na Mary, au mchumba wake Enock.

"Taarifa zimeshanifikia, nilikuwa nataka kupata uthibitisho ni nani. Ngoja nikuulize swali. Kwa nini umemwagia tindikali wakati ni mpenzi wako?"

"Hapana, siyo mpenzi wangu. Ni kweli alikuwa ananitaka, lakini hakuwa mpenzi wangu."

"Siyo kama umeamua kufanya hivyo ili kufuta ushahidi?"

"Hapana mzee Usonzo, yule kijana aliniokoa kwenye ajali ya bodaboda, ndiyo nikafahamiana naye. Kuna siku nilikutana naye nikiwa na mchumba wangu Enock, nikamtambulisha. Wakawa marafiki, kuna wakati wakawa wanatembeleana na yeye akawa anaweza kuja hata kwetu. Akatumia njia hiyo kunitongoza. Nilimkatalia, akawa anazidi kufanya hivyo, nikaona hali ikizidi kubwa mbaya Enock akijua itakuwa matatizo, siku moja akaja nyumbani, akawa ananishikashika, kwa hasira, nikaenda kuchukua tindikali ya baba alikuwa kuna sehemu kaificha, nikamwagia."

Usonzo alimtazama kwa uchu msichana yule, aliyekuwa amevaa gauni laini lililombana na kuonyesha umbile lake vema. Ukiongeza na sura yake ya ujana kama ua linalochanua, lilimvuruga Usonzo.

"Enhee, sasa wewe ulitaka mimi nifanye nini?" Akauliza akiwa anaondoa macho yake kwenye sura ya Mary na kuielekeza kwenye mafaili yaliyo kwenye ofisi yake pamoja na kompyuta.

"Nataka umzuie mzee Chale asilipeleke suala hili Polisi. Akilipeleka nimekwisha. Wewe ni rafiki yake, unaweza ukafanya lolote lile, ndiyo maana nimekuja kwako."

"Tatizo wewe binti unajifanya mjanja. Mimi nilikutaka siku nyingi sana. Ukanikataa tena kwa maneno mabovu. Leo umeona umuhimu wangu eee? Sasa mimi hili swala kwangu ni dogo mno kuliko kuua panzi, nzi au mbu. Ni kiasi cha kukaa naye kumpa mzigo tu, yaani pesa kidogo, tunaiua hii skendo humu humu kijijini, haitoki nje. Lakini kwa sharti moja tu." Safari hii aliongea kwa sauti kidogo ya msisitizo.

"Mimi niko tayari kwa sharti lolote utakalonipa, lakini hili liishie humu."

"Nataka unikubalie, niwe mpenzi wako."

Mary aliangalia juu kama kuna kitu anafikiri, akajibu.

"Mimi sina neno na hilo. Niko radhi, ila tu itabidi univumilie kidogo."

"Kuna nini tena?" Akang'aka.

"Nilikuwa na matatizo ya tumbo, nikaenda hospitali, nikapimwa na kupewa dawa za kutumia ambazo naendelea kuzitumia. Sasa walinaimbia nisifanye kitu chochote kwa miezi mitatu. Ikiisha tu basi tutaanza rasmi uhusiano," akaongea kwa sauti ndogo na ya aibu.

"Mimi nitajuaje kama dozi hiyo imeisha baada ya kufika miezi mitatu?"

"Nitakwambia, lakini na wewe hesabu kuanzia mwezi huu, ikiisha sina hata haja ya kukwambia. Ila naomba sasa usiwe uko sana karibu yangu, si unajua nina mchumba, Enock?"

"Najua Mary. Imeisha hiyo. Mimi kesho tu nitakwenda kwa mzee Chale. Hana tatizo yule anapenda pesa tu, nikimpa milioni zake mbili tu, atanyamaza. Halafu shoo nasimamia mimi mwenyewe. Nitamwambia habari hii haitakiwi kuvuka kijijini hapa."

"Nitashukuru sana."

"Kama kweli umenikubali, hebu naomba nikubusu."

Kwa aibu za kike, Mary aligeuza kichwa chake. Usonzo akapeleka mdogo wake shavuni, akambusu.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# MFAUME AJIANDAA KUMPIGA PIARALI USIKU WA MABINGWA

**Na Saada Akida**

JOTO la pambano la Usiku wa Mabingwa linazidi kupanda baada ya bondia maarufu wa ngumi za kulipwa nchini, Mfaume Mfaume, kutamba yuko kamili kumdunda mpinzani wake, Iddi Piarali, katika pambano litakalofanyika DEsemba 26, mwaka huu kwenye Ukumbi wa AICC, ulioko jijini, Arusha.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mfaume alisema amejiandaa vizuri kuelekea pambano hilo na anaamini ataibuka na ushindi kutokana na ubora aliokuwa nao.

Mfaume alisema amepanga kulimaliza mapema pambano hilo kutokana na kumsoma vyema Piarali.

Bondia huyo alisema anahitaji kumaliza mwaka huu vizuri na kuanza mwaka mpya wa 2023 kwa furaha huku pia akiwapa heshima mashabiki wake wanaoishi Mabibo, Dar es Salaam.

"Nimejiandaa vizuri kuelekea pambano letu hilo, ninachoahidi ni kufanya vizuri, nitahakikisha siwaangushi watu wangu wa Mabibo kwa kumchapa mapema mpinzani wangu Piarali katika pambano hilo," alisema Mfaume.

Aliongeza atacheza kwa nidhamu ya hali ya juu kwa sababu anahitaji ushindi na mazoezi ya muda mrefu aliyofanya yamemsaidia kuimarika kuelekea pambano hilo.

Mabondia wengine watakaopanda ulingano siku hiyo ni pamoja na Zawadi Amos ambaye atapigana na Halima Vunjabei wakati Shabani Kaoneka yeye atatoana jasho dhidi ya Shabani Ndaro huku Saidi Faraji atapambana na Osama Arabi.

Bondia mwenye mbwembwe na aliyejizolea umaarufu katika siku za hivi karibuni, Kareem Mandonga yeye atapigana na Ali Baba na pambano lingine litakalowahusisha mabondia wanawake litakuwa ni kati ya Batuli Yassin dhidi ya Loveness Kokha.




Wachezaji wa timu ya mpira wa kikapu ya Vijana wakifanya mazoezi ili kujiweka imara kwenye Uwanja vya Jakaya Kikwete Youth Park uliopo jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Edna atimuliwa Yanga Princess

**Na Adam Fungamwango**

MABOSI wa Yanga wametangaza kuachana na Kocha Mkuu wa Yanga Princess, Edna Lema, ikiwa ni siku mbili zimepita tangu timu hiyo ilipofungwa mechi yake ya kwanza ya Ligi Kuu ya Wanawake iliyoanza mapema wiki hii.

Edna ametimuliwa sambamba na msaidizi wake, Mohamed Hussein 'Maachinga.'

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema kuondoka kwa Edna na Mmachinga ni suala la kawaida kwa sababu hakuna kocha duniani anayekaa kwenye klabu moja daima.

"Hakuna shida, kocha Lema tumekuwa naye muda mrefu, tunaheshimu mchango wake, duniani kote hakuna kocha anayekaa milele kwenye timu bora, unaweza kuwa bora lakini usifanikishe kitu ulichoahidiana na mwajiri wako, kilichotokea ni makubano ya pande zote mbili, sisi klabu na benchi la ufundi. Kuna malengo ambayo tuliwaweka, sisi na wao, lakini hapa tulipofikia tumeona nafasi wakatafute changamoto nyingine, na wala hatujatibuana, ila tumekubaliana tu," alisema Kamwe.

Lema ameishukuru Yanga kwa ushirikiano waliompa wakati wote alipokuwa akiifundisha timu hiyo.

"Yanga imekuza na kunifanya kuwa mkubwa pengine hata ukubwa nisiostahili kwa sababu ya ukubwa wa klabu, najua kila shabiki anaitakia mema timu na anatamani ipate mafanikio, nilijitahidi kufanya kile kilichokuwa ndani ya uwezo wangu lakini kwa sasa inatosha kwa hapa nilipofika mpaka wakati mwingine," alisema kocha huyo.

## Taifa Jang'ombe, Dulla Boys mkiani

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TAIFA Jang'ombe na Dulla Boys ndio timu zinazoongoza kwa kufungwa mabao katika michezo za Ligi Kuu Zanzibar ambayo mzunguko wake kwanza umemalizika kwa kila klabu kucheza michezo 15.

Timu hizo mbili zote zimefungwa michezo 10 kati ya michezo 15 waliyocheza katika Ligi hiyo yenye timu 16.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Dulla Boys, Abdulmutik Ali, alisema anahitaji kukifanyia maboresho makubwa kikosi chake kuelekea kipindi cha mapumziko ya ligi hiyo.

Ali alisema anatarajia kusajili wachezaji wapya kwa ajili ya kukioongezea nguvu kikosi hicho ili kipate matokeo mazuri na kujinusuri na janga la kushuka daraja.

Alitaja nafasi ambazo ataziboresha ni ya ulinzi na anatarajia kusajili wachezaji wenye uzoefu huku pia akihitaji na washambuliaji.

## Joto laikwamisha netiboli Mbeya

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa timu ya netiboli ya Mbeya, Moses Aizengo, amesema wameshindwa kufanya vyema katika michezo minne waliyocheza ya Ligi Daraja la Pili inayoendelea kwenye Uwanja wa Ndani wa Benjamin Mkapa kutokana na hali ya hewa kutokuwa rafiki kwao.

Aizengo alisema hali ya hewa ya joto la Dar es Salaam limewaathiri wachezaji wake na kusababisha kushindwa kuonyesha uwezo wao.

"Wachezaji wangu wameshindwa kufanya vizuri kwenye michezo yetu ya mwanzo kutokana na kuathiriwa na hali ya hewa, wamezoea kuishi mazingira yenye baridi, lakini hapa (Dar es Salaam) ni tofauti," alisema Aizengo.

Kocha huyo alisema walifanya maandalizi ya muda mrefu kwa ajili kuhakikisha wanafanya vizuri na hatimaye wanapanda daraja lakini matokeo waliyopata hakutarajia.

"Tunaendelea kujiandaa na mchezo wa mwisho tutakaocheza dhidi ya NSSF ya Dar es Salaam, naamini tutafanya vizuri kwa sababu tumeshawafahamu wapinzani wetu," aliongeza kocha huyo.

## ZISIKUPITE

### GARNACHO ATAKIWA MADRID
REAL Madrid inavutiwa na winga wa Manchester United, Alejandro Garnacho, raia wa Argentina mwenye umri wa miaka 18 ambaye alifunga bao lake la kwanza la Ligi Kuu England dhidi ya Fulham mwezi uliopita. ***(Revelo)***

### SOMMER ANUKIA UNITED
KLABU ya Manchester United inashughulikia mpango wa kumsajili golikipa wa Borussia Monchengladbach na Timu ya Taifa ya Uswisi, Yann Sommer, mwenye umri wa miaka 33 kwa uhamisho wa bure msimu ujao. ***(ESPN)***

### ENDRICK SAFI MADRID
REAL Madrid wamekubali mkataba wa miaka sita wenye thamani ya karibu pauni milioni 62 wa kumsajili kijana wa Brazil, Endrick kutoka Palmeiras, lakini mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 16 hatajiunga na klabu hiyo hadi Julai, 2024 atakapokuwa na umri wa miaka 18. ***(Fabrizio Romano)***

### ZIYECH ANUKIA MILAN
AC Milan ipo tayari kumnunua mshambuliaji wa Chelsea, Hakim Ziyech mwenye umri wa miaka 29, ambaye amefanya vyema kwenye Kombe la Dunia akiwa na Timu yake ya Taifa ya Morocco. ***(Gazzetta dello Sport via Football Italia)***

### LEAO ATAKIWA KUAMUA
AC Milan imemwambia mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ureno, Rafael Leao mwenye umri wa miaka 23 kuamua kama ansaini mkataba mpya au anaondoka klabuni hapo. ***(Calciomercato)***

### PSG YAMWINDA RASHFORD
RAIS wa Paris St-Germain, Nasser Al-Khelaifi ameseaa mshambuliaji wa Manchester United na Timu ya Taifa ya England, Marcus Rashford mwenye umri wa miaka 25, anaweza kutafutwa na klabu hiyo ya Ufaransa msimu ujao. ***(Sky Sports)***

### RASHFORD ANOGEWA KUFUNGA
AKIWA tayari amefunga mabao matatu kwenye Kombe la Dunia, Marcus Rashford amesema hakuna kitu kinachompa furaha zaidi ya kuifungia nchi yake. ***(Mirror)***

### PSG: MESSI ATABAKIA HAPA
RAIS wa PSG, Al-Khelaifi amesema ana uhakika mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Argentina, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 35, ataongeza muda wake wa kukaa Paris watakapojadili mustakabali wake ifikapo Januari. ***(Sky Sports)***

### ARSENAL KUINGIA SOKONI
ARSENAL "itaangalia machaguo yaliyopo" baada ya mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Brazil, Gabriel Jesus kupata jeraha la goti kwenye Kombe la Dunia nchini Qatar, amesema Kocha, Mikel Arteta. ***(Football London)***

### MADDISON ATAJWA NEWCASTLE
KIUNGO wa kati wa Leicester na Timu ya Taifa ya England, James Maddison mwenye umri wa miaka 26, ndiye anayelengwa na Newcastle United katika uhamisho wa Januari. ***(90 min)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RICE KAMILI KUIBEBA ENGLAND VS UFARANSA

**Kiungo huyo nyota anatarajia kuiongoza vyema timu yake na kuhakikisha...**

**DOHA, Qatar**

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya England, anayekipiga katika klabu ya West Ham, Declan Rice, yuko fiti kuikabili Ufaransa leo, ameeleza mchezaji mwenzake, Kalvin Philips.

England inatarajiwa kucheza dhidi ya Ufaransa katika mchezo wa robo fainali ya Kombe la Dunia.

Kiungo huyo alikosekana mazoezini Jumatano kutokana na maumivu ambayo hayakuwekwa wazi hivyo kuleta taharuki kubwa huenda atakosekana katika mchezo wa robo fainali hiyo.

Philips ambaye alitengeneza muunganiko bora na Rice katika michuano ya Euro mwaka 2020 na kuiwezesha timu hiyo kufika fainali ameonyesha kutokuwa na wasiwasi na kiungo mwenzake huyo kuwapo katika mchezo wa leo.

"Nina uhakika atakuwa kwenye kikosi kesho (leo), yupo fiti na ameonyesha ari kubwa ya kutaka kucheza," alisema Philips akinukuliwa na BBC Sport.

"Kwa uhakika ninaamini atakuwa bora na ana mchango mkubwa sana kwenye kikosi chetu, hivyo ninamtarajia kwa makubwa."

Rice amekuwa mhimili na mchezaji wa kutegemewa kwenye safu ya kiungo ya England chini ya Kocha, Gareth Southgate kutokana na ubora ambao ameuonyesha tangu alipoanza kupata nafasi kwenye timu hiyo.

Mchezo huo unatarajiwa kuwa wa kusisimua kutokana na ubora wa timu zote mbili.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,056,5
MECHI KALI
ENGLAND
VERSUS
FRANCE
1 | 2.96
X | 3.21
2 | 2.38
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa
airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# FAMILIA YA GLAZER YAKOSA MGAO MANCHESTER UNITED

**MANCHESTER, England**

MATOKEO ya robo ya kwanza ya kifedha ya Manchester United ambayo yalitolewa Alhamisi yanaonyesha familia ya Glazer haijapata mgao kwa mara ya kwanza tangu mwaka 2016 baada ya kutangaza kuiuza klabu hiyo.

Wamiliki hao walikosolewa kwa kuchukua gawio la paundi milioni 11 kutoka kwenye klabu hapo Juni, mwaka huu lakini bodi ya wakurugenzi, ambayo inaundwa na ndugu sita wa Glazer, haikuidhinisha malipo ya hivi karibuni ya nusu mwaka kwa wanahisa.

Takwimu zinaonyesha mapato ya United yalipanda kwa asilimia 13.6 na klabu hiyo inalenga kupata kati ya pauni milioni 590 na 610 kwa mwaka mzima, ingawa imepata hasara ya kabla ya kodi ya pauni milioni 2.5.

Uamuzi huo kutoka kwenye bodi ya wakurugenzi ya United umetajwa kuwa wa kiuchumi, kwa mujibu wa The Athletic, huku mambo yakibainishwa ikiwa ni pamoja na kutumia zaidi ya paundi milioni 200 msimu wa joto, hii ilihusu usajili wa wachezaji kama vile Antony, Casemiro, Lisandro Martinez na Tyrell Malacia.

Uamuzi wa bodi ya wakurugenzi wa kutoidhinisha gawio unakuja baada ya Joel Glazer kuhojiwa kuhusu suala hilo wakati wa mkutano wa bodi ya ushauri wa mashabiki wa United hivi karibuni.

# Barca, Chelsea zamwania Moukoko

**LONDON, England**

KLABU za Barcelona na Chelsea zimeripotiwa kumhitaji mchezaji wa Borussia Dortmund, Youssoufa Moukoko katika dirisha dogo la usajili la Januari, nyota huyo anapokaribia mwisho wa mkataba wake.

Moukoko (18) amekuwa na Dortmund tangu akiwa na umri wa miaka 12, mwaka juzi alicheza kwa mara ya kwanza katika kikosi cha kwanza kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na kuvunja rekodi ya kuwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi katika historia ya mashindano hayo.

Yeye pia ndiye mfungaji mabao mwenye umri mdogo zaidi katika historia ya Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, na baada ya kutumika hasa akitokea benchi hadi kufikia hatua hii katika maisha yake ya soka, alianza mechi saba mfululizo za ligi kabla ya mapumziko ya Kombe la Dunia.

Akiwa na mabao sita na kutoa pasi tatu za mabao katika mechi 14 za Bundesliga msimu huu, ameibuka kuwa mmoja wa watu wanaotarajiwa kuimarika katika soka la dunia, lakini muda wake huko Dortmund unaweza kumalizika.

Mkataba wa Moukoko unamalizika mwishoni mwa msimu huu, na ikiwa hatasaini mkataba wa nyongeza kubakia Dortmund, ataweza kuondoka kama mchezaji huru.



554,107/-

# NIYONZIMA ATAJWA, POLISI TANZANIA IKIMTEGA ZAHERA

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Polisi Tanzania umempa, Kocha Mkuu, Mwinyi Zahera, mamlaka kamili ya kusajili wachezaji katika dirisha dogo la usajili kwa ajili ya kuhakikisha anakinusuru kikosi hicho na janga ya kushuka daraja kwenye Ligi Kuu Bara.

Aliyekuwa kiungo wa Yanga na Simba, Haruna Niyonzima, ni miongoni mwa nyota anayehusishwa na Maafande hao ili kuja kuongeza nguvu.



Akizungumza na gazeti hili jana, Makamu Mwenyekiti wa Polisi Tanzania, Robert Munisi, alisema baada ya kuimarisha benchi lao la ufundi sasa wanasubiri mapendekezo ya usajili kutoka kwa Zahera na ndiyo watayafanyia kazi.

Munisi alisema licha ya kupata matokeo mabaya katika mzunguko wa kwanza wa ligi hiyo, bado wanaimani na timu yao itazinduka na kupata matokeo mazuri katika michezo ya duru la pili.

"Tumepata ufumbuzi tumeanza na kumwajiri mwalimu, na sasa atakuwa na jukumu la kuangalia maboresho ya usajili hasa anahitaji kuongeza nguvu wapi baada ya kuona mapungufu ya kikosi cha timu yetu.

Niwakakikishie Polisi Tanzania haishuki daraja kwa sababu tunaimani na kocha aliyepewa jukumu sasa ni mzoefu, tutafanya usajili kulingana na mapendekezo yake ili kukijenga kikosi," alisema Munisi.

Aliongeza kwa sasa anafahamu nafasi waliyopo si salama lakini hali hiyo itabadilika mara baada ya duru la pili kuanza.

Katika msimamo wa Ligi Kuu, Polisi Tanzania inashika mkia ikiwa na pointi tisa baada ya kushinda mechi mbili, sare tatu na wamepoteza michezo 10.

## Yanga yamtamani Bruno wa Singida

INATOKA UK. 32

ndiyo maana tulisajili wachezaji wazuri, hatuna mpango wa kuuza wachezaji wetu tunaowategemea, tunashukuru wachezaji wetu wametupatia kile ambacho tulikuwa tunakihitaji mpaka sasa, " alisema Masanza.

Ofisa huyo alisema timu yao imekuwa na mafanikio makubwa katika mzunguko wa kwanza wa msimu wao kwanza katika Ligi Kuu Tanzania Bara kwa kuwa kwenye nafasi ya nne katika msimamo.

"Mzunguko wa kwanza tuko kwenye nafasi ya nne, haya ni mafanikio makubwa kwetu na tulihitaji mpaka mwisho wa msimu tuwe hapa au juu ya msimamo ili kwenda kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa," alisema Ofisa huyo.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, aliliambia gazeti hili klabu yao haitashindwa kumpata mchezaji yoyote ambaye itamhitaji ili kuongeza nguvu.

Kamwe alisema uwezo wa kufanya hivyo wanao, na sasa wanachosubiri ni mapendekezo kutoka kwenye benchi la ufundi la timu yao.

## SIMBA YAKAMILISHA

INATOKA UK. 32

wa leo atamkosa, Nelson Okwa, ambaye bado anaendelea na kujiweka sawa baada ya kutoka kwenye majeruhi.

Naye Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema kikosi chao kiko imara na kwao kila mechi ni sawa na fainali.

Ahmed alisema wataingia uwanjani kusaka ushindi kwa sababu ndio matokeo yatakayowapeleka hatua inayofuata kwenye mashindano hayo.

"Tutapambana kwa nguvu zote ili kuhakikisha tunapata ushindi, huwezi kusonga mbele kama utakosa ushindi, kwetu kesho (leo), ndio tunaanza fainali ya kwanza ya Kombe la FA, hatutadharau kila timu tutakayopangiwa nayo kwenye michuano hii," Ahmed aliongeza.

Mechi nyingine za michuano hiyo zitakazofanyika leo ni kati ya JKT Tanzania watakaokuwa wenyeji wa Biashara United, kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo wakati Majimaji watawakabili Kengold FC kutoka Mbeya na Mashujaa watawaalika Pamba FC kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani, Kigoma.

E4M FC na New Dundee zenyewe zitakutana kwenye Uwanja wa Samora, Afya FC watawakaribisha African Sports kwenye Uwanja wa Vwawa, Nzega United itakabiliana na KFC FC (Uwanja wa Samora) huku Transit Camp wakiwafuata Geita Gold FC kwenye Uwanja wa Nyankumbu ulioko Geita.

Ihefu watawaalika Mtama Boys kwenye Uwanja wa Highland Estates, Kagera Sugar watakuwa wenyeji wa Buhare FC kwenye dimba la Kaitaba, Dodoma Jiji dhidi ya TMA Stars kwenye Uwanja wa Jamhuri, Mbao FC watakuwa na kibarua dhidi ya Mapinduzi, Ruvu Shooting nao wataonyeshana ubabe na Ndanda kwenye Uwanja wa Uhuru wakati Wagosi wa Kaya Costal Union, watakuwa Mkwakwani kumenyana na Tanga Middle.


SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. 10/12/22 | 18:00 | Blackpool vs Birmingham | 2.68 | 3.28 | 2.58 |
| 2. 10/12/22 | 18:00 | Swansea vs Norwich City | 2.37 | 3.38 | 2.88 |
| 3. 10/12/22 | 18:00 | Lincoln vs Wycombe | 2.83 | 3.28 | 2.46 |
| 4. 10/12/22 | 18:00 | Bristol Rovers vs Port Vale | 2.52 | 3.32 | 2.72 |
| 5. 10/12/22 | 18:00 | Oxford Utd vs Barnsley | 2.34 | 3.29 | 2.99 |
| 6. 10/12/22 | 18:00 | Grimsby vs Tranmere | 2.26 | 3.19 | 3.24 |
| 7. 10/12/22 | 18:00 | Salford City vs Walsall | 2.42 | 3.20 | 2.95 |
| 8. 10/12/22 | 21:00 | Villarreal B vs Tenerife | 2.74 | 2.83 | 2.88 |
| 9. 10/12/22 | 22:00 | England vs France | 3.04 | 3.24 | 2.43 |
| 10. 11/12/22 | 16:00 | Genclerbirligi vs Erzurum BB | 2.53 | 3.48 | 2.58 |
| 11. 11/12/22 | 16:00 | Gillingham vs Bradford City | 3.24 | 3.14 | 2.28 |
| 12. 11/12/22 | 16:00 | QPR vs Burnley | 3.08 | 3.33 | 2.27 |
| 13. 11/12/22 | 16:30 | Calcio Lecco vs Padova | 2.31 | 3.06 | 3.16 |
| 14. 11/12/22 | 16:30 | Feralpisalo vs Novara | 2.26 | 3.05 | 3.40 |
| 15. 11/12/22 | 16:30 | Roda Kerkrade vs Heracles | 2.59 | 3.43 | 2.59 |
| 16. 11/12/22 | 16:30 | De Graafschap vs FC Eindhoven | 2.41 | 3.43 | 2.79 |
| 17. 11/12/22 | 16:30 | Mantova vs Pro Vercelli | 2.60 | 3.05 | 2.90 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 10/12/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 1026 | Tuzlaspor vs Caykur Rizespor | 3.36 | 3.41 | 1.97 |
| 13:30 | 1829 | Keciorengucu vs Adanaspor | 1.73 | 3.61 | 4.10 |
| 14:30 | 1225 | Perth Glory vs Western United | 2.83 | 3.47 | 2.31 |
| 14:30 | 1391 | Hangzhou NG vs Meizhou Kejia | 1.63 | 3.80 | 4.49 |
| 14:30 | 1534 | Chengdu Qianbao vs Shanghai SIPG | 2.78 | 3.36 | 2.26 |
| 14:30 | 4949 | Guangzhou Evergrande vs Guangzhou RF | 2.48 | 3.40 | 2.48 |
| 15:00 | 2929 | Blackburn vs Preston | 2.16 | 3.16 | 3.31 |
| 15:00 | 3034 | FC Goa vs Delhi Dynamos FC | 2.12 | 3.50 | 2.92 |
| 15:00 | 4709 | Tianjin Teda vs Henan Jianye | 2.90 | 3.45 | 2.30 |
| 15:00 | 5064 | ASK Bravo vs Luka Koper | 2.72 | 3.20 | 2.39 |
| 15:30 | 1374 | Rotherham vs Bristol City | 2.78 | 3.27 | 2.41 |
| 15:30 | 2518 | Shrewsbury vs Bolton | 3.21 | 3.21 | 2.19 |
| 15:30 | 3334 | Ipswich vs Peterborough | 1.53 | 3.97 | 5.76 |
| 16:00 | 3559 | Gap Connahs Quay vs Aberystwyth Town | 1.29 | 5.07 | 7.99 |
| 16:00 | 4026 | Denizlispor vs Altay | 2.87 | 3.31 | 2.23 |
| 16:00 | 4081 | Flint Town United vs Cardiff Met Uni. | 3.45 | 3.26 | 1.99 |
| 16:00 | 4326 | AL Ansar vs Al-Nejmeh | 2.27 | 3.21 | 2.87 |
| 17:00 | 4038 | Burton vs Derby | 2.98 | 3.33 | 2.25 |
| 17:00 | 4249 | Northeast United FC vs Chennaiyin FC | 3.46 | 3.46 | 1.92 |
| 17:00 | 4686 | Reading vs Coventry | 2.48 | 3.17 | 2.77 |
| 17:00 | 5042 | Elgin City vs Clyde | 2.43 | 3.41 | 2.53 |
| 18:00 | 1563 | Woking vs York City | 1.61 | 3.81 | 4.95 |
| 18:00 | 2174 | Dungannon Swifts vs Carrick Rangers | 3.26 | 3.40 | 2.00 |
| 18:00 | 2355 | Glentoran Belfast vs Glenavon | 1.30 | 5.07 | 7.60 |
| 18:00 | 2467 | Millwall vs Wigan | 1.87 | 3.33 | 4.08 |
| 18:00 | 2744 | Middlesbrough vs Luton Town | 1.84 | 3.52 | 3.97 |
| 18:00 | 2759 | Raith Rovers vs Morton | 2.20 | 3.41 | 2.83 |
| 18:00 | 2818 | Blackpool vs Birmingham | 2.62 | 3.22 | 2.58 |
| 18:00 | 3124 | Stoke City vs Cardiff | 2.07 | 3.27 | 3.42 |
| 18:00 | 3139 | Morocco vs Portugal | 5.41 | 3.56 | 1.65 |
| 18:00 | 3577 | Eastleigh vs Wrexham | 5.10 | 4.02 | 1.56 |
| 18:00 | 3851 | Larne vs Newry City AFC | 1.16 | 6.41 | 12.63 |
| 18:00 | 3893 | Sheffield Utd vs Huddersfield | 1.47 | 4.28 | 5.97 |
| 18:00 | 3922 | Swansea vs Norwich City | 2.38 | 3.36 | 2.76 |
| 18:00 | 4106 | Kelty Hearts FC vs Linfield Belfast | 3.35 | 3.59 | 1.91 |
| 18:00 | 4128 | Queens Park vs Montrose | 1.81 | 3.60 | 3.70 |
| 18:00 | 4444 | Lincoln vs Wycombe | 2.78 | 3.22 | 2.44 |
| 18:00 | 5474 | Portadown FC vs Ballymena Utd | 3.65 | 3.55 | 1.84 |
| 18:00 | 5763 | Newport vs Doncaster | 2.04 | 3.23 | 3.58 |
| 19:00 | 4025 | Fasil Kenema vs Dire Dawa Kenema FC | 2.28 | 2.78 | 3.31 |
| 19:00 | 5971 | Goeztepe vs Manisa BBSK | 2.17 | 3.31 | 2.97 |
| 20:00 | 1066 | Anorthosis Famagusta vs Olympiakos Nicosia | 1.56 | 4.01 | 5.62 |
| 20:00 | 1742 | Sevilla Atletico vs Xerez FC Deportivo | 2.19 | 2.82 | 3.46 |
| 20:00 | 2745 | Real Madrid Castilla vs CF Talavera De La Reina | 1.31 | 4.77 | 7.78 |
| 20:00 | 3464 | Hermanstadt vs Farul Constanta | 3.72 | 3.02 | 2.08 |
| 20:00 | 4923 | EN Paralimni vs Apollon Limassol | 4.21 | 3.56 | 1.81 |
| 21:00 | 3202 | Villarreal B vs Tenerife | 2.88 | 2.83 | 2.63 |
| 22:00 | 5771 | England vs France | 2.96 | 3.21 | 2.38 |
| 23:00 | 1711 | Zaragoza vs Huesca | 1.95 | 3.02 | 4.25 |
| 23:45 | 1656 | Oliveirense vs FC Arouca | 3.46 | 3.36 | 1.95 |

18+ CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumamosi Desemba 10, 2022
Nipashe



UKURASA 29

**Rice kamili kuibeba England vs Ufaransa**

# SIMBA YAKAMILISHA HESABU KWA EAGLE

## ●●●Mgunda asema hakuna mechi rahisi hasa wanapocheza dhidi...

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Simba kinatarajia kuikaribisha Eagle FC ya Dar es Salaam pia katika mechi ya raundi ya pili ya kuwania ubingwa wa mashindano ya Kombe la FA itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Simba inaingia katika mchezo huo ikiwa na kumbukumbu ya kutolewa kwenye hatua ya nusu fainali baada ya kukubali kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa Yanga, mchezo uliochezwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini, Mwanza.

Kutokana na matokeo ya msimu uliopita, Wekundu wa Msimbazi wanatarajiwa kucheza kwa tahadhari katika mechi ya leo na kumaliza jinamizi la kuvuliwa mataji ambalo liliwashika msimu uliopita, pia ikiwa na kumbukumbu mbaya ya kutolewa mapema na Mashujaa FC iliyokuwa ikishiriki Ligi Daraja la Kwanza katika msimu wa 2018/19.

Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, aliliambia gazeti hili jana wataingia kwa tahadhari kubwa kuwakabili Eagle FC ambao anafahamu pia wamejipanga kusaka matokeo mazuri.

Mgunda alisema mechi hiyo itakuwa ngumu kwa sababu hawafahamu wapinzani wao hivyo watahitaji kupata muda wa kuwasoma na kujua namna ya kuwashambulia.

Alisema mara kadhaa timu za madaraja ya chini zimekuwa zikiwasumbua vigogo katika mashindano yanayochezwa kwa mfumo wa mtoano, na historia hiyo mbaya imemfanya awasisitize wachezaji wake kutowadharau wapinzani wao.

"Ni wazi utakuwa ni mchezo mgumu, hatutaidharau Eagle kwa sababu ni timu ambayo pia itakuwa inahitaji matokeo chanya ili kujitengenezea jina, tutaingia kwenye mchezo huo tukiwa na tahadhari zote.

Hivi sasa tunaangalia zaidi mechi hii ili tupate ushindi na kusonga mbele, lengo letu ni kushinda mataji na hili litafanikiwa iwapo kama tutashinda kila mchezo ulio mbele yetu. Tunaenda kukutana na timu yenye malengo sawa na sisi, vijana wangu wanajua nini wanapaswa kufanya, naamini hawataniangusha, lengo letu ni kushinda ili kuweka hai matumaini ya kutwaa kombe hili," alisema Mgunda.

Aliongeza kikosi chake kinaendelea vizuri na mazoezi na kuweka wazi katika mchezo

INAENDELEA UK. 31




Kiungo wa Simba, Clatous Chama, akifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya raundi ya pili ya mashindano ya Kombe la FA itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: SIMBA SC**

## Yanga yamtamani Bruno wa Singida

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI dirisha dogo la usajili likikaribia kufunguliwa, Yanga inadaiwa kutaka kumsajili kiungo mkabaji, Bruno Gomes kutoka Singida Big Stars kwa ajili ya kukiongezea nguvu kikosi chake kitakachochuana katika hatua ya makundi ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Hata hivyo taarifa za ndani kutoka Singida Big Stars zinasema klabu hiyo yenye 'udugu' na Yanga haiko tayari kumuuza Mbrazil huyo mpaka msimu huu utakapomalizika.

Habari zilizopatikana jijini zinadai kiwango cha Bruno kimewavutia Yanga na endapo atapatikana ataongeza nguvu katika eneo la kiungo mkabaji kwa ajili ya kusaidiana na Yanick Bangala pamoja na Zawadi Mauya.

Hii ni mara ya pili kwa Yanga kuhusishwa kusajili wachezaji wa Singida Big Stars, mwanzoni mwa msimu huu kulikuwa na tetesi za timu hiyo kumtaka kiungo mshambuliaji, Dario da Silva, ambaye alionyesha uwezo mkubwa katika mechi za majaribio kabla ya msimu huu kuanza.

Akizungumza na gazeti hili, Ofisa Habari wa Singida Big Stars, Hussein Masanza, alisema klabu yao haiko tayari kumuuza mchezaji yoyote yule kwa kipindi hiki cha dirisha dogo.

Masanza alisema wao pia wanahitaji kuingia sokoni kusajili nyota wapya kwa ajili ya kukiongezea nguvu kikosi chao ambacho kimekuwa na msimu mzuri chini ya Kocha, Hans van der Pluijm.

"Hatukaribishi mazungumzo wala biashara kwa mchezaji yoyote wa timu yetu, labda huko baadaye, siyo dirisha hili la usajili, hakuna mipango hiyo na tunawataka mashabiki wa Singida Big Stars wawe na amani.

Ni jambo jema sana kuona tuna wachezaji ambao kila timu inawavutiwa nao, sisi usajili tumeufanya tukiwa na malengo

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >